Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 14 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kwa Mwaka 2002/2003 *(The Annual Report and Audited Accounts of The University College of Lands and Architectural Studies (UCLAS) for the Year 2002/2003).*

Taarifa za Mwaka za Utendaji na Hesabu Zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa Maiaka ya 2001/2002 na 2002/2003 *(The Annual Reports of the Activities and Audited Accounts of the Open University of Tanzania for the years 2001/2002 and 2002/2003).*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 236

**Ofisi za Wabunge katika Majimbo**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali kupitia Kamati ya Huduma za Jamii ilitembelea Ofisi za Wabunge na kuona hali halisi ya Ofisi hizo na kwa kuwa Majimbo mengine hayana hata Ofisi za Wabunge kama ilivyo kwa Jimbo la Mikumi.

Je, Serikali iko tayari kuwapatia fedha ili watafute Mkandarasi Majimboni na kujijengea wenyewe Ofisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilipotembelea Mikoani, pamoja na mambo mengine, ilipata fursa ya kuona jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba, kila Mheshimiwa Mbunge anapatiwa Ofisi yenye hadhi na anayoweza kuitumia vyema katika kutekeleza majukumu yake ya Kibunge. Bahati nzuri, Jimbo la Mheshimiwa Mbunge lilitembelewa na Kamati iliarifiwa kwamba, Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge ipo katika Jengo la Katibu Tarafa wa Tarafa ya Mikumi, Wilaya ya Kilosa. Ndio maana Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa kwa sasa Waheshimiwa Wabunge wengi wanazo Ofisi katika majengo ya Serikali kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, ambazo zinahudumiwa na Mamlaka za Mikoa zimekuwa zikitengewa fedha kwa ajili ya ukarabati na kuweka samani ili kuziboresha na kuziimarisha. Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mikumi, lilitengewa Sh.1,500,000/= mwaka 2003/2004 kwa ajili hiyo. Aidha, kama Bunge lako Tukufu lilivyoarifiwa wakati wa kuwasilishwa hoja ya kuliomba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake na yale ya Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2004/2005, Serikali ilisisitiza kwamba, Ofisi za Waheshimiwa Wabunge Majimboni, zitaendelea kuimarishwa hatua kwa hatua kwa kuendelea kutenga fedha katika Bajeti kupitia Mamlaka za Mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, taarifa zaidi juu ya Ofisi za Waheshimiwa Wabunge na fedha zilizotengwa itatolewa na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ambayo nayo ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi kadhaa za Waheshimiwa Wabunge Mikoani na ninavyofahamu, hivi sasa inaandaa taarifa hiyo ili iwasilishwe na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Aah, mimi ndiyo mwenye swali hapa!

**SPIKA:** Alikuwa hajasimama! Mwuliza swali la msingi, Mheshimiwa Christopher Wegga. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Ni kweli nilikuwa nimesemama, lakini ndiyo umbile langu nilivyo. *(Kicheko)*

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kujibu swali langu vizuri, lakini nataka tu apokee ufafanuzi kwamba taarifa anazopata si sahihi. Sielewi kwamba anazipata kwenye Kamati ya Bunge au kwa Makatibu Tarafa au *RAS* au *DAS?* Nimfahamishe tu kwamba Jumamosi nilikuwa Kilosa kufuatilia shughuli za Jimbo nikaangalia na Ofisi, Ofisi hiyo haiko Mikumi imekarabatiwa ya Kilosa Mjini.

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Sasa niombe tu kwamba, je, huo ndiyo utaratibu wa kutoa maelekezo kwamba ukarabati wanakwambia uko Mikumi wakati uko Kilosa Mjini? Je, anakubaliana na mimi sasa kwamba atapeleka hela atengeneze Ofisi Mikumi? Kwa sababu Ofisi nyingi zimekarabatiwa nje ya Majimbo yenyewe na nia ya Majimbo ilikuwa ni kusogeza huduma za Wabunge karibu na maeneo na wananchi, Sasa atakubaliana nami kwamba arekebishe Majimbo yote yaliyokosewa kama mimi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, taarifa nilizozitoa hapa nimepewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na baadaye mchana huu nitampa Mheshimiwa Christopher Wegga ili tuangalie kama ni ukweli au uongo wa taarifa hiyo. Nitampa aone maana mimi ni lazima niwasiliane na Mamlaka za Mikoa zilizopo. Nimeambiwa Ofisi ya Mheshimiwa Mbunge imetengewa shilingi milioni moja na nusu na Ofisi yake iko kwa Katibu Tarafa Mikumi. Kwa hiyo, kama kuna tofauti ya taarifa, niko tayari kushirikiana naye ili tuweze kusahihisha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi juu ya suala lake la pili. Maelekezo tuliyoyatoa Mikoani ni kwamba, kwa sasa Serikali haina uwezo wa kujenga Ofisi mpya za Waheshimiwa Wabunge. Tulikubaliana kwenye Tume yetu ya Huduma za Bunge kwamba, Ofisi hii itayarishe mpango wa muda mrefu. Kwanza, tulitayarisha michoro inayofaa kwa ajili ya *structure* za Wabunge ili ikiwezekana hatua kwa hatua, Bunge lenyewe lisimamie ujenzi wa Ofisi hizo. Kwa sasa tumeamua kuomba fedha kwa ajili ya kujenga majengo ya Makao Makuu ya Bunge Zanzibar na hapa Dodoma

**SPIKA:** Na Dar es Salaam.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Na Dar es Salaam.

Lakini kwa sasa wakati tunasubiri uwezo mwingine wa kuanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Bunge, tumeelekeza Mikoa kwamba popote pale ambapo pana jengo la Serikali, Mbunge aruhusiwe kulitumia jengo la Serikali lolote lililopo katika jimbo lake. Iwe ni Ofisi ya Kata, iwe ni Ofisi ya Tarafa, iwe ni Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, iwe ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Bajeti yote inayotengwa kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge itumike bila kujali jengo hilo liko wapi ili mradi ni la Serikali. Kama ni jengo la Serikali katika ngazi yoyote, fedha zinaweza zikatumika kukarabati jengo hilo na kununua samani. Kama Mheshimiwa Mbunge amepanga nyumba ya mtu binafsi hatuwezi kukarabati, lakini samani zinaweza zikanunuliwa kwa sababu zitaondosheka pindi Mheshimiwa Mbunge atakapomaliza kipindi chake.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia nina swali moja.

Ni lini Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itafika Zanzibar kuona Ofisi za Wabunge ambazo ziko chini ya miembe, minazi na magari yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo jukumu nimelikabidhi kwa Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, siyo Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tusubiri taarifa yake.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, enhee Mheshimiwa Semindu Pawa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Kanuni ya Bunge Na. 50, Toleo la mwaka 2004. Jibu alilolitoa Mheshimiwa Waziri lilikuwa tofauti na Mbunge na ndivyo ilivyo hivyo hivyo katika Majimbo yetu. Katika hotuba yake ilisema kwamba, Ofisi za Wabunge ziko katika Tarafa, kwa mfano, Ngerengere na Mikumi na maeneo mengine ya Wabunge. Leo amesema kwamba ziko Wilayani, Makao Makuu ya Wilaya, pamoja na ya kwangu. Ni lazima awe na uhakika na majibu haya, je, tunachukua hatua gani kwa kauli hii? Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, nimesema tangu mwanzo aliponiuliza Mheshimiwa Christopher Wegga, utaratibu wa Serikali tunapata majibu au tunawasiliana katika *structure* za Serikali na majibu haya mimi ninayoyasema ninazo taarifa za nchi nzima, kila Wilaya na taarifa zake na taarifa hiyo nimepewa na imeunganishwa na Ofisi ya TAMISEMI na nimemkabidhi Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwa kujua kwamba itamsaidia kuoanisha taarifa halisi kutokana na ziara aliyoifanya na taarifa nilizopata mimi Mkoani. Ndiyo maana nimesema taarifa itawasilishwa na Mheshimiwa Eliachim Simpasa hapa Bungeni na tutaijadili.

Lakini kwa majibu ya Mheshimiwa Christopher Wegga, ambayo mimi nimeandikiwa kama Waziri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, nimesema nitampa na baada ya hapo tukiona kuna taarifa za uongo au mimi nimedanganywa, tutashughulikia pamoja. Nimesema hapa mwanzo. *(Makofi)*

Na. 237

**Vituo vya Afya kwa Kila Tarafa**

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE** aliuliza: -

Kwa kuwa ni Sera ya Serikali kwamba kila Tarafa iwe na Kituo cha Afya: -

(a) Je, kwa nini Tarafa ya Kasanda katika Jimbo la Buyungu haina Kituo cha Afya mpaka sasa?

(b) Kwa kuwa akina mama wengi hasa wa kutoka Kata ya Gwanumpu, hufariki wakiwa wamebebwa kwenye machela wakipelekwa Hospitali ya Wilaya kwa sababu hakuna magari hata ya biashara katika eneo hilo, je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya kuunganisha Kijiji cha Bitare na Katanga ili kupunguza mzunguko kupita Mngunzu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Ruzuba Magayane, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua adha wanayoipata wananchi kwa kukosa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Kasanda. Kwa kutambua hilo, Serikali kupitia Wizara ya Afya, imekwishafanya upembuzi wa ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kijiji cha Gwanumpu katika Tarafa ya Kasanda. Kutokana na ufinyu au ukomo mdogo wa Bajeti, Halmashauri ya Wilaya imeshindwa kutenga fedha za ujenzi kwa mwaka 2004/2005. Hata hivyo, taratibu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo hiki zinaendelea na inatazamiwa kiasi cha Shilingi milioni 60 zitaombwa kwenye Bajeti ya mwaka 2005/2006 ili ujenzi uweze kuanza. Kwa hiyo, wananchi wa Tarafa ya Kasanda tunaomba waendelee kuhamasishwa ili waweze kuchangia kwa hali na mali ujenzi wa Kituo hiki wakati taratibu hizo zinakamilika. Kituo hiki kitakapokamilika kitahudumia Vijiji vya Kasongati, Kasanga, Gwanumpu, Bukirilo, Kasanda, Kazilamihunda, Irabiro, Magunzu, Kiduduye na Nyangwijima vyenye jumla ya wakazi 62,060.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kupunguza au kuondoa tatizo la vifo vya akina mama ambao hufariki kwa sababu ya tatizo la usafiri hadi kwenye Hospitali ya Wilaya, Serikali itajenga barabara inayounganisha Vijiji vya Bifare hadi Katanga. Kazi hii itafanyika katika mwaka wa fedha huu wa 2004/2005 kutokana na fedha za Mfuko wa Barabara na itagharimu Sh.36,300,000/=.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri ya kutia moyo. Nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kutumia fedha za *Basket Fund* kusaidia hospitali binafsi pale zilipo baada ya kutimiza baadhi ya masharti na kwa kuwa katika Wilaya ya Kibondo tuna hospitali mbili za Kabale na Keza ambazo ni za binafsi. Je, katika kipindi hiki cha mpito, Serikali inaweza kuzisaidia hospitali hizi za Kabale na Keza ili zipande hadhi na waweze kuwasaidia pesa kupitia Mfuko wa *Basket Fund? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, siku za karibuni nilijibu swali lingine katika kujaribu kufafanua juu ya suala hili ambalo Mheshimiwa Beatus Magayane ameliulizia na nilieleza kwamba, inapokuwa sasa unapenda hospitali ambayo si ya Serikali iweze kuingizwa katika utaratibu ni suala tu la kuwasiliana na Halmashauri ili iweze kuwasilisha rasmi maombi hayo kwenye Wizara ya Afya ili utaratibu utazamwe kama linawezekana au haliwezekani. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Beatus Magayane, labda tushirikiane kulifanya hilo wakati tunasubiri utaratibu huo mwingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, subira kuna majibu ya nyongeza kutoka Serikalini. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa niongezee kwenye majibu ya Naibu Waziri wa TAMISEMI kama ifuatavyo: Mfuko wa *Basket Fund* una mgawanyo wake ambao umeelekezwa kwa Wilaya zote. Utaratibu uliopo sasa ni kuzipatia hospitali ambazo tunaziita *Voluntary Agencies* au *VAs* ni zile hospitali ambazo ni za Mashirika ya Dini ili ziweze kutoa huduma iliyokuwa bora zaidi. Hivi sasa hospitali hizo zinapatiwa asilimia 10 ya fedha zinazokwenda kwenye Mfuko wa *Basket.* Kwa hiyo, kama hospitali au zahanati anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni hizo za Mashirika ya Dini, basi wanaweza kuingizwa humo, lakini kama ni za binafsi kabisa, za faida, kwa kweli utaratibu huo kwa sasa haupo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, endelea na swali lako.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Gwanumpu kama alivyosema haina Kituo cha Afya na kwa kuwa iko mbali sana na hizi hospitali hata hospitali za watu binafsi kama ile ya Keza. Je, Serikali itakuwa tayari kuikarabati Zahanati ya Bukirilo ambayo iliharibiwa sana na wakimbizi na haina madawa? Je, itakuwa tayari kuwaongezea madawa na kuwaongezea wafanyakazi kusudi iweze kusaidia akina mama wanaoteseka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tumepokea rai yake, nitajaribu kuliwasilisha

kunakohusika tuone kama hilo linawezekana kwa bajeti ya sasa au hata pengine ya mwaka kesho.

Na. 238

**Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza: -

Kwa kuwa hivi karibuni Manispaa ya Kinondoni imeanzisha mpango wa kuwaajiri Maafisa Watendaji katika ngazi ya Mitaa na Vijiji kwa lengo la kuimarisha utendaji na ukusanyaji wa mapato ya Manispaa:-

(a) Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa Halmashauri za Miji na Manispaa ili kuboresha utekelezaji wa zoezi hilo?

(b) Je, Serikali Kuu ipo tayari kutoa ruzuku kwa Halmashauri za Miji na Manispaa ili kuwezesha kulipa mishahara kwa Maafisa watakaoajiriwa?

(c) Kwa kuwa katika ngazi hizo Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji wanafanya kazi kubwa katika mazingira magumu na hata hizo asilimia tatu za makusanyo ya kodi mbalimbali huwa hawarejeshewi kama posho yao, je, Serikali haioni kuwa badala ya kuwaajiri Watendaji wa Mitaa na Vijiji ni bora iwape posho Wenyeviti ili iwe motisha kwa lengo la kuwapunguzia makali ya maisha na hivyo kuboresha utendaji wa kazi zao za kila siku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa Kauli Bungeni kuhusu ajira ya Watendaji wa Vijiji tarehe 9 Februari, 2004. Tamko lilielekeza kuwa Watendaji wa Vijiji wataendelea kuwepo kazini kwa kupatiwa Mkataba wa miaka mitatu. Halmashauri zote ziliagizwa na baadhi zimetekeleza zoezi hili kwa kuingia Mikataba na Maafisa Watendaji wa Vijiji ambao tayari walikuwa kazini na nyingine bado zinaendelea kukamilisha zoezi hilo. Maafisa Watendaji hao pia wamepatiwa mafunzo ya awali ya wiki mbili. Ajira ya Watendaji wa Mitaa kwa kuwa ni ajira mpya ilipangwa kuanza mwezi Julai, 2004. Serikali tayari ilikwishatoa maelekezo kuhusu utaratibu wa ajira hizi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali ilitenga jumla ya Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kutoa mafunzo na ajira za Watendaji wa Vijiji na Mitaa na katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, Sh.5,900,000,000/= zimetengwa kwa ajili hiyo. Fedha hizi ni kidogo kuliko mahitaji halisi ya kuwaajiri Watendaji wote wa Vijiji 10,200 na Watendaji wa Mitaa 2,666 ambapo jumla ya

Sh.16,381,291,800/= zinahitajika pamoja na kutoa mafunzo. Kwa hiyo, Ofisi yangu inaendelea kuwasiliana na mamlaka husika juu ya suala hili ili tuweze kulipatia ufumbuzi. Aidha, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kuwa, ajira ya watumishi hawa zitaendelea kufanywa na Halmashauri zenyewe kwa kuzingatia taratibu zote zinazotakiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji wanafanya kazi kubwa ya kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Kwa kutambua jambo hilo, Serikali kwa kupitia Tangazo la Serikali Na.3 la tarehe 7 Januari, 1999, lilielekeza Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kulipwa si chini ya asilimia tatu ya makusanyo ambayo yeye amehamasisha. Pamoja na baadhi ya vyanzo vya mapato kufutwa, bado Halmashauri zinapaswa kuendelea kutoa posho hiyo kutokana na vyanzo vilivyobakia na pia ruzuku inavyotolewa na Serikali ambayo inafidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu, kuendelea kuziasa Halmashauri zote kuzingatia tangazo hilo kwa kuhakikisha kwamba, utaratibu huo unaendelezwa kwa kadri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuajiri Watendaji wa Mitaa na Vijiji ni kuimarisha Uongozi katika ngazi husika. Hivyo, Serikali itaendelea na azma yake hiyo na haioni kwamba ni jambo lenye mantiki kufuta ajira zao ili mishahara yao itumike kulipa posho kwa ajili ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa vile tangu mwaka 1995 Wenyeviti wa Serikali za Mitaa hawajapata hiyo posho ya asilimia tatu kama Serikali ilivyoagiza, je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kwa hilo? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, maelekezo ya Serikali yalikuwa wazi kwa kila Halmashauri na ilikuwa ni jukumu la kila Halmashauri kuhakikisha wanatekeleza maagizo haya. Ziko Halmashauri ambazo zimetekeleza na hatukupata tatizo, lakini ziko Halmashauri vile vile ambazo hazikutekeleza na hizi muda wote tumeziagiza zihakikishe kwamba, zoezi hilo linafanyika, lakini pengine tusaidiane tu kwa sababu wote tunashiriki katika Vikao hivi ili tuweze kuzibana Halmashauri hizo kutekeleza maagizo haya ya Serikali.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Watendaji wa Mitaa na wa Vijiji ni watu wenye majukumu ya kifamilia na ya kijamii na kwa kuwa kutokuwalipa mishahara yao kwa wakati ni kuwafanya washawishike zaidi katika kudokoa kile kidogo kinachokuwepo. Je, Waziri

anaeleza nini kwamba Watendaji wengi katika Manispaa ya Kinondoni na hata kwenye Miji na Manispaa nyingi hawajalipwa tangu walipoajiriwa na tangu agizo la kuwarudisha kazini lilipotolewa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa kwamba, kwa mwaka 2003/2004, Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuwalipa Watendaji wa Vijiji ambao tulikuwa tumeamua waajiriwe pamoja na Watendaji wa Mitaa. Zoezi hilo lilifanyika na wale ambao tulikuwa tumewaajiri walilipwa kuanzia Bajeti iliyopita mwezi Mei, 2004. Sasa inawezekana kabisa kwamba, katika baadhi ya maeneo bado wanasuasua, tutahakikisha hili jambo linatekelezwa kikamilifu mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Na. 239

**Uchomaji Moto Kwenye Maeneo Mbalimbali Nchini**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania inasifika kwa utulivu, amani na upendo ndani ya jamii; na kwa kuwa kupata taarifa za kuchomwa moto kwa Mashule, Makanisa, Mabanda ya Sokoni na ya Wafanyabiashara ndogo ndogo huko Moshi na Arusha, Ikulu Dar es Salaam, ujambazi na mabomu, limekuwa ni jambo la kawaida ndani ya masikio yetu hapa nchini; na kwa kuwa zana zinazotumika mara nyingi zimeonyesha ni za Kijeshi:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti za kumaliza matatizo ya uhalifu huo unaotishia amani na maisha ya wananchi?

(b) Kama kila siku watu wamekuwa wakifa katika ajali, vibaka kuchomwa moto, watu wanauawa na wezi/majambazi, je, ni nini tasfiri ya amani tunayozungumzia?

(c) Kulingana na takwimu za matukio hayo ya wizi, ujambazi, mauaji ya vikongwe, vibaka wanaochomwa moto, ajali mbaya za Baharini/Ziwani na barabarani, je, ni nchi gani nyingine katika Bara la Afrika inayotufikia au kutuzidi kwa uhalifu, ajali na mikosi ya aina hiyo na ufumbuzi wake ni nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, yapo matukio kadhaa ya uhalifu yaliyojitokeza katika kipindi hiki, lakini matukio hayo yamekuwa yakidhibitiwa kwa nguvu zote za vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kuwa hali ya amani na usalama inadumishwa hapa nchini.

Kuhusu matukio ya moto, katika kila tukio Serikali hufanya uchunguzi kwa kushirikisha wadau na wataalam mbalimbali. Hadi sasa uchunguzi katika matukio mbalimbali umebaini kuwa hapakuwepo na hujuma, bali chanzo kimekuwa ama hitilafu ya umeme au visababishi vinginevyo vya bahati mbaya. Serikali inachukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hili ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa majengo na kutoa ushauri namna ya kujikinga na janga la moto kwa kuweka viashiria moto, yaani *fire detectors,* kutoa elimu kwa umma kuhusu njia za kinga ya moto na namna ya kutumia zana ndogo ndogo za kuzima moto pindi ukitokea. Aidha, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuviimarisha Vikosi vya Zimamoto hasa katika kuwapatia vitendea kazi, mafunzo na vifaa vya kujikinga na moto.

(b) Mheshimiwa Spika, tasfiri ya amani inayozungumziwa hapa nchini ni pamoja na kuwepo kwa utaratibu imara wa kisheria unaotambulika na kuheshimika na watu wote ambao unawezesha kero za wananchi kufuatiliwa na kutatuliwa. Aidha, nchini mwetu hamna mapambano ya wazi au ya chini chini baina ya vikundi, makabila, Vyama vya Siasa na kadhalika, badala yake nchi yetu inasifika kuwa na umoja wa Kitaifa, upendo na mshikamano wa wananchi bila kujali tofauti zetu za dini, makabila wala rangi ya mtu. Hii ndiyo tasfiri ya amani ya nchi yetu ambayo ni nadra kupatikana katika nchi nyingine Barani Afrika na kwingineko duniani na ndiyo maana Tanzania imekuwa kimbilio la wakimbizi kutoka nchi mbalimbali.

(c) Mheshimiwa Spika, uhalifu upo katika kila nchi duniani bali hutofautiana katika aina na viwango. Kwa takwimu zilizopo, kiwango cha uhalifu hapa nchini ni kidogo ikilinganishwa na hali ya uhalifu ilivyo katika nchi zinazotuzunguka za Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika na kwingineko Barani Afrika. Kwa sababu hii, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane na Serikali katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulinda, kudumisha na kuimarisha amani tuliyonayo hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa matukio ya moto husababisha kupotea kwa mali nyingi na roho za watu; na kwa kuwa wahusika ni *innocent,* yaani kama watoto wa shule wanakuwa *innocent;* na kwa kuwa mpaka sasa hivi hawajawahi kukamatwa, hatujapata taarifa za kukamatwa tunaambiwa tu moto umeunguza kutokana na hitilafu za umeme na vitu mbalimbali; je, Serikali haioni haja ya kufidia watu kama hao?

(b) Kwa kuwa mambo ya moto ni ya muda mrefu kuanzia miaka zaidi ya 10 iliyopita kuunguza kwenye mashule hasa Kilimanjaro kama Shauritanga, Machame, Marangu, Stendi ya Moshi, Stendi ya Arusha na kwa kuwa watu wengi wamekuwa hawana uhakika na hawana imani kwamba unatokea kwa njia hiyo ya umeme kwani kwa mfano Stendi ya Moshi...

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Kwa kuwa ...

**SPIKA:** Aaah! 'Kwa kuwa' siyo swali.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Je, Serikali haioni kwamba kuna mkono wa mtu wenye kuunguza vitu hivyo, kwa sababu lawama zinakwenda Serikalini?

**SPIKA:** Sawa, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, mpaka sasa katika uchunguzi ambao umefanyika haijaonekana kwamba kuna mtu amefanya kitendo hicho kwa hujuma na kama Mheshimiwa Mbunge anazo taarifa za hakika kwamba kuna mkono wa mtu, basi atupatie na huyo mtu, tunamtafuta huyo mtu vile vile. *(Makofi)*

Kuhusu fidia, kama nilivyosema hii mioto hii kwanza ni mingi sana katika nchi nzima na inatokea kwa bahati mbaya kabisa. Kwa hiyo, kwamba Serikali itamfidia kila mtu anayepata tatizo la moto Serikali, siyo rahisi ni ajali tu kama ajali zingine. Isipokuwa kama alivyowahi kusema hapa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwamba, kwa ile mioto inayotokea kwa hitilafu ya umeme, ikidhihirika kwamba umeme ule hitilafu yake ilitokea *TANESCO* haikusababishwa na wewe umefanya *wiring* vibaya bali imesababishwa na umeme wa *TANESCO,* katika mazingira hayo fidia inaweza ikatolewa. *(Makofi)*

Na. 240

**Kituo cha Polisi cha Dunga - Unguja**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Dunga - Unguja kimejengwa kwa msaada wa Wahisani hadi kukamilika na kwa kuwa kuta za kituo hicho sasa zimepata nyufa na zinaweza kubomoka na kuleta hatari kwa watumiaji:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kutengeneza kituo hicho kabla hakijaathiri wafanyakazi waliopo kituoni hapo?

(b) Je, kuviachilia vituo ambavyo tumepata misaada kwa wahisani hadi kufikia kutaka kuanguka si njia mojawapo ya kuwavunja moyo wale waloitusaidia?

**NAIBU WAZIRI WAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wahisani wote waliochangia ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Dunga. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuhamasisha hao wahisani ambao walijenga hicho kituo. Hivi sasa Serikali inakabiliwa na tatizo la majengo mengi ya vituo vya Polisi kuwa katika hali mbaya kutokana na uchakavu na hii ni pamoja na majengo ya kituo cha Dunga - Unguja. Majengo haya hayafanyiwi ukarabati mapema kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa mujibu wa sera ya ujenzi wa vituo vidogo vya Polisi, tunawaomba viongozi na wananchi wa Jimbo la Chwaka, waanze kazi ya ukarabati wa jengo hilo na Wizara yangu itawaunga mkono.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kama alivyosema, Vituo vinavyohitajika kujengwa na kukarabatiwa ni vingi katika nchi yetu; na kwa kuwa alisema kwamba atatuunga mkono; je, muda gani anatazamia au kufikiria kituo hicho kitaanza kukarabatiwa ili kutuunga mkono katika Kituo cha Dunga?

**NAIBU WAZIRI WAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu lini tutaanza kuwaunga mkono kama nilivyosema, kilio na mwenyewe, kwa hiyo, wakati wowote mkianza hata kama ni kesho, sisi tuko tayari kuwaunga mkono na hata katika Bajeti yetu mliyoipitisha jana, kuna kipengele mle ambapo tumetoa ahadi pale ambapo wananchi wanaonyesha juhudi zao za kujenga Kituo cha Polisi au nyumba za polisi, tutawaunga mkono. Kwa hiyo, Chwaka wakati mkianza na sisi hapo hapo tutaanza kuwaunga mkono.

Na. 241

**Barabara ya Nyashimo - Dutwa na Lamadi - Sapiwi**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara za Nyashimo - Ngasamo - Dutwa na ile ya Lamedi - Mkula - Sapiwi inaunganisha Mikoa mitatu ya Mwanza, Shinyanga na Mara na kwamba barabara hizo zina umuhimu wa pekee ikiwa ni pamoja na kusafirisha bidhaa mbalimbali za mazao na mifugo na wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia matengenezo makubwa na ya kudumu ili ziweze kuhimili wingi wa magari, tofauti na matengenezo yanayofanyika sasa ambayo hayakidhi mahitaji halisi ya barabara hizo?

(b) Je, Serikali haioni pia ipo haja ya kuyadhibiti magari makubwa na yenye uzito mkubwa, yaani zaidi ya tani 10, kutumia barabara hizo ambazo zimejengwa kwa kiwango hicho?

(c) Je, ni kwa namna gani wananchi wa maeneo husika wanaweza kushirikishwa katika udhibiti huo ili kuepusha uharibifu unaosababishwa na madereva kwa kutokuheshimu sheria husika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara za Nyashimo - Ngasamo - Dutwa kilometa 46 na ile ya Lamadi - Sapiwi kilometa 16 ni barabara za Mkoa zinahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Barabara hizi zimekuwa zikifanyiwa matengenezo makubwa *(Spot Improvement)* kwa kiwango cha changarawe na kuzifanya zipitike kwa wakati wote. Ni kweli kuwa, kwa sababu ya uzuri wa barabara hizi, magari yanayotumia barabara hizo yameongezeka. Matokeo yake ni kuwa, barabara hizi zinaharibika mapema. Wizara yangu itaendelea kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara barabara hizi kwa kiwango cha changarawe ili ziweze kupitika hadi pale fedha za kujenga barabara hizi kwa kiwango kikubwa kinachokidhi zitakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli magari mazito yanayotumia barabara yanapelekea kuharibika haraka kwa barabara hizi, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* imeweka alama za kuzuia magari mazito ya zaidi ya tani 10 kutumia barabara hizi. Kwa kuwa bado kuna wakorofi wachache wanaopitisha magari mazito, Wizara yangu inaomba ushirikiano wa wananchi wanaoishi maeneo ya jirani na barabara hizi, kutoa taarifa kwa Uongozi wa Wilaya na *Police Traffic* mara wanapoona magari haya mazito yanapita katika barabara hizi ili sheria ichukue mkondo wake.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la sehemu (b), Wizara yangu inaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge katika kuwahamasisha wananchi waishio maeneo ya barabara zote, kutoa taarifa Polisi mara waonapo magari mazito kuliko kiwango kinachoruhusiwa yanatumia barabara hizi ama nyingine zozote nchini.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa tatizo la magari yenye uzito kupindukia lipo sehemu nyingi nchini na hata katika barabara ya Busisi/Nyahorongo magari yanayotoka Kahama kupitia barabara hiyo na kuharibu daraja la Ligembee katika Jimo la Nyang'hwale na kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri anasema wananchi wakiona watoe taarifa Polisi. Je, Waziri anasemaje kwenye sehemu ambako hakuna Vituo vya Polisi au vipo mbali, wananchi wachukue hatua gani, anaruhusu Sungusungu wachukue nafasi ya Polisi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la awali, nimesema wananchi watoe taarifa kwenye uongozi ama *Police Traffic,* pale ambapo Polisi hawapo na sidhani kama kuna Wilaya ambayo haina Polisi lakini pale ambapo polisi hawapo kwenye Wilaya hiyo, basi uongozi ambao unasimamia Utawala Bora wa sehemu hiyo upewe taarifa ili hatua za Serikali zichukuliwe. Sungusungu wasichukulie madaraka mikononi wakaanza kubamiza watu makofi. *(Makofi)*

Na. 242

**Uingizaji wa Sukari kutoka Malawi**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa sukari inayozalishwa na viwanda vyetu hapa nchini haitoshelezi mahitaji kwa baadhi ya maeneo ya nchi, kama ilivyo kwa Mikoa ya Kusini na Kusini Magharibi ambayo haipati kahbisa bidhaa hiyo, jambo linalopelekea wafanyabiashara ndogo ndogo kuvuka mipaka na kuingia nchini Malawi kuchukua sukari kwa ajili ya biashara ndogo ndogo:-

(a) Je, kwa nini Serikali haiwashukuru na kuwapongeza wafanyabiashara hao wadogo wadogo wanaoingia nchini Malawi kuchukua kiasi kidogo cha sukari, badala yake, Serikali kupitia *TRA,* inawabughudhi vijana hao na kuwapokonya sukari hata kama ni kilo 10 za matumizi ya nyumbani, kwa kisingizio cha kutolipia ushuru wa forodha?

(b) Je, katika mwaka 2002, Serikali ilipata fedha kiasi gani kutokana na sukari iliyopokonywa kutoka kwa vijana hao wafanyabiashara ndogo ndogo?

(c) Je, Serikali inamsaidiaje mfanyabiashara kama huyo anayevuka mpaka wa nchi kuchukua sukari kiasi kidogo tu kama kilo 20 kwa ajili ya biashara ndogo kwenye kibanda chake ambacho anawajibika kulipia ushuru/kodi kwenye Halmashauri yake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Maafisa wa Forodha wanafanya kazi yao kufuatana na maagizo ya Sheria ya Sukari Na. 26 ya mwaka 2001 *(Sugar Act No.26 of 2001),* kwa mujibu wa vifungu Na. 7 na 16 vya Sheria hiyo, kila mwagizaji wa sukari anatakiwa kuwa ameandikishwa na Bodi ya sukari na awe na leseni ya uingizaji wa sukari. Hivyo, wafanyabiashara wote wakiwemo wale wa Kyela wanapaswa kufuata sheria hiyo. Kwa hali hiyo, Serikali haiwezi kuwapongeza wafanyabiashara wa Kyela kwa ajili ya uingizaji wa sukari kutoka Malawi kinyume cha Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2002 Serikali Mkoani Mbeya ilikusanya jumla ya Sh.20,488,000/= kutokana na kuuza sukari iliyokamatwa. Fedha hizo siyo kodi bali mauzo ya sukari iliyoingizwa nchini kibiashara bila kibali na siyo kilo 10 au 20 kwa matumizi ya nyumbani. Sukari hiyo iliuzwa kwa taasisi za umma kama shule, jeshi na kadhalika.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na Sheria ya Sukari Na. 26 ya mwaka 2001, iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, Serikali haina jinsi ya kumsaidia mfanyabiashara

ndogo ndogo anayevuka mpaka kwenda nchi jirani kuchukua sukari kidogo kwa ajili ya biashara kwenye kibanda chake ambacho anawajibika kulipia ushuru/kodi kwenye Halmashauri yake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, kama nilivyosema, uingizaji wa sukari nchini kinyume cha Sheria Na. 26 kifungu Na. 7 na 16 umezuiliwa.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa hali ya Kyela ndiyo hiyo hiyo inayonipata na mimi kule Tunduma; na kwa kuwa tuliambiwa kwamba kuna *depot* ya sukari inayotoka Kilombero na sehemu nyingine zote kuelekea Mbeya na hapa hapa tukajibu tukawaeleza hiyo *depot* ya sukari ambayo inatoka huku kwenda kule kwetu haipo kule na kwa hiyo sasa nauliza Serikali sasa kama haitatambua mchango wa hawa vijana wanaotusaidia, itatusaidia kuleta sukari ya kutosha kujaza Mkoa wa Mbeya ambao kwa kweli mimi katika umri wangu huu sijawahi kwenda kununua sukari ya kwetu kwenye duka lolote katika eneo letu, haijapatikana sukari yoyote ya Tanzania kule kwetu, itatuhakikishia leo kwamba itajaza sukari kutoka Kilombero au kutoka wapi katika Mkoa wa Mbeya kule Tunduma na Kyela? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, nilidhani ni swali la Wizara ya Kilimo na Chakula hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, nilipotembelea Tunduma nilifuatana na Mheshimiwa Mbunge na tuliangalia tatizo la uingizaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nchi jirani ikiwemo sukari.

Mheshimiwa Spika, hawa waliokamatwa ni wale walioingiza sukari nyingi kibiashara bila kibali. Lakini tatizo la Tunduma ni kwamba, mpaka wa nchi hizi mbili haujulikani sawa sawa kwa maana kwamba, unaweza ukakuta nyumba *sitting room* iko Zambia na *bedroom* iko Tanzania na maduka yale yaliyoko kule wananchi wanakwenda kununua kilo moja moja na kutumia nyumbani. Lakini hao tunaowazungumzia ni wale wanaokwenda kununua sukari nyingi kibiashara na kuiuza bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mazungumzo na wazalishaji wa sukari wa hapa nchini ili wapeleke sukari nyingi katika Mikoa ya Kusini na hilo wanalitekeleza na mipango inafanyika zaidi ili *depot* hizo ziweze kupelekewa sukari na sukari hii ya Tanzania iweze kuwa nyingi kama ambavyo wananchi wa Kusini wanahitaji.

Na. 243

### *Quasi Financial Institutions*

**MHE. ROBAERT K. MASHALA (k.n.y. MHE. LEONARD N. DEREFA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mashirika kama *NIC, LAPF, PPF* na *NSSF* ni kama aina ya mabenki *(Quasi Financial Institutions):-*

(a) Je, kwa nini Benki Kuu haijihusishi kudhibiti shughuli za mashirika hayo ili kuwalinda wateja wanaowekeza katika mashirika hayo kama inavyofanya kwa mabenki mengine?

(b) Je, ni nani hasa anayehusika kudhibiti shughuli za uwekezaji katika mashirika hayo ambao unasababisha baadhi yake kushindwa kulipa wateja wake kama vile *NIC?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya mabenki na taasisi za fedha ya mwaka 1991, pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1995, Benki Kuu pamoja na mambo mengine, inatakiwa kukagua na kuratibu shughuli za mabenki na taasisi za fedha zinazojishughulisha na biashara ya kibenki *(Banking Business).*

Kwa upande wa mifuko ya hifadhi ya jamii, Sheria zilizoanzisha mifuko hii, zinatamka kwamba, kila mfuko utasimamiwa na kudhibitiwa na Bodi za Wadhamini kwa niaba ya wanachama. Kwa mfano, Mfuko wa *LAPF* husimamiwa na kudhibitiwa na Bodi ya wadhamini chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mfuko wa *NSSF* husimamiwa na Bodi ya Wadhamini chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Mifuko ya *PSPF* na *PPF* inasimamiwa na Bodi ya Wadhamini chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Shirika la Bima la Taifa na makampuni mengine ya Bima husimamiwa na Idara ya Bima chini ya Kamishna wa Bima. Idara hii iliundwa chini ya Sheria ya Bima Na. 18 ya mwaka 1996, ambayo inatamka wazi kuwa mwenye jukumu la kuratibu na kusimamia shughui za Bima nchini ni Idara ya Bima *(Insurance Supervisory Department),* ambayo ipo chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli za mifuko ya *LAPF, NSSF, PPF* na *PSPF* siyo ya kibiashara za kibenki, Benki Kuu haina mamlaka kisheria, kusimamia udhibiti wa mashirika hayo. Hivyo, mifuko hii husimamiwa kulingana na sheria zilizoiunda.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, sheria za mifuko ya pensheni zinatamka kwamba, mifuko ya hifadhi ya jamii, inasimamiwa na kudhibitiwa na bodi za wadhamini kwa niaba ya Serikali na wanachama wake. Hivyo, usimamizi na udhibiti wa

shughuli za uwekezaji katika taasisi hiyo unafanywa na Bodi za wadhamini chini ya Wizara mama husika.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri amesema kwamba, hii mifuko si ya kibiashara ingawa inafanya kazi za kibiashara pamoja na kukopesha watu wakalipa. Hafikiri kwamba hiyo ni sababu ya kutosha kabisa kuingiza haya mashirika yasimamiwe na Benki Kuu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, sheria zinazosimamia uendeshaji wa mifuko hii ni zile zilizoundwa ama zilizopitishwa na Bunge lako ambazo zinasema kwamba, inasimamiwa na kudhibitiwa na Bodi za Wadhamini kwa niaba ya Serikali. Mifuko hii haifanyi shughuli za kibiashara za kibenki. Lakini kwa sababu Bodi hizi zinasimamia kwa niaba ya Serikali, kwa hiyo, mahali popote ambapo kunakuwa na matatizo ya uendeshaji, Serikali inaingilia kati. Lakini uendeshaji wa siku hadi siku uko chini ya Bodi za Wadhamini. Lakini Bodi za Wadhamini zinafanya kazi kwa niaba ya Serikali. Kwa hiyo, mahali ambapo kunakiukwa taratibu na kuna matatizo makubwa ambayo yanashindwa kutatuliwa na Bodi hizi, Serikali inaingilia kati na inafanya maamuzi kwa niaba ya wanachama na wananchi kwa ujumla. Kwa mfano, kwenye Shirika la Bima la Taifa, Serikali imeagiza Bima wauze *none core assets* zao kwa ajili ya kutatua matatizo yaliyopo katika shirika hilo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee jibu zuri sana la Mheshimiwa Naibu Waziri kwa suala hili kwa swali la Mheshimiwa Kisyeri Chambiri kwamba, kimsingi Serikali inakubaliana na wasiwasi wa Mheshimiwa Kisyeri Chambiri na Mheshimiwa mwuliza swali kwamba, Mashirika ya Pensheni ya Kitaifa lazima yasimamiwe ili yaweze kutimiza majukumu yake ipasavyo na yaweze kuleta tija kwenye Sekta ya Fedha. Kwa hiyo, Serikali hivi sasa tunavyozungumza, inafanya mipango ya kuanzisha Chombo Maalum cha kusimamia na kudhibiti miendo ya vyombo hivi vya Fedha visiwe vya kibenki ili kusudi matakwa na Sera za Taifa ziweze kusimamiwa na kutekelezwa ipasavyo. Kwa hiyo, naomba anipe muda, muda si muda nitakuja hapa na mawazo kamili ili kwa baraka zenu niweze kufanya hiyo kazi mnayoitaka Serikali ifanye. *(Makofi)*

Na. 244

**Madini Mikoa ya Kusini**

**MHE. ALHAJI AHAMAD H. MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa ipo dhana kwamba katika Mikoa ya Kusini yapo madini mengi na ya aina mbalimbali:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya dhana hiyo?

(b) Kama kweli yapo madini, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaleta wawekezaji ili kuwekeza katika miradi ya madini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamad Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba, Mikoa ya Kusini ina madini mengi ya aina mbalimbali. Madini hayo ni pamoja na makaa ya mawe, *uranium,* chuma, *base metals*, chumvi, madini ya vito na kadhalika.

(b) Kwa kuzingatia sera, Serikali imekuwa ikitangaza mikoa ya Kusini sambamba na mikoa mingine katika kuvutia wawekezaji. Serikali imekuwa ikifanya hivyo kwa kupitia majarida, kushiriki katika mikutano ya uwekezaji na vyombo mbalimbali vya habari. Serikali haimchagulii mwekezaji maeneo ya kuombea leseni za madini, ni mwekezaji mweneywe, baada ya kupitia kumbukumbu za kijiolojia na takwimu za kijiofizikia zilizopo, yeye mwekezaji huteua maeneo ya kuombea leseni. Jambo kubwa linalozingatiwa mara nyingi na wawekezaji ni mahitaji ya madini husika katika soko la ndani na soko la nje ya nchi.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza. Je, kwa kuwa sasa kuna makundi ya vijana ambao wanajishughulisha na uchimbaji wa madini ambao ni wachimbaji wadogo wadogo, Serikali ina mpango gani wa kuwapa uwezo wa vifaa kwa kuwakopesha pamoja na uwezo wa kitaalam ili waweze kufanya vizuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali imeandaa maelezo mbalimbali kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo ambayo yanapatikana katika vitabu vitatu hivi mbalimbali, kuhusu utaratibu mzuri wa kuchimba, namna ya kuchimba na kuhakikisha kwamba kazi hii ya uchumbaji mdogo mdogo inafanyika kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu nyenzo za kufanyia kazi. Serikali imekuwa ikiwaunganisha vikundi ambavyo hasa ni vikundi vya ushirika na Taasisi ambazo zimekuwa zikihusika na kutoa misaada au kutoa mikopo yakiwemo mabenki kwa ajili ya uchimbaji mdogo mdogo. Lakini kwa kweli inabakia kazi ya wachimbaji wenyewe wadogo wadogo kuhakikisha kwamba, wanajiunga katika vikundi mbalimbali na kutokana na taarifa zilizopo basi huweza kufahamishwa wapi waende wakaombe misaada fulani fulani.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa miaka 12 iliyopita Tunduru ilikuwa maarufu sana kwa uchimbaji wa madini na *centre* ilikuwa Mtwara na tulikuwa tunachangamka Mtwara. Je, Serikali ina mpango

gani wa kuendeleza machimbo hayo ili uchangamfu ule wa fedha uwe unaendelea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wajibu wa kuchangamkia uchimbaji mdogo mdogo wa madini kama ulivyotokea kule Tunduru kwa hakika ni wa wachimbaji wenyewe na hufanywa hivyo kutokana na hali ya soko kama nilivyosema katika maelezo ya msingi, soko la madini fulani, soko la ndani na soko la nje.

Lakini wachimbaji wadogo wadogo pia wamekuwa na tabia ya kuhama kutoka eneo hadi eneo au kukimbilia eneo fulani pale panapoonekana kwamba, sasa hapa kuna madini ya aina fulani na kwamba kuna soko la madini hayo.

Na. 245

**Madhara ya kukatika kwa umeme mara kwa mara bila taarifa**

**MHE. ARIDI M. ULEDI (k.n.y. MHE. TALALA B. MBISE)** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme unapozimika mara nyingi bila taarifa, unasababisha uharibifu mkubwa wa vifaa vitumiavyo umeme vya watumiaji wa umeme huo majumbani kama vile *Fridge, TV, Cookers* na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini wasambazaji wa umeme kama *TANESCO* wasiwajibike kufidia hasara inayotokana na uharibifu wa vyombo vya wateja wake unaotokana na kuzimika kwa umeme bila taarifa?

(b) Je, ni lini Serikali itatunga sheria ya kumlinda mtumiaji wa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilivyojibu swali Na. 77 tarehe 18 Juni, 2004, kwenye kikao hiki cha Bunge, baada ya kutokea uharibifu wa vyombo/vifaa vya mteja kutokana na matatizo katika mfumo wa usambazaji umeme, mteja anatakiwa kutoa taarifa mara moja katika kituo cha *TANESCO* kilicho karibu yake. Wataalamu wa *TANESCO* watafika katika eneo husika na kuchukua taarifa mbalimbali za kusaidia kubaini sababu za uharibifu. Taarifa zinazochukuliwa ni pamoja na vyombo vilivyoharibiwa na umeme, vifaa vitumiavyo umeme katika nyumba husika na iwapo mteja amekinga vyombo vyake kwa kutumia vifaa maalum vya kukata umeme mara unapoanza kuwa na hitilafu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizo hufanyiwa uchunguzi wa kina na kitengo maalum cha kufuatilia madai cha *TANESCO,* yaani *claims section,* ili kubaini sababu za uharibifu

wa vyombo vya mteja, hususan kama uharibifu umetokana na matatizo katika mfumo wa usambazaji au ni hitilafu za umeme zilizotokea ndani ya nyumba ya mteja.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* haina utaratibu wa kulipa fidia kwa mali au vyombo vilivyoharibiwa, inapodhihirika kuwa hitilafu za mfumo wa usambazaji ndicho chanzo cha uharibifu wa vifaa. Hata hivyo, vifaa vya mteja vitakavyofidiwa ni vile tu zilizowekwa katika mkataba kati ya *TANESCO* na mteja.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Umeme ya mwaka 1957, inamlinda mteja pamoja na mtoa huduma ya umeme, inapotokea hitilafu na uharibifu wa vifaa au kuteketea kwa mali. Sheria hiyo inaeleza majukumu ya pande zote mbili yaani ya Mteja na *TANESCO*. Baada ya uharibifu wa mali ya mteja kutokana na umeme kutokea, uchunguzi hufanyika kama nilivyosema awali na ikibainika kwamba chanzo kikuu ni umeme wa *TANESCO,* basi Shirika hulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwafahamisha wananchi kwamba, vitu vilivyoharibika wakati wa ajali ya moto unaotokana na umeme vinaweza kuhitajika kwa ajili ya ukaguzi kama vielelezo. Hivyo, ni vyema watoe ushirikiano wakati wa zoezi zima la kuhakiki.

Aidha, wakati wananchi wanapounganishiwa umeme, vifaa vyote vinavyotumia umeme viorodheshwe au *TANESCO* iarifiwe vifaa vinapoongezeka ili *TANESCO* iweze kutoa ushauri kama kuna haja ya kurekebisha mfumo wa umeme wa ndani ya nyumba au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyosema tarehe 18 Juni, 2004 hapa Bungeni, ni muhimu sana katika usambazaji katika kuunganishiwa umeme wateja watumie mafundi wenye leseni za kusambaza umeme na wasitumie vishoka.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hitilafu inapokea wanaofanya tathmini ni wataalam wa *TANESCO*.

Je, hii haiwapi *loop hole TANESCO* kuficha ukweli ili kukwepa kulipa fidia? *(Makofi)*

Pili, je, *TANESCO* itakuwa tayari sasa kuwatumia wataalam huru badala ya wao wenyewe ili kufanya tathmini hiyo ili kuwe na haki kwa wote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kimsingi ni kweli kwamba, inawezekana kwa sababu wanaotathmini ni wao, panaweza kutokea udhaifu wa kibinadamu tu wa kutaka kuficha baadhi ya matatizo. Lakini napenda kwanza nieleze kwamba, inategemea na ukubwa wa tatizo. Kama nilivyojibu tarehe 18 Juni, 2004 hapa Bungeni, kwa mfano, kama nyumba imeungua na inahisiwa kwamba imeungua kutokana na matatizo ya umeme, siyo *TANESCO* peke yao wanaofanya tathmini hiyo. Kama nilivyoeleza tarehe 18 Juni, 2004, uchunguzi wa tukio kubwa kama hilo

hujumuisha *TANESCO,* Polisi na Askari wa Zimamoto. Kwa hiyo, pale hakuna uwezekano wa kufichaficha au kufanya unjanja wa aina hiyo.

Lakini pia kwa kuzingatia udhaifu huu kwamba, inawezekana wateja wanaweza wakakosa kutendewa haki na katika utawala mzuri tu wa usambazaji huduma hii muhimu ya umeme nchini, ndio maana Serikali imeunda chombo ambacho hapo baadaye kitaweza kuhakikisha kwamba, kinafuatilia kwa karibu na kinasimamia kwa karibu haki za mteja na haki za mtoa huduma, hiki chombo tunakiita *EWURA* na kama nilivyosema awali, kitakapoanza kufanya kazi, naamini kabisa kinaweza kusaidia kuondoa hata kama ni hisia kwamba pengine kuna uonevu wa aina fulani ambao unafanyika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yaliyopangwa kujibiwa leo yamejibiwa na muda wa maswali umekwisha. Sasa tunaendelea na mambo mengine, kwanza, ni matangazo ya vikao vya leo. Kwanza ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 14 Julai, 2004 saa tisa mchana kutakuwa na kikao cha Kamati chumba Na.231.

Kamati nyingine ni Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawatangazia Wajumbe wake kwamba, leo tarehe 14 Julai, 2004 kutakuwa na kikao kuanzia saa sita na nusu mchana chumba Na.219, ghorofa ya pili kwenye kumbi za Kamati.

Kamati nyingine ni ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, anawaarifu Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 14 Julai, 2004 saa saba mchana kutakuwa na kikao kwenye ukumbi Na.428, ghorofa ya nne.

Kikao cha mwisho kimeombwa na Katibu Mkuu wa *UPNAC*, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, anatoa taarifa kwamba, kutakuwa na kikao cha Wajumbe wa *UPNAC,* ambao ni Waheshimiwa Wabunge leo tarehe 14 Julai, 2004 kuanzia saa saba kwenye chumba Na.227, ghorofa ya pili kwenye kumbi za Kamati.

Mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, kwa kuichambua na kuijadili bajeti ya Wizara yangu kwa kina. Ushauri uliotolewa na Kamati hiyo pamoja na mawazo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakijadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na hotuba za Mawaziri wenzangu waliokwisha kuwasilisha bajeti zao, umesaidia sana katika kuboresha bajeti ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Profesa Anna Tibaijuka, kwa kuteuliwa kwao kuwa Makamishna katika Kamisheni ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair. Pia nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa katika Bunge la Afrika ambao ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, aliyechaguliwa kuwa Rais wa Bunge hilo, Mheshimiwa Dr. Amani W.A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani Zanzibar, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe na Mheshimiwa Dr. William Ferdinand Shija, Mbunge wa Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira na Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa *SADC*. Pia nawapongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwa tiketi ya CCM kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha Bunge kimekumbwa na pigo kubwa la kuondokewa na Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, ambaye amefariki dunia. Marehemu alikuwa ni mmoja wa waasisi na wasanifu wa Mradi wa Gesi ya Songo Songo, ambao Watanzania wataanza kunufaika nao hivi karibuni. Nachukua fursa hii kutoa rambirambi kwa Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu, jamaa na marafiki.

Aidha, napenda kutoa rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na wazazi au ndugu zao wa karibu akiwemo Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, ambao walifiwa na baba yao mzazi hivi karibuni. Pia nawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti zao. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *amina.*

Ninapenda vile vile kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamepata ajali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio makubwa ya Wizara katika mwaka 2003/2004 ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka kisiwa cha Songo Songo hadi Dar es Salaam na kusainiwa kwa mikataba mipya minne ya kuuza gesi hiyo kwa wateja wa viwandani; *(Makofi)*

(ii) Kuongezeka kwa wastani wa ukusanyaji maduhuli ya Wizara kutoka Sh.1.4 bilioni kwa mwezi hadi kufikia Sh. 1.9 bilioni kwa mwezi na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 36; na

(iii) Kuongezeka kwa idadi ya Makao Makuu ya Wilaya na vijiji vilivyopatiwa umeme nchini. Hata hivyo, kama nitakavyofafanua baadaye, kasi ya utekelezaji wa malengo ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2003/2004, hasa kwa upande wa nishati iliathiriwa na ukame ulioikumba nchi yetu. Ukame huo uliathiri upatikanaji wa maji kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa mwaka 2004/2005 imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuwezesha sekta binafsi kuongeza uwekezaji katika miradi ya sekta za nishati na madini ikiwemo Mradi wa Mchuchuma, Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay* na Mradi wa Gesi ya Songo Songo;

- Kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na kuweka misingi ya kufikisha umeme wa gridi katika Mikoa ya Ruvuma na Kigoma;

- Kuimarisha mfumo wa kuzalisha na kusambaza umeme katika maeneo ya mijini na vijijini;

- Kuimarisha uwezo wa kukusanya, kutunza na kuchambua takwimu kwa lengo la kuboresha usimamizi wa sekta za nishati na madini;

- Kuboresha ukusanyaji wa mapato;

- Kuongeza mazingira ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini ili kuongeza tija na uzalishaji;

- Kusimamia utunzaji wa mazingira, kuendeleza utafiti wa awali *(Basic Exploration)* katika sekta za nishati na madini, kuhamasisha usanifu wa *tanzanite* na madini mengine; na

- Kuongeza uwezo wa utendaji wa watumishi na vitengo vya Wizara ikiwemo *TANSORT.*

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya nishati kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 mwaka 2003 ukilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2002. Aidha, ukuaji wa sekta hii kwa mwaka 2003 ulifikia asilimia 5 ukilinganishwa na asilimia tatu mwaka

2002. Kama ilivyoelezwa awali, sekta hii iliathiriwa na ukame kutokana na mfumo wetu wa umeme kuwa bado unategemea nguvu ya maji kwa zaidi ya asilimia 60. Kukamilika kwa Mradi wa Gesi ya Songo Songo kutatuwezesha kubadilisha uwiano huo. Wizara ina mpango wa kufunga mitambo mingine ya kuzalisha umeme *(Gas Turbines)*. *Gas turbine* yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 36 itafungwa Oktoba, 2004 na kufuatiwa na nyingine yenye uwezo huo huo kabla ya Februari, 2005. Ufungaji wa mitambo hiyo utapunguza sana kiasi ambacho Taifa linategemea vyanzo vya maji kwa uzalishaji umeme ifikapo mwishoni mwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya umeme hapa nchini kwa mwaka 2003 yalifikia *kilowatt-hours* 2,387,635,995 ikilinganishwa na mwaka 2002 ambapo kiasi cha *kilowatt-hours* 2,264,861,710 kilitumika. Jinsi matumizi yalivyogawanywa miongoni mwa makundi tofauti ya watumiaji imeonyeshwa katika Jedwali Na. 1. Mahitaji ya juu katika mfumo wa gridi *(Peak Demand)* yaliongezeka kutoka Megawati 475 mwaka 2002 hadi megawati 506 mwaka 2003, likiwa ni ongezeko la asilimia saba. Kwa upande wa nishati ya petroli, mauzo na usambazaji wa bidhaa hizo kwa mwaka 2003 yalifikia mita za ujazo 1.24 milioni ikilinganishwa na mita za ujazo 1.0 milioni kwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, aya ya 5(iii) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, iliahidi kutekeleza mpango wa Serikali wa kuyapatia umeme Makao Makuu ya Wilaya ambazo zilikuwa hazijapata huduma ya umeme. Wakati Ilani ya Uchaguzi inatolewa mwaka 2000, Makao Makuu ya Wilaya 18 yalikuwa hayana umeme. Kuanzia mwaka huo hadi sasa Makao Makuu ya Wilaya 8 yamepatiwa umeme. Makao makuu ya Wilaya za Geita, Igunga, Mbarali, Meatu, Mkuranga, Ruangwa, Tandahimba na Sikonge, tayari yamepatiwa umeme. Ifikapo mwaka 2005 Wilaya za Biharamulo, Ngara, Rufiji, Serengeti, Ukerewe na Urambo zitakuwa zimekwishapatiwa umeme chini ya mpango unaoendelea. Ili kuboresha huduma ya umeme katika mji wa Mtwara, jenereta mpya yenye uwezo wa kuzalisha megawati 1.8 imekwishafungwa. Aidha, wakati Serikali ikitafuta namna ya kupeleka umeme wa uhakika Songea na Kigoma, jenereta mpya zitafungwa katika miji hiyo. Katika mwaka 2003/2004 vijiji 52 vilipatiwa huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi niliyoitaja ya kupeleka umeme kwenye Makao makuu ya Wilaya, hatua za awali pia zimeshaanza kuchukuliwa ili kufikisha umeme mikoa ya Kigoma na Ruvuma, pamoja na Wilaya za Bukombe, Kilindi na Simanjiro. Kuhusu Mkoa wa Ruvuma, tayari mkataba umetiwa saini wa kujenga kituo Makambako cha kupunguza nguvu ya umeme kutoka kilovoti *(kV)* 220 hadi kV 132 na *kV* 33. Mradi huo utafadhiliwa na Serikali ya Sweden. Aidha, Serikali hiyo imeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kufanya upenguzi yakinifu kwa mradi wa kupeleka umeme wa gridi Mkoani Kigoma. Hapo awali, ilitarajiwa kuwa mradi wa kupeleka umeme Urambo na Kaliua ungehusisha mpango wa kupeleka umeme Kigoma. Hata hivyo, ili kutochelewesha umeme wa Urambo na Kaliua imeonekana bora mradi mahususi wa umeme wa Kigoma uandaliwe.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2004, *Kahama Mining Corporation Limited (KMCL,)* iliingia Mkataba na *TANESCO* wa upanuzi wa kituo cha kupunguza nguvu ya

umeme na kujenga njia ya umeme kutoka eneo la machimbo hadi kwenye makazi ya wafanyakazi Ilogi na Bugarama na pia eneo la Kakola. Awamu ya pili inayofuata, ni kuufikisha umeme Ushirombo kutokea Ilogi. Hivi sasa Serikali inafanya mashauriano na wafadhili kwa ajili ya kupata fedha za kukamilisha awamu ya pili ya kuufikisha umeme Ushirombo pamoja na kuusambaza kwenye miji ya jirani na vitongoji vyake, kama vile Masumve na Unyovu. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. 3.5 bilioni. Ni matumaini ya Serikali kuwa fedha hizo zitapatikana haraka ili mradi utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchelewa kupata shilingi bilioni nne zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Umeme wa Simanjiro, sasa Serikali ya Sweden kupitia Sida imeonyesha nia ya kufadhili mradi huo. Aidha, kutokana na majadiliano yanayoendelea, Simanjiro inatarajiwa kupata umeme kati ya mwaka 2005 na 2006. Upenguzi yakinifu ulikamilika mwezi Machi, 2004 na mradi huo sasa umewasilishwa Sida kwa ajili ya kupatiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Wilaya ya Kilindi umeanza kutekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa njia ya umeme kutoka Handeni kwenda Kwediboma. Kazi hiyo iko katika hatua za mwisho kukamilika. Kilindi itapatiwa umeme kwa kujenga njia ya umeme kutokea Kwediboma baada ya umeme kufika huko.

Mheshimiwa Spika, ipo pia miradi mingine ya umeme inayoshughulikiwa mwaka huu, ikiwemo ya Sumve, Malya na Ntinko- Iyambi. Serikali imekuwa ikishughulikia suala la umeme Sumve, Malya kwa pamoja. Utekelezaji wa Mradi wa kupeleka umeme Sumve ulianza rasmi mwezi Juni, 2004 na hivi sasa kazi inaendelea. Aidha, kazi ya kupeleka umeme Malya itaanza baada ya maandalizi ya kupima njia ya umeme pamoja na ununuzi wa vifaa vya kujengea laini ya umeme kukamilika. Kazi hii inatarajiwa kuanza mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine mengi nchini ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyaombea yapatiwe umeme. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali inafanya kila jitihada ili kuyapatia maeneo hayo umeme. Moja ya hatua muhimu kabisa katika azma hii ni uanzishwaji wa Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kugharimia miradi ya umeme vijijini ni jukumu la Serikali. Ili kutekeleza jukumu hilo kwa uwazi na uhakika, Wizara inaandaa Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini *(Rural Electrification Master Plan - REMP)* itakayokuwa dira ya kutekeleza miradi hiyo. Mkataba kati ya Wizara, *TANESCO* na mshauri wa kuandaa *REMP* ulisainiwa na kazi kuanza mwezi Januari, 2004. Mpango huo utakamilika mwezi Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency - REA)* na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund - REF).* Mwezi Februari, 2004 Wizara iliandaa warsha juu ya *REA* na *REF* kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Katika warsha hiyo ilithibitika kuwa Waheshimiwa

Wabunge wanaunga mkono kuanzishwa kwa vyombo hivyo viwili. Mapendekezo na mkakati wa *REA* na *REF* baada ya kujumuisha maoni ya wadau yamewasilishwa kwenye ngazi husika Serikalini ili kupata ridhaa ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka miwili kuanzia Mei, 2002, *TANESCO* imekuwa chini ya uongozi wa kampuni ya *NET Group Solutions.* Kampuni hiyo ilipewa kazi kuu tano ambazo ni;-

- Kuboresha hali ya kifedha kwa kuongeza mapato na kupunguza gharama za uendeshaji;

- Kubadilisha mtazamo wa menejimenti ili uwe wa kibiashara; na kuimarisha njia za usafirishaji na usambazaji umeme ili kupunguza upotevu wa umeme. Katika kipindi hicho, *NET Group Solutions* imeweza kuongeza mapato ya *TANESCO* kwa asilimia 60 kutoka Sh. 10 bilioni kwa mwezi mwaka 2002 hadi Sh. 16 bilioni mwaka 2004;

- Kuwapa mafunzo mameneja 220 ili wabadili mtazamo wao kuwa wa kibiashara;

- Kupunguza upotevu wa umeme katika njia kuu za kusafirisha umeme kutoka asilimia 27 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 23 mwaka 2004;

- Kuongeza makusanyo kutoka kwa wateja kutoka asilimia 75 mwaka 2002 hadi asilimia 93 mwaka 2004; na

- Kufanya ukaguzi wa mita za umeme na kupunguza wizi wa umeme kwa takriban shilingi bilioni tatu kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *NET Group Solutions* una sehemu mbili za malipo ambazo ni *fixed retainer fee* au *management fee* na *success fee* au *bonus. Management fee* ni ada inayolipwa kulingana na matokeo ya zabuni ya Kimataifa ambayo *NET Group Solutions* ilishinda. Fedha zote za kulipa *management fee* zinatokana na msaada wa *SIDA*. Kwa miaka miwili ni *US$* 2,649,010 zimelipwa. Aidha, *success fee* imekuwa ikilipwa kutokana na *NET Group Solutions* kuvuka malengo yake ya utendaji kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kwenye Mkataba. Malipo hayo yametofautiana kutoka robo moja ya mwaka hadi nyingine. Kwa mwaka wa kwanza wa mkataba ulioisha mwezi Aprili, 2003, kiwango cha juu cha ada hiyo kilichofikiwa kilikuwa asilimia sita ya faida *(Net Cash Flow),* ambayo ilitokana kwa kiasi kikubwa na juhudi za *NET Group Solutions*. Kadri uboreshaji wa hali ya kifedha ya *TANESCO* ulivyoendelea ndivyo kiwango cha *success fee* kilivyopungua hadi kufikia asilimia nne ya faida kwa robo mwaka ulioshia Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, malipo ya ankara zote yaliyokusanywa na *TANESCO* katika kipindi cha miaka miwili ni Sh. 364 bilioni na faida *(Net Cash Flow)* ilikuwa Sh. 168 bilioni. Malipo ya *success fee* yamekuwa yakilipwa baada ya mshauri maalumu, *AF International* wa Sweden, kuhakiki utendaji wa *NET Group Solutions* na kuridhika kuwa vigezo vya mkataba vimefikiwa. Mshauri huyo amekuwa analipwa ada yake kutoka *SIDA*

na anawajibika kwa Bodi ya *TANESCO* na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC).* Kwa miaka miwili ya Mkataba kiasi cha *US$* 6,502,285 kitalipwa na *TANESCO* kama *success fee.*

Mheshimiwa Spika, Mkataba kati ya *NETGroup Solutions* na *TANESCO* uliisha muda wake wa miaka miwili mwezi Aprili, 2004. Ili kutoa nafasi ya kuandaa mkataba mpya, *NET Group Solutions* imeongezewa kipindi cha miezi mitatu hadi mwezi Julai, 2004. Aidha, Serikali ya Sweden imekubali kuendelea kulipa management fee ya *NET Group Solutions*iwapo Serikali itaamua kuingia Mkataba mpya.

Mheshimiwa Spika, wateja wamekuwa wakilalamikia *TANESCO* kwa kero mbalimbali zikiwemo kukatikakatika kwa umeme, matukio ya moto yanayotokana na umeme, bei kubwa za umeme, kuungua kwa vifaa kutokana na umeme kuwa na nguvu kupita kiasi na kuchelewa kufungiwa umeme baada ya kukamilisha taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, kukatikakatika kwa umeme ni kero kubwa na imekuwa ikiharibu sifa ya *TANESCO*. Kuna aina mbili za ukatikaji umeme, ule unaopangwa na *TANESCO* na ule usiopangwa. Katizo la umeme linalopangwa na kutangazwa katika vyombo vya habari huwa ni kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mfumo au mitambo ya umeme. Serikali inawaomba wananchi kuvumilia hali hiyo na kufuatilia kwa karibu matangazo ya *TANESCO* ili kupanga shughuli zao mbalimbali ipasavyo.

Hata hivyo, Serikali imeitaka *TANESCO* kutumia kwa kiasi kikubwa zaidi teknolojia ya kufanya matengenezo bila ya kuzima umeme. Katizo la umeme lenye kero zaidi ni lile lisilopangwa ambalo hutokana na mitambo, vifaa au mfumo kwa ujumla kuhitaji marekebisho ua hata kubadilishwa. Mfumo wa umeme nchini ni mkubwa wenye uwezo wa kuzalisha megawati 770 za umeme. Ili umeme uwafikie watumiaji, *TANESCO* ina njia za usafirishaji *(Transmission Lines)* zenye urefu wa jumla ya kilometa 4,532 na njia za usambazaji umeme kwa wateja *(Distribution Lines)* zenye urefu wa jumla ya kilometa 29,826. Kuufanyia marekebisho mfumo huo kunahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, matukio ya moto yanayotokana na umeme yameleta athari kubwa kwa wateja ikiwemo Serikali yenyewe. Aidha, kumekuwa na malalamiko kuwa *TANESCO* haishughulikii ipasavyo madai ya fidia yanayotokana na matukio hayo. Kuna vyanzo mbalimbali vya moto unaotokea na kuunguza vifaa na majengo. Vyanzo hivyo vinasababishwa na ama kutokuwa na uangalifu wa matumizi ya moto ndani ya nyumba, uchakavu na matumizi mabaya ya vyombo vitumiavyo umeme kama vile pasi, majiko ya umeme, majokofu na viyoyozi, ufungaji mbaya wa nyaya za umeme ndani ya nyumba au umeme mwingi kuzidi kiwango kinachostahili. Kutokana na hali hiyo ndiyo maana baada ya tukio la moto uchunguzi unatakiwa ufanywe ili kubainisha chanzo halisi cha moto na hatua za kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa makandarasi wa umeme hudhibitiwa kwa kutumia Sheria ya Umeme na Bodi ya Leseni za Umeme, pamoja na Bodi ya Usajili wa Makandarasi. Sheria ya Umeme *(Electricity Ordinance Cap. 131. Supp. 57 Sect. 84)* inaipa *TANESCO* uwezo wa kutunga kanuni ndogondogo za kuongoza matumizi ya

umeme. Sheria hizo ndizo zinawawajibisha *TANESCO* na mteja kwenye masuala yote yanayohusiana na usambazaji umeme. Kwa mfano, zinaainisha mambo ya kuzingatiwa kabla mteja hajawekewa umeme, mambo ya kuzingatia baada ya kuwekewa umeme, namna mteja atakavyolipia umeme na umbali ambao mtu anaruhusiwa kujenga nyumba kutoka kwenye njia kubwa za umeme. Kwa maana hiyo, kanuni hizo zinaweka mkataba kati ya *TANESCO* na mteja. Aidha, sheria ya umeme inaitaka *TANESCO* kuwapatia wateja umeme katika kiwango kinachotakiwa kwa maana ya voltage na frequency za umeme zinazokubalika. Inapotokea *TANESCO* au mteja kukiuka sheria, aliyeathirika anaweza kumchukulia mwenzake hatua ikiwemo kumshitaki. Napenda kutoa wito kwa wananchi wawe waangalifu katika matumizi ya vifaa vya umeme, waajiri mafundi wenye leseni za kufunga nyaya za umeme na wafuate taratibu zilizowekwa katika kufuatilia madai. *TANESCO* inaagizwa kushughulikia malalamiko kwa haki na kwa haraka bila ya usumbufu kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Januari, 2004, kati ya saa 11.00 na 12.00 jioni kulitokea moto katika eneo la matangi ya kuhifadhia mafuta ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme katika kituo cha umeme cha Ubungo, Dar es Salaam. Moto ulipotokea matangi hayo yalikuwa na mafuta yanayotumika kuzalishia umeme kituoni hapo. Hasara iliyopatikana kutokana na moto huo ni jumla ya Sh. 760 milioni ikiwa ni hasara ya Sh. 103 milioni kutokana na miundombinu ya umeme kuungua, Sh. 107 milioni kutokana na uharibifu wa *civil structures*, Sh. 369 milioni kutokana na uharibifu wa *mechanical structures* na Sh. 181 milioni, ambayo ni robo ya gharama yote iliyosababishwa na moto huo, kutokana na mafuta kuungua. Mara baada ya tukio hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza kuundwa kwa Kamati ya wataalamu ya kuchunguza tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa chanzo cha tukio hilo ulibainisha kuwa moto ulisababishwa na matatizo ya kiufundi ndani ya pampu moja ya kusukuma mafuta kutoka kwenye matangi yaliyoungua kuelekea kwenye matangi ya mitambo ya *gas turbines.* Ingawa moto ulianza kidogo kidogo, uliendelea na kuongezeka hadi kuzidi uwezo wa askari wa zimamoto. Wakati alipohutubia Bunge mwezi Februari, 2004, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa aliwapongeza wote waliohusika katika kuzima moto huo. Serikali imechukua hatua za tahadhari kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya uchunguzi.

Napenda kutoa wito kwa wananchi kuacha kufanya biashara au kujenga katika maeneo ya kuzalisha na kupitisha umeme au gesi ili kuepuka madhara kama haya yaliyotokea Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali kuhusu bei za umeme ni pamoja na kupunguza ruzuku kwa watumiaji wa umeme wa majumbani ambayo hugharimiwa na watumiaji wakubwa wa umeme, hususan wenye viwanda na wafanya biashara, ili wateja hao wakubwa weze kuhimili ushindani ndani na nje ya nchi. Marekebisho ya bei za umeme yaliyofanyika mwezi Aprili, 2002 na Juni, 2004 yalikuwa ni hatua ya utekelezaji wa sera hiyo. Kwa watumiaji wadogo, bado bei za umeme Tanzania ni nafuu kuliko Kenya na Uganda, kama ilivyoonyeshwa katika Majedwali Na. 2, 3 na 4, lakini umeme kwa watumiaji wakubwa ni ghali hapa Tanzania kuliko Kenya na Uganda. Kadri

tutakavyoongeza matumizi ya gesi, makaa ya mawe na vyanzo vingine vya nishati kwa kufuata *Power System Master Plan* ndivyo tutakavyofanikiwa kudhibiti upandaji wa gharama za umeme hapa nchini na hatimaye kuweza kuzipunguza.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2003, *TANESCO* ilikuwa inachukua wastani wa miezi mitatu kumfikishia mteja ankara ya umeme. Hivi sasa hauzidi mwezi mmoja na nusu kumfikishia mteja ankara ya matumizi ya umeme ya mwezi anaodaiwa, baada ya *TANESCO* kuboresha mfumo wa kutayarisha na kuwafikishia ankara wateja wake. Uboreshaji huo ni pamoja na kuanzishwa kwa utaratibu wa kuandaa ankara hizo katika ofisi za *TANESCO* na mikoa na baadhi ya Ofisi za Wilaya badala ya Makao makuu tu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuchelewa kuwafungia umeme wateja limekuwa likisababishwa zaidi na uhaba wa vifaa. Asilimia 90 ya vifaa vya kufungia wateja umeme vinanunuliwa kutoka nje ya nchi. Kwa uzoefu uliopo, kwa kufuata taratibu za Sheria ya Ununuzi ya 2001 vifaa huchukua miezi mitano hadi sita tangu kutangazwa katika zabuni hadi kufikishwa kwenye eneo la ujenzi. Ili kutekeleza miradi kwa haraka bila kukiuka taratibu, hatua zifuatazo zinachukuliwa na Shirika: Bodi ya Zabuni ya *TANESCO* hutoa zabuni kwa ajili ya vifaa vinavyotosheleza mahitaji ya mwaka mzima na ununuzi wa vifaa hufanywa kwa awamu kulingana na uwezo wa kifedha wa Shirika, unapotokea ukosefu wa vifaa, *TANESCO* haipokei malipo ya waombaji wapya wa huduma ya umeme. Kutokana na athari za ukame, mwaka 2003/2004, wateja 28,000 tu ndio walifungiwa umeme kati ya 36,000 waliopangwa kufungiwa. Aidha, Shirika lilikuwa na mpango maalumu wa kuwaunganishia umeme wateja 100,000 lakini mradi huo ulisitishwa kutokana na athari hizo kwa hali yake ya kifedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bomba la gesi ya Songo Songo ambao ulianza mwezi Agosti, 2003 umekamilika. Matumizi ya gesi ya Songo Songo kwa ajili ya kuzalisha umeme katika mitambo ya umeme ya Ubungo na baadaye katika mitambo ya *IPTL* ni hatua muhimu ya kuacha kutegemea sana nguvu za maji kwa ajili ya kuzalisha umeme. Gesi hiyo itatumiwa pia na *Tanzania Portland Cement Company Limited* kwenye kiwanda cha simeti cha *Wazo Hill* na viwanda vingine kama vile vya *Kioo Limited* na *Tanzania Breweries Limited,* ambavyo tayari vimeingia mikataba ya kununua gesi na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* na mshiriki wake *Pan African Energy Limited.* Viwanda hivyo vinalenga kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutumia gesi badala ya mafuta. Kama nilivyoeleza awali, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2005 uwezo wa kuzalisha umeme wa mitambo ya thermal utaongezeka kutoka takriban asilimia 30 ya uwezo wa mitambo yote katika mfumo wa gridi hivi sasa hadi kufikia asilimia 45. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa Gesi ya Songo Songo, imeandaa mpango wa kuipatia umeme miji ya Kilwa Masoko, Ikwiriri, Kibiti, Utete, Bungu na vijiji zaidi ya 30 vilivyo karibu na bomba la gesi ya Songo Songo. Umeme kwa ajili ya miji hiyo utazalishwa na mitambo ya *MW 4.5* itakayotumia gesi ya Songo Songo. Mitambo hiyo itajengwa Somanga Funga. Njia ya *kV* 33 itajengwa kutoka Somanga hadi Songino, Kilwa Masoko na njia nyingine pia itajengwa kutoka Somanga hadi Utete, Ikwiriri, Kibiti na Bungu kupitia Nyamwage. Vijiji vingine vidogo vitapatiwa umeme wa

solar. Fedha kiasi cha *US$* 8 milioni za utekelezaji wa mpango huu zimeshatolewa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya kujenga bomba la gesi ya Songo Songo, ambayo mshindi wake alikuwa ni kampuni ya *Larsen and Toubro* ya India, ilikuwa ya gharama nafuu kuliko fedha zilizotengwa kwa kiasi cha *US$* 70 milioni. Serikali imekubaliwa na Benki ya Dunia kutumia salio hilo kwa ajili ya kukarabati na kupanua mfumo wa gridi ambao umechakaa katika sehemu nyingi nchini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza hapa Bungeni wakati wa kujibu maswali, ni kweli kuwa Benki ya Dunia iliwahi kutenga fedha kwa ajili ya Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay.* Mwaka 1992, wakati wa kuandaa mradi wa umeme wa *Sixth Power Project*, Benki ya Dunia ilitenga *US$* 15 milioni katika bajeti ya mradi huo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *Mnazi Bay,* lakini kwa masharti kwamba, kama gharama za utekelezaji wa mradi huo zitazidi *US$* 15 milioni, itabidi fedha zote zinazohitajika zipatikane kwanza kabla ya kutumia fedha hizo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, taarifa za upenguzi yakinifu zilizotolewa mwaka 1994 zilibaini kuwa Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay* ungegharimu *US$* 32 milioni. Serikali ilijitahidi kuwapata wawekezaji wa kuchangia gharama hiyo na kutekeleza mradi bila ya mafanikio. Wawekezaji walioonyesha nia ya kushiriki kwa nyakati tofauti walikuwa ni pamoja na kampuni za *Santa Fe, Tullow Oil, Tornado Resources* na *Deepak Fertilizers.* Kutokana na kutokutimiza masharti ya Benki ya Dunia, baada ya ukame kuikumba nchi yetu mwaka 1994/95 na kusababisha mgao wa umeme, ilibidi fedha hizo zitumike kutekeleza mradi wa dharura wa ununuzi wa mitambo ya umeme *(Gas Turbines)* iliyosimikwa kwenye kituo cha umeme cha Ubungo. Kupata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay* kutahitaji majadiliano na makubaliano mapya. Kutokana na taratibu na masharti ya Benki ya Dunia, mpango mzima utachukua muda mrefu, ndiyo maana Serikali imeingia makubaliano na Kampuni ya *Artumas Group* ili kuendeleza Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2004, Serikali ilitiliana saini Mkataba *(Production Sharing Agreement)* na kampuni ya *Artumas* kwa lengo la kuzalisha umeme kwa ajili ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na baadaye Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma. *Artumas* inatarajia kupata mkopo kutoka kwa asasi za fedha za *FMO* ya Uholanzi na *IDC* ya Afrika Kusini. Mradi wa *Mnazi Bay* unatarajiwa kutekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itakayochukua miezi sita kuanzia Julai, 2004, itahusu kufanya tathmini ya kuhakiki kiwango cha gesi iliyopo ili kuwezesha maandalizi ya mradi kukamilika na awamu ya pili itahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha megawati 15 za umeme, bomba la kusafirisha gesi hadi kwenye kituo hicho, ukarabati wa njia za umeme za Mtwara na Lindi na ujenzi wa njia ya umeme ya kilometa 24 kati ya Mingoyo na njia ya umeme inayotokea Ndanda. Serikali ina matumaini makubwa kuwa Mradi wa Gesi ya *Mnazi Bay* utafanikiwa.

Hata hivyo, endapo matokeo ya uhakiki wa gesi iliyopo Mnazi Bay hayataridhisha, Serikali inakusudia kutumia njia nyingine ya kuwa na umeme wa uhakika

katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Njia hiyo ni kujenga kituo kikubwa cha kuzalisha umeme Somanga Funga kwa kutumia gesi ya Songo Songo na njia ya umeme ya *kV* 132 ya kusafirisha umeme huo kutoka Somanga hadi maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2004 Wizara iliwasilisha mapendekezo Serikalini ya namna ya kuukwamua Mradi wa Umeme wa Mchuchuma. Mapendekezo hayo, ambayo yalitolewa baada ya kutafakari uchambuzi wa uendelevu wa Mradi huo uliofanywa na mshauri mtaalamu, yalikuwa ni pamoja na kuuendeleza mradi kwa awamu badala ya kuujenga ukiwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 400 tangu mwanzo, wawekezaji kukamilisha utafiti wao katika maeneo kadhaa ili kuwa na uhakika zaidi juu ya gharama za mradi na mitambo na wakandarasi wa ujenzi wa mradi kupatikana kwa njia ya ushindani. Hata hivyo, hivi karibuni wawekezaji wa Mradi wa Mchuchuma wameieleza Wizara kuwa wao wangependa kujenga kituo ha umeme chenye uwezo wa Megawati 400, wako tayari kujitafutia masoko ya umeme na hawataitaka *TANESCO* kununua au kulipia umeme zaidi ya mahitaji yake. Wizara imewataka wawekezaji hao kuthibitisha maelezo hayo ili maandalizi ya mradi huu yaendelee. Kuna matumaini kuwa kama Mradi wa Mchuchuma utatekelezwa kwa misingi hiyo, utekelezaji wake utafungua ukurasa mpya wa maendeleo ya ukanda wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992 Serikali ilitangaza Sera ya Nishati ambayo iliruhusu sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza sekta ya umeme. Mwaka 1994/95, Serikali iliingia makubaliano ya kuendeleza Mradi wa Umeme wa *IPTL* baada ya nchi kukumbwa na ukame uliosababisha upungufu mkubwa wa upatikanaji wa umeme nchini na kuathiri uchumi wa nchi yetu. Wakati huo, kama ilivyo sasa, uwezo wa kuzalisha umeme nchini ilikuwa unategemea sana mitambo inayotumia nguvu ya maji.

Mheshimiwa Spika, wakati kazi ya ujenzi wa Mradi wa *IPTL* ikiwa karibu kukamilika, *TANESCO* iliingia katika mgogoro na *IPTL* kuhusu gharama na bei ya umeme ya mradi huo. Serikali iliiruhusu *TANESCO* kufikisha mgogoro huo katika Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro ya Uwekezaji *(ICSID).* Maamuzi ya *ICSID* yaliipa unafuu *TANESCO*, kwani bei ya huduma ya *IPTL (capacity charge)* ilipunguzwa kwa kiwango kikubwa kutoka *US$* 4.5 milioni hadi *US$* 2.6 milioni kwa mwezi (kabla ya kodi ya *VAT)* na madai ya *IPTL* ya fidia ya zaidi ya *US$* 53 milioni kwa gharama zilizolimbikizwa kuanzia Septemba, 1998 hadi Januari, 2002, wakati mradi ulipoanza kuzalisha umeme, yalikataliwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *IPTL* hivi sasa unatarajiwa kufanyiwa marekebisho ili uweze kutumia gesi ya Songo Songo. Marekebisho hayo yanatarajiwa kugharimu jumla ya *US$* 11.6 milioni ambazo ziliamuliwa na *ICSID.* Faida itakayopatikana kutokana na marekebisho hayo ni kushuka kwa bei ya ununuzi wa kila uniti ya umeme utakaozalishwa na *IPTL (energy charge)* na hivyo kupunguza mzigo kwa *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba mradi wa *IPTL* umelisaidia Taifa kuepukana na janga la mgao wa umeme wakati wa ukame hivi karibuni, ni lazima tukiri kuwa umeme wa *IPTL* ni ghali, hasa wakati huu ambapo bei za mafuta yanayotumiwa na *IPTL* kuzalisha umeme ziko juu sana katika soko la dunia.

Katika hatua nyingine yenye lengo la kupunguza gharama ya umeme wa *IPTL,* Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Malaysia, wawekezaji wa mradi huo (Kampuni za *Mechmar* ya Malaysia na *VIP Engineering and Marketing Limited* ya Tanzania), asasi za fedha zinazotaka kununua deni la *IPTL* kutoka Serikali ya Malaysia na Benki ya Dunia. Suala la Serikali kununua *IPTL* kwa mkopo au msaada bado linafanyiwa kazi kwa kuwashirikisha wadau hawa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, bei za mafuta katika soko la dunia zilipanda na ni muhimu wananchi wakaelewa hali halisi ilivyo katika biashara ya mafuta na sababu za kupanda kwa bei ya mafuta nchini. Hadi sasa Tanzania haizalishi mafuta ya petroli na mafuta yote yanayotumika nchini huagizwa kutoka nchi za nje, hususan nchi zilizopo katika ghuba ya Arabia na Afrika Kusini. Serikali ilianzisha soko huria la mafuta ya petroli nchini na kujiondoa katika biashara ya mafuta mwaka 2000. Kabla ya hapo, mafuta ghafi na yaliyosafishwa yalikuwa yakiagizwa na *TPDC* na kusambazwa na makampuni binafsi ya mafuta katika soko la ndani. Baada ya mfumo wa soko huria kuanza, uagizaji na usambazaji wa mafuta ya petroli umekuwa ukifanywa na makampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *TPDC* na kwa mujibu wa sheria ya kubana matumizi ya mafuta *(Petroleum (Conservation) Act, 1981),* imekuwa ikifuatilia hali ya upatikanaji wa mafuta ya petroli hapa nchini. Kwa sasa wastani wa mahitaji ya mafuta kwa Taifa kwa aina mbalimbali za mafuta ni tani 3,400 kwa siku. Kwa kupitia makampuni yanayoagiza mafuta, Wizara huhakikisha kuwa nchi inakuwa na akiba ya kutosheleza matumizi ya nchi ya mwezi mmoja kwa wastani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na soko la mafuta nchini kuwa huria, bei za mafuta hutegemea gharama za mafuta, pamoja na ushindani miongoni mwa makampuni ya mafuta. Kwa ujumla, gharama zinazohusika hujumuisha gharama za ununuzi, usafirishaji na bima, gharama za uendeshaji wa makampuni husika, faida kwa makampuni, kodi za Serikali na gharama na faida kwa wenye vituo vya mafuta. Gharama hizo hupangwa kwa kuzingatia kushuka kwa thamani ya sarafu yetu.

Mheshimiwa Spika, msingi wa upangaji wa bei za mafuta nchini unategemea hali ya soko la mafuta duniani. Aidha, bei katika soko la dunia hutegemea kiwango cha uzalishaji wa mafuta ghafi, gharama za kuyasafisha, pamoja na hali ya usalama duniani ambayo huathiri soko na gharama za bima. Ongezeko la bei za mafuta ghafi hivi karibuni kutoka *US$* 32 hadi *US$* 41 kwa pipa limesababisha kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania.

Sababu kubwa zilizoelezewa kuchangia upandaji huo ni pamoja na hali mbaya ya usalama nchini Iraq na Mashariki ya Kati kwa ujumla, kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta duniani, nchi zenye matumizi makubwa ya mafuta kuongeza viwango vya akiba yao ya mafuta; nchi wanachama wa *OPEC* kupunguza uzalishaji wa mafuta na kupanda kwa gharama za kusafirisha mafuta.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na zitakazochukuliwa na Serikali ili kupunguza athari za bei kubwa ya mafuta nchini ni pamoja na kuzuia vitendo vinavyopunguza ushindani katika soko, kuanzisha chombo kitakachosimamia sekta ya nishati *(Energy and Water Regulatory Authority - EWURA),* kuandaa sheria mpya ya biashara ya mafuta *(Petroleum Supply Act)* na kuwashawishi na kuwawezesha wafanyabiashara wasio na maghala ya kuhifadhia mafuta watumie maghala yaliyopo *TIPER,* Malawi *Cargo Centre* na sehemu nyingine ili kupunguza gharama zao za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa soko huria la mafuta mwaka 2000 hadi sasa, hakujajitokeza upungufu wa mafuta nchini kama ilivyokuwa ikitokea mara kwa mara kabla ya kuchukuliwa kwa hatua hiyo. Serikali kuacha kupanga bei za mafuta kumewezesha wafanyabiashara kufikisha mafuta sehemu yanakohitajika kwa bei ya soko. Pamoja na mafanikio hayo, bado soko limeendelea kukumbwa na udanganyifu wa baadhi ya wafanyabiashara na ongezeko la bei lisilowiana na hali halisi ya soko. Kufuatia hali hiyo, mwezi Mei, 2004 Wizara iliandaa mkutano na viongozi wa makampuni makubwa ya uagizaji na uuzaji mafuta ya petroli. Lengo la mkutano lilikuwa ni kuwaonya na kuwakumbusha kuwa ni kinyume cha sheria kupanga bei kwa kushirikiana badala ya kushindana. Kukamilika kwa zoezi la Serikali la kuanzisha mamlaka kama vile *EWURA* kunatarajiwa kuongeza uwezo wa kusimamia na hivyo kudhibiti makampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Ndovu Resources* ya Australia ilichoronga kisima cha utafutaji wa mafuta katika eneo la Kisiwa cha Nyuni. Kisima hicho kilichorongwa kuanzia mwezi Septemba, 2003 hadi Machi, 2004 na kufikia kina cha meta 3,905. Kampuni hiyo imetumia zaidi ya *US$* 13 milioni kwa kazi hiyo. Ingawa hayakugunduliwa mafuta wala gesi kwenye kisima hicho, takwimu zilizopatikana zitasaidia katika uchunguzi zaidi utakaofanywa katika eneo la visiwa vya Nyuni na Okuza kabla ya kuamua ni wapi kisima kingine kichorongwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, tumeweza kukamilisha majadiliano na makampuni matatu ya utafutaji wa mafuta na kusaini mikataba *(Production Sharing Agreements)* nayo. Makampuni hayo ni *Artumas* ya Canada (kwa eneo la *Mnazi Bay*), *Maurel and Prom* ya Ufaransa (kwa maeneo ya Mafia, Bigwa na Rufiji) na *Petrobras* ya Brazil (kwa eneo la baharini mashariki ya Kisiwa cha Mafia).

Mheshimiwa Spika, kuanzia miaka ya 1990 teknolojia ya utafutaji mafuta, hususan katika maeneo ya vilindi vya bahari *(Deep Sea),* imeendelezwa sana na kuyawezesha makampuni ya mafuta kuanza kuwekeza katika maeneo hayo. Nchi ambazo zimefanikiwa kugundua mafuta katika vilindi vya bahari barani Afrika ni pamoja na Mauritania, Guinea Bissau, Angola na Nigeria na kwa upande wa *Latin America* ni pamoja na Mexico na Brazil. Kwa upande wetu, Serikali imekamilisha majadiliano na kampuni ya Shell ya Uholanzi ili kampuni hiyo itafute mafuta katika maeneo ya vilindi vya bahari ya Hindi, mashariki ya Zanzibar na taratibu za kuingia mkataba na kampuni hiyo zinaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuyashawishi makampuni kutafuta mafuta katika maeneo ya vilindi vya Bahari ya Hindi, Wizara imekuwa pia ikiendelea na juhudi za kuyashawishi kutafuta mafuta katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi na maeneo ya Bonde la Ufa.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kuwa pengine watafutaji wa mafuta wanapewa muda mrefu mno kushikilia maeneo yao. Kutokana na gharama kubwa za uwekezaji ni muhimu watafutaji wapewe muda wa kutosha kukamilisha kazi zao, vinginevyo haitakuwa rahisi kupata wawekezaji katika eneo hili lenye ugumu wa kuvutia mitaji, ambapo gharama ya kuchoronga kisima kimoja cha utafutaji mafuta inaweza kuwa kati ya *US$* 10 milioni na *US$* 15 milioni na kuna uwezekano mkubwa wa kutogundua mafuta wala gesi.

Mheshimiwa Spika, hatima ya kampuni ya *TIPER* ambayo inamilikiwa nusu kwa nusu na Serikali na *Oryx Limited* inajadiliwa katika ngazi za juu Serikalini. Kampuni hiyo ilisitisha kazi ya kusafisha mafuta mwaka 1999 na matangi ya kampuni hiyo hutumika kuhifadhi ya mafuta ya makampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* imeendelea kutafuta wawekezaji katika maeneo yaliyo wazi na yale ambayo yana jiolojia inayofaa kwa ugunduzi wa mafuta na gesi. Katika kipindi cha 2003/2004, mada za kitaalamu zilitolewa kwenye mikutano ya wawekezaji huko Barcelona, Calgary, Cape Town, Dallas, London na Paris. Makampuni kadhaa yamenunua takwimu za utafutaji za maeneo mbalimbali ili yazifanyie kazi. Kutokana na kujitokeza kwa makampuni hayo, Serikali na *TPDC* zinajiandaa kuitisha zabuni nyingine ya utafutaji wa mafuta *(Third Tanzania Licensing Round)* mwaka 2004/2005. Mafanikio ya zabuni hiyo yatategemea sana kupatikana kwa ufumbuzi wa hoja zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu mgawanyo wa madaraka na faida za utafutaji na uzalishaji wa mafuta kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kufikiwa kwa maelewano juu ya hoja hizo kutatuwezesha kurekebisha sheria ya utafutaji wa mafuta *(Petroleum (Exploration and Production) Act, 1980)* ili ihusishe taratibu na masharti yanayofaa zaidi kwa utafutaji wa mafuta kwenye vilindi vya bahari.

Mheshimiwa Spika, azma ya kujenga bomba la kusafirisha mafuta toka Dar es Salaam hadi Mwanza ni ya miaka mingi, lakini haijatekelezeka. Kampuni ya hapa nchini, *Africommerce International Limited,* ilipewa fursa ya kuendeleza mradi huo lakini baada ya miaka mingi haikuweza kuendeleza mradi huo. Mwezi Juni, 2004 Wizara ilisaini makubaliano ya awali na kampuni nyingine, *Richmond Development Company* kutoka Marekani, ambapo kampuni hiyo imepewa miezi 18 ili iwekeze katika kufanya upenguzi yakinifu wa kina kwa lengo la kuiwezesha Serikali kufanya maamuzi juu ya hatua za kuchukua ili mradi huo uweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishati mbadala, sehemu kubwa ya nishati itumikayo nchini hutokana na kuni na mkaa, hasa kwa kupikia, hali ambayo huwaathiri wananchi kiafya kutokana na moshi, pamoja na uharibifu wa mazingira. Pamoja na kwamba upatikanaji wa umeme hasa vijijini unasisitizwa, utafiti umeonyesha kwamba ni watu wachache sana

wanaotumia umeme kwa kupikia. Kwa mfano, hata kwa mji kama Dar es Salaam bado zaidi ya nusu ya kaya zenye umeme zinatumia mkaa au kuni kupikia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kutafuta nishati ya kutumia badala ya kuni na mkaa, imejitahidi pia kuhamasisha matumizi bora ya kuni na mkaa kupitia majiko bora, na kueneza majiko ya pumba ili yaweze kutumika katika maeneo ambayo kuni au mkaa havipatikani kwa urahisi. Mwaka huu wa 2004, Wizara imesaini mkataba na shirika lisilo la Kiserikali la *TATEDO* kwa lengo la kuhamasisha na kuendeleza utengenezaji wa majiko sanifu ya mkaa, pumba na mabaki ya mazao katika mikoa ya Dodoma na Tanga. Kwa upande mwingine, Tanzania ni mojawapo ya nchi tatu ambazo zimefanikiwa kuingia katika programu ya *SADC* ya kuboresha matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa ufadhili wa Serikali ya Uholanzi. Vilevile jitihada bado zinaendelea za kuhamasisha matumizi ya vijitofali vya makaa ya mawe kwa kupikia, hasa kwenye taasisi, ambazo matumizi yake ya kuni na mkaa ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kuwa kiwango cha umemenuru *(Solar Electricity)* kinachozalishwa na mitambo midogomidogo nchini ni jumla ya Megawati moja. Umeme huo unatumika kwenye taasisi, mashuleni, majumbani na katika mawasiliano. Mashirika ya *UNDP/GEF* yanafadhili mradi wa umemenuru huko Mwanza ambao ulianza mwezi Machi, 2004. Mradi mwingine kama huo unaofadhiliwa na Sida utaanza kabla ya Oktoba, 2004 na utahusisha maeneo mengi zaidi nchini kulingana na soko la umemenuru litakavyopanuka. Miradi yote hii ina lengo la kuondoa vikwazo vinavyozuia soko la teknolojia hiyo kuendelea na kuhamasisha sekta binafsi na wananchi kwa ujumla kuitumia. Matarajio ya Wizara ni kwamba wananchi wengi wataweza kutumia umemenuru na hivyo kuongeza idadi ya Watanzania ambao wanapata umeme, hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, nguvu ya upepo inatumika hapa nchini zaidi kwa kusukuma maji, hususan katika sehemu za Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa. Kasi ya upepo katika maeneo hayo haitoshi kuweza kuzalisha umeme wa uhakika. Hata hivyo, ili kuendeleza matumizi ya umeme utokanao na nguvu ya upepo, Serikali inafanya mazungumzo na Serikali ya Denmark kupitia Shirika lake la *DANIDA* ili kupata fedha za kuendeleza upimaji wa kasi ya upepo katika maeneo ya Mkumbara na Karatu. Lengo ni kupata takwimu za kusanifu na kujenga wind farm zenye uwezo wa kuzalisha kati ya Megawati 30 na 50 za umeme.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2002 hadi asilimia tatu mwaka 2003. Aidha, sekta hiyo ilikua kwa asilimia 17 mwaka 2003 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15 kwa mwaka 2002. Uwekezaji, ukusanyaji maduhuli, utoaji ajira kwa Watanzania na mchango kwa mapato ya fedha za kigeni vinaendelea kuongezeka katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Serikali yanayotokana na mrabaha na kodi kwenye migodi mikubwa nchini yamekuwa yakiongezeka kila mwaka tangu 1999. Migodi mikubwa pia imekuwa ikisaidia katika utekelezaji wa miradi ya jamii kama vile ya afya, elimu, maji, barabara na kadhalika, imekuwa ikigharimia mafunzo kwa

wafanyakazi wao na inazidi kuongeza ununuzi wa vifaa na huduma kutoka ndani ya nchi, kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 7. Kwa ujumla, vivutio vinavyotolewa na Tanzania kwa wawekezaji kwenye sekta ya madini viko karibu sawa na nchi nyingine zinazovutia wawekezaji wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utafutaji na uchimbaji wa madini ni sehemu muhimu ya mkakati wa Serikali katika sekta ya madini na unalenga kuhakikisha kuwa madini yanachangia ipasavyo kukuza Pato la Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea na shughuli za usimamizi wa sekta ya madini ambazo zinajuhusisha utoaji wa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini, ukaguzi wa migodi na utoaji wa huduma za ushauri kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kurahisisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini nchini, Wizara kwa kushirikiana na *Nordic Development Fund (NDF),* itaanza kutekeleza mradi mpya ujulikanao kama *Mining Cadastre Information Management System*. Mfumo unaokusudiwa kuwekwa chini ya mradi huo utatumia teknolojia ya kisasa ya kompyuta na mawasiliano katika uwekezaji, uchambuzi na matumizi ya ya taarifa zote kuhusu leseni na shughuli zinazoendelea chini ya leseni hizo kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika utafutaji wa madini nchini umeendelea kuongezeka. Maombi mengi ya leseni za madini ni kwa ajili ya utafutaji wa dhahabu ingawa kumejitokeza pia mwelekeo kwenye *base metals* na *platinum.* Hali hii inatokana na ongezeko la mahitaji ya madini na bei nzuri ya madini hayo duniani, hasa Uchina. Maeneo maarufu kwa utafutaji wa dhahabu ni sehemu za Ziwa Victoria, Chunya na Mpanda. Makampuni yanaendelea na utafutaji wa madini ya *base metals* hususan katika maeneo ya kusini na kusini magharibi mwa nchi yetu. Utafutaji wa madini ya *platinum* unaendelea katika mikoa ya Rukwa, Kigoma na Mbeya na Wilaya za Nachingwea na Masasi. Utafutaji wa madini ya vito unaendelea katika Wilaya za Morogoro, Mbinga, Handeni, Arusha, Sumbawanga, Tanga, Mpwapwa na Ruangwa. Utafutaji wa madini ya viwandani ambao unafanywa zaidi na wawekezaji wa ndani unahusisha chokaa, chumvi na jasi. Utafutaji wa jasi unafanyika katika Wilaya za Mpwapwa, Same, Manyoni na Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukusanya, kuandaa na kuhakiki taarifa na takwimu za kijiolojia, kijiokemia na kijiofizikia ambazo hutumiwa na wawekezaji katika kuomba leseni za utafutaji. Katika mwaka 2003/2004, maeneo yaliyohusika ni Kigoma, Mpanda na Urambo. Kazi hiyo inatekelezwa na *Tanzania Geological Survey (TGS),* kitengo cha Wizara ambacho kiko katika hatua za mwisho za kugeuzwa rasmi kuwa Wakala wa Serikali. Katika mwaka 2003/2004, Wizara kupitia *TGS* ilisimamia pia ukusanyaji wa takwimu za kijiofizikia kwa njia ya anga *(Airborne Geophysical Survey)* uliofanyika katika maeneo yenye jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 32,000. Maeneo husika yako katika Wilaya za Kahama, Bukombe, Biharamulo, Mpanda, Urambo, Sikonge, Musoma, Bunda, Tarime na Serengeti. Takwimu za uchunguzi huo zinapatikana *TGS* Dodoma. Kazi inayoendelea sasa ni ukusanyaji wa takwimu zaidi kwa kuyatembelea maeneo husika. Mradi huu unafadhiliwa na *NDF.*

Mheshimiwa Spika, kati ya migodi mitano mikubwa inavyozalisha dhahabu hapa nchini ambayo ni Geita, Kahama, Mara, Musoma na Tarime, mgodi wa Geita umepanuliwa na hivi sasa unazalisha wakia 650,000 (sawa na tani 22) za dhahabu kwa mwaka, ikilinganishwa na wakia 500,000 (sawa na tani 16) za dhahabu kwa mwaka kabla ya upanuzi. Upanuzi pia unaendelea katika mgodi wa Tarime wa *Afrika Mashariki Gold Mines.* Upanuzi wa mgodi huo utakapokamilika mgodi utakuwa na uwezo wa kuzalisha wakia 300,000 (sawa na tani tisa) za dhahabu kwa mwaka ikilinganishwa na uzalishaji wa sasa wa wakia 200,000 (sawa na tani sita) za dhahabu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 mgodi wa *Williamson Diamonds Limited (WDL)* uliopo Mwadui ulizalisha karati 207,400 za almasi ikilinganishwa na karati 177,250 mwaka 2002. Mgodi mpya wa almasi unaomilikiwa na *El Hillal Minerals Limited* umeanzishwa jirani na mgodi wa *WDL*. Mgodi huo, ambao una lengo la kuzalisha kati ya karati 18,000 na 24,000 za almasi kwa mwaka, ulianza uzalishaji wa majaribio mwezi Januari, 2004. Mgodi wa *Merelani Mining Limited* uliendelea kuzalisha na kusanifu tanzanite huko Merelani, Manyara.

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba, 2003, Serikali ilisaini mkataba na kampuni ya *Pangea Minerals Limited* kuanzisha mgodi wa dhahabu wa Tulawaka uliopo Wilayani Biharamulo. Ujenzi wa mgodi umekwishaanza na unatarajia kugharimu *US$* 50 milioni. Utafiti uliofanyika hadi sasa umeonyesha kuwa mgodi huo una mashapo ya wakia 525,680 (sawa na tani 16) za dhahabu. Mgodi utakuwa unazalisha wastani wa wakia 100,000 (sawa na tani tatu) kwa mwaka zenye thamani kati ya *US$* 38 milioni na *US$* 40 milioni kwa bei ya sasa ya dhahabu katika soko la dunia. Utafiti zaidi unafanyika ili kuongeza mashapo na hivyo kuongeza muda wa uhai wa mgodi. Mgodi unatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Januari, 2005 ambapo utatoa ajira kwa jumla ya watu 300, kati ya hao 250 wakiwa ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, migodi mingi imekuwa ikishirikiana na asasi mbalimbali pamoja na *NGOs* katika kudhibiti UKIMWI migodini na kuchangia katika vita dhidi ya UKIMWI nchini. Mgodi wa *Geita Gold Mining Limited* umekuwa na utaratibu wa kuandaa matembezi ya kupanda Mlima Kilimanjaro ili kuchangisha fedha za kupiga vita UKIMWI. Mwaka huu, mgodi huo umechangisha zaidi ya Sh. 150 milioni. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri Mkuu na wengine wote walioshirikiana na mgodi huo katika juhudi zake za kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Mradi wa *Kabanga Nickel* Wilayani Ngara uliendelezwa kwa uchorongaji zaidi ili kuthibitisha wingi wa madini. Matokeo hadi sasa yanaonyesha kuwepo kwa mashapo yanayofikia tani 26 milioni yenye kiasi cha nickel cha wastani wa asilimia tatu. Matokeo hayo pamoja na mwelekeo mzuri wa bei ya *nickel* katika soko la dunia yameweza kuivutia kampuni ya *Falconbridge Limited* ya Canada ambayo ni miongoni mwa makampuni makubwa duniani yanayoongoza katika uzalishaji wa *nickel, copper* na *cobalt*. Tangu mwezi Februari, 2004, kampuni hiyo imekuwa ikifanya tathmini ya mradi ili iweze kufanya uamuzi wa

kuingia ubia na mmiliki wa sasa wa mradi huo, *Barrick Gold Corporation.* Iwapo makubaliano yatafikiwa, kampuni hiyo inatarajiwa kutumia *US$* 45 milioni kufanya uchunguzi zaidi na kukamilisha upenguzi yakinifu ndani ya miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa dhahabu kwa kuzingatia maoni na hisia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine juu ya udhibiti wa madini hasa kwenye migodi mikubwa, Serikali iliajiri Kampuni ya Kimataifa ya *Alex Stewart (Assayers) GBC* ya Marekani ili kuhakiki uzalishaji na uuzaji wa dhahabu kutoka migodini. Serikali iliingia mkataba wa miaka miwili na kampuni hiyo mwezi Juni, 2003. Kazi ya uhakiki inayofanywa na kampuni hiyo imegawanywa katika sehemu mbili ambazo ni kukagua uzalishaji na usafirishaji wa dhahabu na kukagua gharama za uwekezaji na uzalishaji. Kazi ya sehemu ya kwanza ilianza Julai, 2003 na ya pili ilianza mwezi Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika kikao cha Bunge la Bajeti ya mwaka 2003/2004, Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja nyingi kuhusu sekta ya madini. Kwa kuzingatia hoja hizo, mwezi Februari, 2004 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda kamati maalumu ya kudurusu Sera ya Madini. Kamati hiyo inayoongozwa na Dr. Jonas Kipokola ina Wajumbe watano akiwemo Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda. Wajumbe wengine wanatoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shirika la Maendeleo la Taifa na sekta binafsi. Kamati hiyo itaangalia mambo yafuatayo: Taratibu za uwekezaji kwenye sekta ya madini, hasa umiliki wa hisa kwenye migodi, mfumo wa kodi na vivutio kwenye sekta ya madini, namna ya kuvutia wawekezaji ili kukuza uwezo wa kuongeza thamani ya madini kabla ya kuyasafirisha nje, usimamizi wa shughuli za uchimbaji na utoaji huduma kwa wachimbaji wadogo na namna ya kuondoa vikwazo kwenye biashara ya madini na kuondoa migongano kati ya wadau kwenye sekta ya madini. Kamati hiyo ilipewa miezi mitatu hadi Mei, 2004 kukamilisha kazi yake. Hata hivyo, baada ya kubaini ukubwa wa kazi yenyewe, Kamati imeongezewa muda hadi Agosti, 2004. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa ushauri ambao Serikali itapata kutoka kwenye Kamati utafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu wananchi wa Kijiji cha Mtakuja na vitongoji vyake huko Geita kutokupata fidia waliyostahili wakati wa kuanzishwa kwa mgodi wa *Geita Gold Mining Limited.* Serikali, kwa nia ya kumaliza kero hiyo, ilitoa fedha na kuunda Kamati mwezi Januari, 2004 ambayo iliwasilisha taarifa yake mwezi Machi, 2004. Kamati hiyo ilipendekeza kuwa madai yote ambayo imebaini kuwa ni ya kweli yalipwe na yamekwishalipwa. Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita amewalipa wananchi ambao hundi zao zilichacha. Kufuatia malipo yaliyofanyika, zoezi la ulipaji fidia Geita limemalizika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mfumuko wa uchimbaji wa dhahabu katika maeneo kadhaa nchini yakiwemo yale ya Idiwili Wilayani Mbozi, Sakale Wilayani Muheza na sehemu kadhaa Mkoani Morogoro kama Melela, Dete na Kisanga. Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa na Wilaya imekuwa ikifuata taratibu za kutenga baadhi ya maeneo hayo kuwa maalumu kwa wachimbaji wadogo wa madini. Kamati ya Ushauri wa Madini, pamoja na mambo mengine, hunishauri kuhusu utengaji wa maeneo

hayo, na ugawaji hufanywa na kamati ambayo mwenyekiti wake ni Mkuu wa Wilaya. Maeneo ya mfumuko wa uchimbaji wa madini yanayohusika ni yale ambayo yanaruhusiwa kisheria kuchimbwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekwishatenga maeneo kadhaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Maeneo hayo ni ya uchimbaji wa almasi katika Kijiji cha Maganzo Mkoani Shinyanga na uchimbaji wa dhahabu katika maeneo ya Nyamtukuza Wilayani Kibondo na Sakale Wilayani Muheza. Maeneo hayo yatatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuongeza udhibiti katika machimbo ya tanzanite Wilayani Simanjiro. Baada ya kulitangaza eneo hilo kuwa eneo maalumu *(Mererani Controlled Area)*, vituo vya ukaguzi *(checkpoints)* kwenye sehemu za kuingia na kutoka kwenye machimbo vimejengwa. Aidha, vitambulisho maalumu kwa wachimbaji na wahusika wengine vimeshaandaliwa na ununuzi wa uzio maalumu umefanyika. Hivi sasa mkandarasi anaendelea kutengeneza njia ili kupitisha uzio huo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, mwezi Juni, 2004 Wizara iliendesha mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa Mererani ili kuwaelimisha juu ya Sheria ya Madini na kanuni zake; Sheria ya Baruti na kanuni zake; njia bora na salama za uchimbaji, matumizi bora ya baruti, kuhifadhi mazingira machimboni na tahadhari dhidi ya UKIMWI. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza tija na usalama wa wachimbaji. Mafunzo kama hayo pia yaliendeshwa Mjini Tanga mwezi Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mradi wa mazingira unaofadhiliwa na *Global Environment Facility (GEF)* wenye lengo la kutunza mazingira na afya za wananchi katika maeneo ya uchimbaji dhahabu. Kupitia mradi huu, wataalam wa mazingira na afya walitoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Rwamagaza Wilayani Geita. Mradi huu unaojulikana kama *Global Mercury Project* unatekelezwa pia katika nchi nyingine tano duniani ambazo ni Brazil, Indonesia, Laos, Sudan na Zimbabwe. Uzoefu utakaopatikana katika nchi hizi utatumiwa ili kupunguza madhara ya zebaki kwa wachimbaji wadogo na jamii zao katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata katika mradi huo ni kuandaa maonyesho ya teknolojia bora ya kuchenjua dhahabu ambapo lengo ni kwamba vifaa vitakavyoonyeshwa vitapatikana kwa urahisi humuhumu nchini, kwani mradi utawafundisha wenye karakana za ufundi, hususan *VETA,* jinsi ya kutengeneza na kueneza vifaa hivyo. Aidha, taratibu za kutoa mikopo midogo ya kununulia vifaa hivyo zitaandaliwa na wachimbaji watapata mafunzo ya namna ya kuvitumia wakati wa maonyesho hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kueneza teknolojia bora ya uchimbaji mdogo wa madini kwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha uchenjuaji dhahabu cha Matundasi Wilayani Chunya. Lengo la kituo hicho ni kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu juu ya njia bora na salama za uchenjuaji dhahabu. Kituo hicho kimeanza kutoa huduma ya kukodisha vifaa vya uchimbaji kwa gharama

nafuu na kutoa ushauri wa kitaalamu. Mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo yataanza mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utunzaji wa mazingira kwa kukagua maeneo ya migodi na kutoa ushauri juu ya kuboresha mazingira. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais ilihamasisha wachimbaji kushiriki katika shindano la Tuzo ya Rais ya Uongozi na Utunzaji Bora wa Mazingira katika Uchimbaji wa Madini. Katika mwaka 2004, jumla ya washiriki wanane, yakiwemo makampuni sita ya wachimbaji wakubwa na wa kati na wachimbaji wadogo wawili, wamejitokeza kushiriki kwenye kushindania tuzo hiyo. Ukaguzi wa maeneo ya washindani unafanyika na kitakachofuata ni kuwapendekeza washindi.

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa madini nchi za nje kwa mwaka 2003 ulifikia *US$* 560 milioni ikilinganishwa na *US$* 430 milioni mwaka 2002. Ongezeko hilo limetokana na uzalishaji wa dhahabu kwenye migodi mikubwa kuongezeka na kupanda kwa bei ya madini hayo katika soko la dunia. Dhahabu ilichangia takriban asilimia 90 ya mauzo yote ya madini nchi za nje kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya kuwasilisha bajeti ya mwaka 2003/2004, Waziri wa Fedha alitangaza kusudio la Serikali la kupiga marufuku usafirishaji nje wa tanzanite ghafi. Kufuatia tamko hilo, Wizara ilituma ujumbe kutembelea nchi ambazo huchukua madini ya Tanzania kama malighafi. Nchi hizo ni India, Thailand pamoja na Italia ambayo ni maarufu duniani kwa usonara. Ziara zililenga kutoa fursa ya kujifunza na kuvutia uwekezaji. Ujumbe uliongozwa na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na ulimjumuisha Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Salome Mbatia. Wajumbe wengine walitoka Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, *TRA, TIC, NDC,* Chama Cha Wafanyabiashara wa Madini, *TAMIDA, AREMA* na mwakilishi wa wachimbaji wakubwa wa *Tanzanite.* Katika uandaaji na ufanikishaji wa ziara hizo, balozi zetu zilizoko nchini India, China na Italia zilitoa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu tuliyojifunza kutokana na ziara hizo ni pamoja na kwamba azma ya Serikali ya kusanifu tanzanite nchini inatekelezeka na italeta faida kubwa kwa Taifa. Mambo ya msingi ambayo Tanzania inabidi iyatekeleze kwa kasi ni pamoja na uanzishaji wa maeneo ya *EPZ* ambayo yanaweza kuharakishwa kwa kuyakaribisha mashirika ya *pension funds* nchini kuwekeza katika ujenzi wa majengo ya kupangisha katika maeneo hayo, kuongeza mafunzo ya ukataji vito ndani na nje ya nchi; kurekebisha mfumo wetu wa kodi na ukusanyaji wake, kuhamasisha ujasiriamali ili Watanzania wengi zaidi wajiingize katika usanifu wa vito na kuyawezesha mabenki kutoa mikopo. Masuala yote haya yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine yenye lengo la kufanikisha azma ya kusanifu tanzanite nchini, itakumbukwa kuwa Serikali iliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Madini yaliyopitishwa mwezi Februari, 2004 chini ya sheria ya *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2004*. Ni matumaini yetu kuwa kufuatia marekebisho hayo, wafanyabiashara wengi zaidi

wa vito watajitokeza kuwekeza katika ukataji wa vito kwani mrabaha umeondolewa kwa vito vilivyosanifiwa.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1996, Serikali imekuwa na kitengo huko London, Uingereza kinachojulikana kama *Tanzania Government Diamond Sorting Organisation (TANSORT).* Kitengo hicho kina jukumu la kuchambua almasi zinazochimbwa na mgodi wa *Williamson Diamonds Limited (WDL)* na kuzithamini kabla ya kuziuza kwa kampuni tanzu ya *DeBeers, Diamond Trading Company (DTC).* Kitengo kinaendeshwa kwa ada ya kuchambua almasi ambayo ni *US$* 4.50 kwa kila karati inayochambuliwa. Umuhimu wa *TANSORT* unatokana na haja ya kuzuia *transfer pricing* katika hali iliyopo kwamba, mmiliki wa hisa nyingi katika *WDL, De Beers,* ndiye mnunuzi pekee wa almasi za *WDL* kupitia *DTC*, hivyo anaweza kushawishika kujiuzia almasi za *WDL* kwa bei ya chini kuliko inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000, baada ya Wizara kubaini kuwa uendeshaji wa TANSORT ulikuwa haufuati taratibu za Kiserikali kutokana na sababu za kihistoria, iliunda kamati maalum ya Watendaji wa Serikali *(inter-ministerial committee),* kuichaunguza na kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kurekebisha hali hiyo. Kamati hiyo ilihusisha asasi muhimu zifuatazo: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Nishati na Madini. Kwa kuzingatia ushauri wa kamati hiyo, hatua zifuatazo zimechukuliwa: Mwaka 2001 *TANSORT* iliingizwa rasmi kwenye muundo wa Wizara, mwaka 2003 kibali kilitolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuhalalisha ajira ya *diamond sorters* wawili Watanzania wanochambua almasi huko *TANSORT* kama watumishi wa Serikali na kuanzia mwaka 2004/2005, *TANSORT* imeingizwa katika Bajeti ya Serikali. Hatua zitakazofuata ni kujaza rasmi nafasi ya Mkurugenzi wa *TANSORT* na kuhakikisha kuwa *TANSORT* inaimarishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kifedha na kiutawala za Serikali. Aidha, fedha zote zilizotokana na ada ya kuchambua almasi ambazo zimekuwa zikitunzwa na *DTC* kwa niaba ya Serikali zitahamishiwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni mwanachama wa kituo cha madini cha *Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC)* kilichopo Kunduchi, Dar es Salaam. Lengo kuu la kituo hicho ni kuunganisha nguvu za nchi wanachama kwa kuendesha mafunzo, kufanya utafiti na kuchunguza miamba, ili kuendeleza sekta yao ya madini. Gharama za uendeshaji wa *SEAMIC* zinatokana na michango ya nchi wanachama ambazo ni pamoja na Angola, Comoro, Ethiopia, Msumbiji, Tanzania na Uganda. Kwa sasa nchi hizo ziko katika hatua ya kuridhia mkataba unaokusudia kubadili umiliki wa *SEAMIC* kuwa katika msingi wa hisa na kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika umiliki wa kituo hicho. Michango ya nchi wanachama itatolewa hisa, na kila nchi itakuwa na umiliki kulingana na wingi wa hisa zake.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na ujenzi wa Chuo cha Madini, kazi inayojumuisha ujenzi wa maabara, maktaba, zahanati, nyumba za wafanyakazi na kiwanja cha michezo. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya ufundi sanifu katika nyanja za teknolojia ya uchimbaji, uchenjuaji na utafutaji wa madini. Kwa sasa uongozi wa

Chuo unakamilisha taratibu za kuwawezesha wahitimu wa kwanza wa mafunzo ya muda mrefu (ya miaka mitatu) kuweza kufanya mitihani ya Kitaifa mwezi Mei, 2005. Taratibu hizo zinafanyika kwa ushirikiano na Baraza la Taifa la Mitihani *(NECTA)* na Baraza la Vyuo vya Ufundi *(NACTE).* Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi yanayochukua hadi wiki nne, Wizara inaendelea kuwahimiza watu binafsi na wachimbaji wadogo kujitokeza kila chuo kinapotangaza mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilikuwa inaendelea na taratibu za kuiunda upya *STAMICO* kuwa Wakala wa Serikali wa kuendeleza madini ambayo hutumika kama malighafi viwandani na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wachimbaji wadogo. Wizara imeendelea na mashauriano na maandalizi na hivi sasa mapendekezo yamefikia hatua ya kuwasilishwa katika ngazi za juu Serikalini kwa uamuzi. Shirika linaendelea na shughuli za utafutaji wa madini katika maeneo ya leseni zake ambazo liliomba na kupewa na Wizara kama mwombaji mwingine yeyote. Katika baadhi ya leseni hizo, Shirika lina ubia na makampuni ya nje. Aidha, Shirika limeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa malipo kwa makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003, mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira ulizalisha tani 54,610 ya makaa yaliyosafishwa ikilinganishwa tani 79,210 mwaka 2002. Hali ya uzalishaji inazidi kuzorota kutokana na uchakavu wa vifaa na mitambo iliyoanza kutumika takriban miaka 20 iliyopita. Kwa kuwa mgodi ulijengwa kwa teknolojia, msaada na mkopo kutoka serikali ya China, juhudi za kumtafuta mbia ili aweze kuufufua mgodi huo zimekuwa zikielekezwa kwa makampuni kutoka China. Hata hivyo, kwa kuwa jitihada hizo za muda mrefu hazijazaa matunda, sasa *PSRC* imefungua milango kwa wawekezaji wengine watakaojitokeza.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake unategemea pamoja na mambo mengine elimu na afya ya watumishi wake. Katika kujenga uwezo wa Wizara kukabiliana na changamoto zinazoikabili, mwaka 2003/2004, Wizara iliwapeleka mafunzoni watumishi 94 chini ya mpango wake wa mafunzo. Kati ya watumishi hao, 15 walihudhuria kozi za muda mrefu na 79 walishiriki kozi fupi. UKIMWI umeendelea kuathiri nguvukazi ya Wizara. Mwaka 2003/2004, Wizara iliendesha semina za kujikinga na ugonjwa huo katika ofisi za Wizara nchini kote pamoja na kwenye maeneo manne ya uchimbaji mdogo. Katika bajeti ya mwaka 2004/2005, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuwahudumia watumishi watakaojitokeza ambao wameathiriwa na ugonjwa huo, pamoja na familia zao. Kwa kufanya hivyo, Wizara itatumia sehemu kubwa ya bajeti ya kupambana na UKIMWI kuwasaidia waathirika badala ya semina na warsha.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* zimekubali kushirikiana katika kuendeleza sekta ya nishati. Maandalizi yanafanywa ya kuwezesha gridi za umeme za nchi wanachama kuunganishwa. Aidha, warsha za pamoja zimekuwa zikiendeshwa na kuvutia wawekezaji katika utafutaji wa mafuta na kuendeleza majadiliano juu ya kuwianisha sera za nishati. Ushirikiano pia umeendelea katika utafiti juu ya namna ya kuendeleza nishati mbadala na matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika *EAC* na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* kwenye sekta za nishati na madini. Mwezi Machi, 2004 Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Mkakati wa Maendeleo wa *SADC, Regional Indicative Strategic Development Plan (RISDP),* ambao sekta za nishati na madini pia zitaufuata katika kuandaa mipango yake ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara zilikutana Dakar, Senegal mwezi Juni, 2001 na kuazimia kusitisha matumizi ya petroli yenye madini ya risasi *(Leaded Petrol)* ifikapo Desemba, 2005. Madhumuni ya azimio hilo ni kutunza mazingira na afya ya binadamu kutokana na athari mbaya za madini ya risasi. Katika kutekeleza azimio hilo, hivi sasa takriban asilimia 95 ya petroli yote inayoingizwa nchini haina risasi. Ili kuhakikisha kwamba hakuna tena uingizaji wa petroli yenye risasi, Serikali kuanzia sasa imeamua kupiga marufuku uingizaji wa petroli hiyo. Serikali imeliagiza Shirika la Viwango la Taifa kufuatilia utekelezaji wa uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, katika ushirikiano wetu na Jumuiya ya Kimataifa, mwezi Mei, 2004 ,Tanzania, ikiwa Mwenyekiti wa *SEAMIC,* ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa kila mwaka wa hicho ambao ulifanyika jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Viongozi wenzangu ambao kwa pamoja tumeweza kufanikisha shughuli za Wizara kwa mwaka 2003/2004. Kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, kwa msaada wake mkubwa alionipa katika kusimamia shughuli za Wizara. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Patrick Rutabanzibwa, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, viongozi wa mashirika yaliyo chini ya Wizara wakiwemo Watendaji Wakuu, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi na Kamati zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani kwa Serikali za nchi nyingine na mashirika ya Kimataifa kwa ushirikiano na msaada walioutoa katika kuendeleza sekta za nishati na madini. Naomba nizishukuru Serikali za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Ujerumani. Aidha, natoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi za Ulaya na kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, *DANIDA, Global Environmental Facility, IAEA, IMF, KfW, NDF, NORAD, SIDA, UNDP, UNESCO, UNIDO* na *USAID. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ina majedwali kadhaa kuanzia ukurasa wa 42 ambayo yanatoa taarifa au takwimu zaidi kuhusu baadhi ya mambo niliyoyagusia.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Same Mashariki kwa umoja, ushirikiano na kujitolea kwao katika kazi za maendeleo ya Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya Sh.179,933,476,200 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na mashirika yake kwa mwaka 2004/2005. Mchanganuo wa bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya maendeleo ni Sh.46,897,934,700 ambazo kati yake Sh. 5,199,552,300 ni fedha za hapa na Sh. 41,698,382,400 ni fedha za nje; na

(ii) Bajeti ya Matumizi ya kawaida ni Sh.133,035,541,500 ambapo Sh. 1,104,651,300 ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* na Sh. 131,930,890,200 ni matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wachangiaji wa nne wa mwanzo baada ya watakaotoa taarifa kwa niaba ya Kamati na Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Thomas Nyimbo na Mheshimiwa Stanley Kolimba. Najua wapo kwenye chai, lakini kama wamenisikia basi wajiandae kurudi ndani ya Ukumbi. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua makadirio haya, Mheshimiwa William Shelukindo.

**MHE.WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara *(Parliamentary Committee for Investments and Trade - INTRA)* kuhusu utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2003/2004, pamoja na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutekeleza masharti ya Kanuni ya 81(1), Toleo la Kanuni za Kudumu za Bunge la mwaka 2004, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa ushirikiano wao na kuwa makini wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti za Wizara zilizo kwenye *Portfolio* yake. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo, Mheshimiwa Omari S. Chubi, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa,

Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Christopher S. Wegga, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Aisha Phillipo Magina, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Khamis Awessu Aboud, Mheshimiwa Ismail J.R. Iwvatta, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga na Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed na mimi William H. Shellukindo, Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mtanzania la hivi karibuni kwa kutukumbusha kwamba, mtu hujitambulishi wewe mwenyewe kwa cheo chako ila kwa jina kwanza halafu ndiyo cheo. Namshukuru sana. Ndio maana sikujiita Mheshimiwa nimesema mimi William Shellukindo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilitoa ushauri mbalimbali wakati inajadili utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha wa 2002/2003 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2003/2004. Ushauri ulitolewa ulihusu maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa bei za umeme nchini bado ni kubwa pamoja na hatua zilizochukuliwa hivi karibuni kuvipunguzia Viwanda gharama hiyo kwa kutumia utaratibu wa kuondoa ruzuku iliyokuwa inatolewa kwa watumiaji wadogo. Aidha, mwezi Mei, 2004, Serikali ilipandisha bei ya umeme kwa watumiaji wadogo kutokana na sababu iliyotolewa ya kupanda kwa gharama za uzalishaji umeme kutoka Sh.63.47 kwa *unit* mwaka 2002 hadi Sh.81.67 kwa *unit* mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Uongozi mpya wa *TANESCO (Net Group Solutions),* za kuimarisha na kuboresha miundombinu ya umeme kutokana na kuongezeka kwa makusanyo ya fedha, bado tatizo la kukatikatika kwa umeme linaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuchelewa kuwaunganishia umeme wananchi, hili bado ni tatizo na kero kubwa miongoni mwa wananchi hususan pale ambapo mhusika amekwishalipia ada na malipo mengine kwa mujibu wa Mkataba wa kuunganishiwa umeme. Aidha, hali hii huashiria kuwepo kwa rushwa ndani ya *TANESCO* kwa hisia za wateja wake. Hili likichunguzwa vizuri pengine wanaweza kuondoa hiyo hisia kwamba mtu amelipa anakaa miezi mingi bila kuwekewa na pengine anafikiria atoe chochote. Kamati haijasema kuna rushwa *TANESCO* hapana, tunasema hii inaashiria kuwepo kwa rushwa.

Kuhusu Mkataba wa *Independent Power Tanzania Limited (IPTL),* pamoja na maelezo ya Wizara kuwa gharama za ununuzi wa umeme wa *IPTL (Capacity Charge)* itapungua mara mtambo huo utakapoanza kutumia gesi ya Songosongo, bado Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali kuharakisha majadiliano na Benki ya Dunia na Wawekezaji wengine kuhusu kuununua mtambo huo ili iondokane na gharama hii ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la migogoro kwenye maeneo ya machimbo ya madini bado linaendelea. Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea migodi kadhaa kwenye Mikoa ya Mara, Manyara, Tabora na Mwanza mwezi Aprili, 2004 na kujionea hali hiyo hususan kwenye migodi ya *Tanzanite* katika eneo la Mererani, Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, bado Kamati inasisitiza haja ya Wizara kutoa elimu ya kutosha kuhusu UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuanzisha vituo vya kutolea Ushauri Nasaha na kupima kwa hiari kwenye maeneo ya machimbo ya madini kwa kushirikiana na Taasisi na Asasi zinazojishughulisha na vita dhidi ya janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, makadirio ya makusanyo ya mapato yalikuwa Sh. 16,315,027,100/= na hadi kufikia mwezi Machi, 2004 kiasi cha Sh. 16,658,796,122/= ambazo ni sawa na asilimia 102 zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuvuka lengo la makadirio ya makusanyo ya mapato kwa asilimia mbili. Aidha, kuhusu fedha za matumizi, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara ilitengewa Sh.127,457,538,800/= ambapo Sh. 25,365,980,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.102,091,552,300/= ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo ya Sh. 102,091,552,300/=, kiasi cha Sh. 5,199,552,300/= ni fedha za hapa na Sh.96,892,000,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka 2003/2004, Wizara imepata mafanikio yafuatayo:-

- Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kuboresha Utendaji Kazi Serikalini, yaani *Performance Management System.*

- Upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kipindi cha miezi kumi mfululizo kuanzia Aprili, 2003 hadi Februari, 2004. Katika kipindi hicho, kulikuwa na tukio moja tu la kukatika kwa umeme katika Gridi ya Taifa.

- Upoteaji wa umeme umepungua kutoka asilimia 27 mwaka 2002 hadi kufikia asilimia 23 mwaka 2003.

- Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya *TANESCO* kutoka wastani wa Sh. 10bn/= hadi kufikia wastani wa Sh. 16bn/=.

- Kukamilika kwa ujenzi wa Bomba la Gesi ya Songosongo ambayo itatumiwa na wateja wa viwandani.

- Kupatikana kwa Mshauri *(Consultant)* kwa ajili ya kuendeleza nishati ya jua Vijijini chini ya mradi wa huduma za umeme Vijijini ambao utaendelezwa kwa majaribio Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati haikuona mantiki ya kufanyia majaribio mradi wa huduma za Umeme Vijijini katika Jiji la Mwanza wakati Mradi unawalenga Wananchi waishio Vijijini. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Wizara kuhamishia majaribio hayo Vijijini hukohuko Mkoani Mwanza ili ufanisi wake upimwe katika mazingira halisi ya Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa yalijitokeza matatizo mbalimbali wakati wa utekelezaji wa mpango wa Wizara na Bajeti ya mwaka 2003/2004, baadhi yakiwa ni pamoja na ukame, bajeti finyu, udhibiti mdogo wa biashara ya madini na kadhalika. Vilevile, Kampuni ya *Antrim Resources Limited* kushindwa kutafuta Mafuta katika maeneo ya Leseni yake kutokana na Serikali ya Zanzibar kutotoa idhini ya kufanya hivyo hadi wakati wa kujadili mapendekezo ya malengo ya Bajeti ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, maeneo yafuatayo yamepewa kipaumbele:-

- Uhamasishaji wa wawekezaji kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Nishati na Madini.

- Uwekaji wa muundo muafaka utakaowezesha uhamasishaji wa utaratibu bora wa sekta binafsi pamoja na sekta ya umma kushirikiana katika kuwekeza kwenye nishati mbadala.

- Uimarishaji wa mfumo wa kuzalisha na kusambaza umeme wa uhakika kwa maeneo ya Mijini na Vijijini.

- Uimarishaji wa uwezo wa kukusanya, kutunza na kuchambua takwimu kwa ajili ya ukusanyaji zaidi wa mapato kutokana na Sekta za Nishati na Madini.

- Uboreshaji wa mazingira na kuwasaidia wachimbaji wadogo kuongeza tija katika uzalishaji madini.

- Kuweka utaratibu endelevu katika Sekta za Nishati na Madini na kuhakikisha kwamba mazingira yanatunzwa.

- Uendelezaji wa utafiti wa awali *(Basic Exploration)* katika Sekta za Nishati.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kuchambua kwa kina makadirio ya matumizi na mapato ya Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini na kazi zilizopangwa kwa mwaka 2004/2005, Kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuboresha utekelezaji wa kazi hizo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme hapa nchini bado ni kubwa pamoja na hatua zilizochukuliwa hivi karibuni kuvipunguzia Viwanda gharama hiyo kwa kuondoa ruzuku iliyokuwa inatolewa kwa watumiaji wadogo. Aidha, mwezi Mei, 2004, Serikali ilipandisha bei ya umeme kwa watumiaji wadogo kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni

kupanda kwa gharama za uzalishaji umeme kutoka Sh.63.45 kwa *Unit* mwaka 2002 hadi Sh.81.67 kwa *unit* mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa njia endelevu ya kulitafutia ufumbuzi tatizo hili ni kuweka mkakati wa kuendeleza vyanzo vingine vya umeme kama vile Makaa ya Mawe ya Mchuchuma yenye uwezo wa kuzalisha *MW*.400, matumizi ya Gesi iliyokwishapatikana ya Songosongo na miradi mingine ya gesi iliyo katika maeneo mengine kwa mfano ya *Mnazi Bay* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha mradi wa utafiti wa Umeme Vijijini *(Rural Electrification Study),* ambao hata hivyo haukutengewa fedha zozote za ndani katika mwaka huu wa fedha. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kutekeleza mapema iwezekanavyo, uanzishaji wa Wakala wa Umeme Vijijini *(Rural Energy Agency - REA)* na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund - REF),* kama ilivyopitishwa na Bunge hili. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za kuwaunganishia umeme Wananchi Vijijini ili nishati hiyo iwafikie Wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea maelezo kuwa majadiliano kuhusu ununuzi wa *IPTL* yanaendelea kati ya Serikali, Benki ya Dunia na Wawekezaji ili mtambo huo uweze kununuliwa na Serikali. Pamoja na maelezo kuwa gharama za Umeme *(Capacity Charge)* ya *IPTL* itapungua mara mtambo huo utakapoanza kutumia gesi asilia ya Songosongo, Kamati inaendelea kuzidi kuishauri Serikali kununua mtambo huo ili kuepusha gharama hizo za kudumu. Kamati pia inaishauri Serikali kuwa makini wakati wa kusaini Mikataba na makapuni binafsi ya aina ya *IPTL* ili kuondokana na hisia hisia hizi ambazo zinapoteza wakati.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuchelewa kuwaunganishia umeme wateja, limekuwa sugu na kero miongoni mwa wahusika hususan pale ambapo mteja amekwishalipia ada na gharama nyingine kwa mujibu wa Mkataba lakini anakaa muda mrefu. Aidha, tatizo hili halionekani kupungua pamoja na taarifa kuwa makusanyo ya fedha za *TANESCO* yameongezeka kutoka Sh. 10bn/= hadi Sh. 16bn/= kwa mwezi. Kwa hiyo, Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake wa mwaka 2003 kwamba, *TANESCO* ihakikishe kuwa ina mkakati maalum wa kutatua tatizo hili na uwasilishwe Wizarani na Wizara iweze kuutoa kwa Kamati nayo iweze kuutafakari.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta zimepanda kwa kiasi ambacho kinatishia maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, ongezeko hilo kubwa la bei, limesababisha bei za bidhaa na huduma za usafiri kupanda. Kufuatia hali hii na wakati huohuo kuzingatia kuwa tuko katika uchumi wa soko, lakini uchumi wa soko unahitaji kuongozwa na kudhibitiwa *(to be guided and regulated),* kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali ifuatavyo:- .

Uwekwe utaratibu wa udhibiti wa bei za mafuta ili kuepusha athari zinazoweza kutokea katika uchumi na maeneo mengine ya maisha ya Watanzania kutokana na upandishaji holela wa bei za mafuta. Aidha, Serikali iweke utaratibu wa kutoa taarifa za

mara kwa mara kuhusu mabadiliko ya bei za mafuta katika Soko la Dunia ili punguzo au ongezeko la bei la mafuta lijulikane wazi kwa wadau wote. Isiwe siri ya Makampuni ya Mafuta peke yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC),* bado lina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Lakini fedha za maendeleo zinazotengewa *TPDC* ni kidogo sana. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kati ya Sh.1bn/= zilizotengwa ni Sh. 230m/= tu ndizo zilizotolewa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, Kamati inapenda kutoa ushauri ufuatao: Serikali ianzishe Mfuko Maalum kutokana na Tozo la mauzo ya mafuta na gesi ili kuisaidia *TPDC* iweze kutekeleza majukumu yake, kwa niaba ya Taifa na sambamba na hilo, Serikali ilete Bungeni mapema iwezekanavyo, marekebisho ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta ya mwaka 1980 *(The Petroleum Exploration and Production Act of 1980*) ili kuwezesha utafutaji wa mafuta eneo la bahari ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanyika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Jengo la Mafuta *(Mafuta House),* linalomilikiwa na *TPDC* ni kitega uchumi muhimu katika utekelezaji wa shughuli zake hasa wakati huu ambapo Serikali imejiondoa katika shughuli za uchumi na biashara. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kutafuta uwezekano wa kuidhamini *TPDC i*li ipate fedha za kumalizia ujenzi wa jengo hilo. Aidha, kwa kuwa tayari *TPDC* na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* wamewekeza Sh.15bn/=, Wizara isaidie kuhamasisha Makampuni mengine kuwekeza kiasi cha fedha kinachohitajika cha Sh. 10bn/= ili kukamilisha jengo hilo na kugawana hisa. Vilevile, Kamati haioni kuwa ni busara kutoa Jengo hilo kwa Taasisi nyingine bila kuzingatia uwekezaji uliokwishafanywa na *TPDC* na *National Housing Corporation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na marekebisho yote, Nyongeza ya Kwanza kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 4(3), Maliasili ya Mafuta pamoja na gesi asilia ni Mambo ya Muungano. Kwa mantiki hiyo, hakuna tatizo litakalotokana na ugawanaji wa mapato yanayotokana na rasilimali hiyo iwapo mafuta au gesi itapatikana katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano. Hivyo, Kamati inazishauri Serikali zote mbili kuwasiliana na kushirikiana kwa karibu katika suala hili ili kuondoa hisia ambazo zinaweza kuchelewesha Taifa kunufaika na maliasili ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha migogoro kwenye migodi ya machimbo ya madini, Kamati inashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Ushirika na Masoko kuhamasisha Wachimbaji Wadogo kuanzisha Vikundi vya Ushirika kwenye maeneo hayo. Hii itawasaidia kuweka nguvu zao pamoja na kuviwezesha kupata mikopo ya kuvijengea ujasiriamali pamoja na tija.

Mheshimiwa Spika, imedhihirika wazi kwamba, biashara ya Vito *(Gemstones)* haihitaji uwekezaji mkubwa tofauti na uchimbaji wa madini mengine kama dhahabu na almasi. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kuitenga biashara hiyo ili ibaki mahsusi

kwa Wazalendo tu. Napenda kurudia, kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali kuitenga biashara hiyo ya vito kubaki mahsusi kwa ajili ya wazalendo. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, kuliteua eneo la Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro *(KIA)* kuwa Ukanda wa Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo ya Nje *(Export Processing Zone - EPZ)* ili kurahisisha usanifu na usafirishaji wa Vito. Usafirishaji wa Vito haufai kufanyika kwa masafa marefu barabarani. Wanunuzi wa Vito watafurahi kutumia muda mfupi kutua, kununua na kuondoka *(Land, Buy and Take off)*. Eneo la *KIA* lina vigezo muhimu katika kuanzisha *EPZ* ya Vito vya *Tanzanite*, kwa mfano, umeme wa uhakika, usafiri wa ardhini na angani wa uhakika na mazingira ya kuvutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo ya *TANESCO* Kidatu ambayo hapo awali yalikuwa yanatumika kama kambi ya Wafanyakazi hivi sasa hayatumiki kwa kazi hiyo. Hivyo, ili kuyaokoa majengo hayo kutokana na uchakavu na uharibifu, Kamati inaishauri Wizara kuyatoa majengo hayo ili yageuzwe kuwa Shule ya Sekondari. Ushauri huu unaimarisha na kuongeza kasi ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari itakayoanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2004/2005, kama ilivyotamkwa Bungeni na Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpogeza Mheshimiwa Daniel Ndhira Yona, Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati yangu wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Watendaji wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa ushirikiano wao wakati Kamati inatekeleza jukumu hili zito. Pia namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Kipenka Msemembo Mussa na Katibu wa Kamati hii Bwana Daniel Eliufoo, kwa kuihudumia Kamati hii ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi uliofanyika na ushauri uliotolewa na Kamati, Kamati kwa jumla imekubaliana na Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa katika Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini ni: Matumizi ya kawaida *(Recurrent Expenditure)* Sh. 133,035,541,500/= na Miradi ya Maendeleo *(Development Budget)* Sh. 46,897,934,700/=. Jumla yote ni Sh. 179,933,476,200/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka mwingine tena wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, nasimama hapa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kutoa maoni yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu Na. 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam kwa kuiandaa bajeti yao, bajeti ya kutuomba tuwape Sh.179,933,476,200/= za kutekeleza na kusimamia mipango iliyopangwa chini ya ofisi yao kwa kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nishati inayotumika katika nchi yetu vyanzo vyake ni maji *(hydropower),* mafuta na nishati inayotokana na misitu (kuni na mkaa), kuni na mkaa hutokana na misitu ya asili na misitu ya kupandwa, hii inachukua asilimia 93 ya nishati yote inayotumika katika nchi yetu. Umeme kama sehemu ya nishati inachangia 0.6% tu ya nishati nzima inayotumika.

Mheshimiwa Spika, nishati itokanayo na upepo na jua ni njia pekee inayoweza kuwapatia wananchi wetu wa Vijijini ambao kupata umeme wa *Grid* ya Taifa ni ndoto kwa sasa. Hii inatokana na ukubwa wa nchi yetu na gharama, tofauti ya matumizi ya nishati inayochangiwa na hali ya hewa, matumizi ya nishati hizi mbadala ni muafaka. Tunahitaji kutumia nishati upepo, *Windmill* moja inaweza kuzalisha kati ya 400 hadi 50,000 *Watts* na hii inategemea ukubwa wa hiyo *windmill* na nguvu ya kasi ya upepo.

Mheshimiwa Spika, nishati itokanayo na jua *(Sollar Power)* inaweza kuzalisha umeme kwa matumizi ya vitu vingine vitumiavyo umeme majumbani.

Mheshimiwa Spika, nishati ya upepo na jua ni nishati mbadala ya ile inayotokana na mafuta, maji na misitu bila kusahau makaa ya mawe; uendelezaji wake bado ni wa kiwango cha chini sana katika nchi, licha ya kwamba hiyo ndio njia ambayo ingepunguza matumizi ya kuni, mkaa na mafuta kwa wananchi waishio Vijijini. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani, inaona bado tuna matatizo kuwa, ruzuku inayotolewa kwa *TANESCO* ingekwenda kwenye uendelezaji wa nishati hizi za upepo na jua, basi sasa hivi tusingekuwa tunatupiana mpira juu ya kueneza umeme Vijijini na kupunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa *UNDP* inafadhili *NGOs* nyingi ambazo zinafanya kazi ya kueneza umeme kwa kutumia nguvu upepo na *solar.* Tungeishauri Serikali ishirikiane na *UNDP* kufanya mradi huu uwe ni wa Kitaifa kuliko kubakia kama *Pilot Project* tu.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya Tanzania ni wafugaji, hivyo uwezekano wa kutumia nishati ya *Biogas* inayotokana na kinyesi cha mifugo ni mkubwa sana. Kwa hiyo, tunaikumbusha Wizara ijipange sawasawa kuwafikishia wananchi waishio vijijini teknolojia hiyo ili waweze kujijengea chanzo imara cha nishati badala ya kutumia kinyesi cha ng'ombe kama kuni.

Mheshimiwa Spika, *Biogas Power Station* ni maarufu sana katika nchi za German na Denmark, ambapo kila *station* inaweza kutumiwa na viwanda vikubwa 20. Hii tunadhani inaweza kuwa ni ukombozi kwa Wananchi wengi badala ya kutegemea nishati ya mafuta na maji ambavyo hata ujenzi wake ni wa gharama kubwa. Wanyama tunao kinachotushinda ni hulka ya kuamini kuwa *hydropower* na *thermal power* ndio njia pekee ya kujenga nishati.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inao wataalamu wengi katika nyanja hizi za nishati ya umeme itokanayo na upepo, jua na *Biogas* kama ambavyo wamekuwa wakiendesha Miradi ya Majaribio katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu chini ya ufadhili wa *UNDP.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamshauri Waziri na Timu yake wasione kuwa umeme ni lazima utokane na *TANESCO* au *IPTL,* Tanzania kuna wataalam wengi ambao hawapati nafasi ya kuishauri Serikali kutokana na ukiritimba na Umimi, kitu kinachotuletea matatizo katika sekta nyingi na kuendelea kutufanya kuwa maskini na wategemezi wa ushauri kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO* alishauri njia bora ya kuongeza utendaji na uwajibikaji wa Shirika hilo kwa umma kuwa ni kuligawa Shirika hilo kuwa Mashirika binafsi tofauti tofauti, *TANESCO* ikawa *Single Transmission Company and Several Privately owned Regional Distribution Companies.*

Kambi ya Upinzani inauliza Serikali ushauri huu haiuoni kuwa ni wa maendeleo zaidi na inauzingatia vipi kwa maendeleo ya Mikoa yetu?.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji umeme kutokana na maporomoko ya maji nchini unategemea mito ya Pangani na Ruaha na mpaka sasa Mradi wa *Lower Kihansi* nao una uwezo wa kutoa *180 MW.*

Kambi ya Upinzani inaomba maelezo kutoka kwa Waziri, maeneo ambayo yameshaonekana kuwa yanaweza kutoa vyanzo vya umeme kama vile Rumakali ambayo ina uwezo wa kuzalisha *204 MW*, Ruhudji *250 MW,* Mpanga *160 MW, Stiggler's Gorge 1400MW, Rusumo Falls 180 MW* na *Upper Kihansi 40 MW.* Serikali ina mpango gani na maeneo haya kuyafanya yaweze kuzalisha umeme ambao utatosha kabisa kwa matumizi ya nchi na kuuza sehemu ya nishati hiyo kwa majirani zetu?

Mheshimiwa Spika, *Rural Electrification Policy,* inaruhusu wazalishaji binafsi wa nishati ya umeme, kutokana na nishati mbadala ya aina yoyote ile na kwa madhumuni ya wananchi waishio vijijini. Makampuni binafsi yangepewa ruhusa ya kujenga *Power*

*Stations* na kuuza umeme kwa watumiaji wengine badala ya kuiuzia *TANESCO* peke yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza hivi sasa tuko kwenye soko huria, hakuna sababu ya *TANESCO* kuhodhi biashara ya nishati ya umeme. *TANESCO* kama Shirika la Serikali linaweza kubaki kama *regulatory body*, badala ya kuhodhi shughuli na biashara nzima ya uzalishaji na usambazaji wa umeme. Kwa kuruhusu makampuni mengine kwenye biashara ya umeme wananchi wengi watapata huduma hii kwa haraka na kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali imetangaza kufuta deni ambalo *TANESCO* ilikuwa inalidai Shirika la Umeme la Zanzibar.

Kambi ya Upinzani na Wananchi wanauliza hayo mabilioni yaliyofutwa yanarudishwa kwa njia gani au ndiyo kwa kuwapandishia bei ya umeme wateja kama ilivyotokea hivi karibuni?

Mheshimiwa Spika, Utendaji kazi wa *TANESCO* chini ya Utawala wa *Net Group Solutions*, haujaonyesha ufanisi kama ilivyokuwa inaaminika baada ya kuwaondoa Watanzania waliokuwa wanaongoza Shirika la Umeme, bado umeme unakatika kama ilivyokuwa wakati akina Luhanga walipokuwepo. Umeme bado unapanda bei na hakuna dalili za kushuka na hii inatokana na ukweli kwamba, wao wanafanya kazi ya kuendeleza miundombinu iliyopo badala ya kuongeza miundombinu katika Wilaya ambazo hazijawahi kuwa na umeme toka tupate uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini uwezo waliopewa *Net Group Solutions* na Serikali, wangelipewa Watanzania wangeifanya *TANESCO* kuwa Shirika lenye nguvu na la kujiendesha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, Serikali kutokana na sababu inazozielewa yenyewe, huwa inashindwa kuzipa nguvu *Management* za Watanzania kama *TANESCO*, kazi inayofanywa na Utawala wa *Net Group Solutions.* Tunaamini kabisa Watanzania wasingelishindwa kama wangelikuwa wanalindwa na Serikali katika utendaji wao bila ya kuingiliwa na Watendaji wengine wa Serikali kama ambavyo Utawala wa leo wa *Net Group Solutions* unavyofanya kazi. Tunauliza hivi marupurupu wanayopata hao watu wa *Net Group Solutions* ni sawa na waliyokuwa wanapata uongozi uliopita? Je, baada ya *Net Group Solutions* kuja Mtera imejaa maji mbona tunafahamu kuwa *Mtera Dam,* haijajaa maji kwa mwaka uliopita. Tunaamini Watanzania wamehukumiwa kwa matatizo ambayo siyo ya kwao. Hivyo, tuwalinde na kuwathamini wataalam wetu kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha suala la nishati, naomba nitoe na kuomba maelezo kuhusu Mkataba wa Serikali na *IPTL*. Watanzania kama sehemu ya Serikali, wana haki ya kuelewa nini kilichomo katika mikataba ya uwekezaji na mikopo inayopewa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, *IPTL* ni Kampuni binafsi, sasa kitu cha ajabu ni Serikali kutoa ruzuku kwa kampuni hiyo wakati kila mwezi *TANESCO* au Serikali inalipa mabilioni ya shilingi kwa Kampuni hiyo. Kwa hilo Kambi ya Upinzani inaomba maelezo ya kina toka kwa Waziri, kwa manufaa ya walipa kodi na wananchi wote. Kama Kampuni binafsi, ni tegemeo letu fedha inayolipwa kila mwezi kiasi cha shilingi bilioni tatu zingekuwa ndiyo malipo ya mauzo ya umeme kwa *TANESCO.* Leo tunaambiwa Serikali inawapatia *IPTL* kiasi cha shilingi bilioni 18 kama matumizi ya kawaida kwa bajeti ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliopewa dhamana na kuaminiwa na kuwakilisha kwenye maslahi ya nchi yao. Lakini mambo yanavyoonyesha wamesalitiwa na watu waliowapa dhamana hiyo. Wasiwasi ambao Kambi ya Upinzani inao ni kwamba, kizazi kijacho pindi kikishaanza kuona udhaifu na uzembe ambao sisi tumeufanya, watafukua makaburi yetu na kuanza kuchapa bakora mafuvu yetu kwa kutuona tulikuwa watu wa ajabu ambao tulikuwa tunaingia mikataba bila kuielewa vyema pamoja na madhara ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunanyimwa kuangalia mikataba ambayo Tanzania inaingia na wabia, lakini kwa kipindi kijacho, mikataba hiyo itakuwa wazi kutokana na kukua kwa *Technology.* Mfano ni mikataba ya akina Machifu Magungo wa zamani, ya kuuza nchi kwa shanga na vioo tu, hivyo hivyo na sisi kwa kizazi kijacho tutaonekana watu wa ajabu sana.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu *IPTL* ni mali ya *VIPEM* na *Mechmar Corporation of Malaysia* na hiyo *ownership* haijafutwa. Je, Serikali ina uhalali gani wa kupeleka shilingi bilioni 18 kama matumizi ya kawaida kwa *IPTL* na bado kuna bili ya shilingi bilioni tatu kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, hapo kuna kitu ambacho hakieleweki, kwani katika majibu ya Serikali kwa Kamati, Serikali inaonyesha kama ina-*own IPTL* mpaka kufanya makubaliano na *World Bank* ya kubadili mitambo ya *IPTL* ili itumie Gesi ya Songosongo badala ya mafuta, kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji. Hapa tunajiuliza makubaliano haya kwa nini yafanywe na Serikali badala ya mwenye mali? Tunataka majibu kama Serikali ina umiliki wa aina yoyote katika *IPTL* kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haina ugomvi na kuwepo kwa *IPTL* ila ni kwa namna gani imeingia nchini na mikataba yake na *TANESCO* na Serikali. Kuna giza nene linaambatana na Mkataba wa *IPTL.* Tunamwomba Waziri atueleze kama kuna *tender* iliyotolewa kwa wawekezaji ili washindane na ni makampuni mangapi yaliomba?

Mheshimiwa Spika, *IPTL* inaweza kuwa ni jibu la kudumu la ukatikaji wa umeme, lakini haiwezi kuwa jibu la upatikanaji wa umeme wa kuaminika kwa nchi yetu. Tunataka Serikali ifanye uamuzi wa kuinunua *IPTL* ili kutuondolea mzigo huu. Mheshimiwa Waziri, ameshasema katika *speech* yake kwamba, kuna matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa tumezungumza juu ya madini jinsi yanavyoporwa na wawekezaji kutokana na mikataba mibovu, ni Serikali ya Tanzania pekee ulimwenguni ambayo madini yanachimbwa na makampuni ya nje, bila ya kuwa na *share* ya aina yoyote. Bulyanhulu inamilikiwa 100% na *Canadian Company, Geita Gold Mines* na kadhalika, zote ni mali ya wageni. Hii ina maana chochote kinachopatikana kama faida, Tanzania haipati gawio la aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, tulishauri mikataba hii iangaliwe upya. Serikali imeteua Kamati Maalum. Tunaiachia Serikali ihimize na kuyaleta Bungeni mapendekezo ya Kamati ili kuliwezesha Bunge kutunga sheria ambayo italazimisha makampuni ya madini kuingia ubia na Serikali hata kama ni kwa asilimia 25 kwa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuipongeza Serikali ya Awamu ya Kwanza kwa kuanzisha *TANSORT,* chombo cha kuchambua almasi yote inayotoka Tanzania, kwa kuwa huko nyuma mzalishaji mkubwa wa almasi alikuwa ni *Williamson Diamonds*, kwa kuwa sasa wapo wazalishaji wengine tunashauri kuwa *TANSORT* iwe mchambuaji mkuu wa almasi yote itokayo Tanzania, vile vile *TANSORT* iwe *Executive Agency* ili ifanye kazi ya kibiashara na ikiwezekana iweze kutoa huduma hiyo kwa nchi nyingine zinazozalisha almasi. Aidha, tunaishauri Serikali izungumze na nchi za Afrika zinazozalisha almasi ili tuunde umoja wetu chini ya mpango wa *NEPAD,* kama *OPEC* na vitu vingine ili tuweze kulidhibiti soko na uzalishaji wa almasi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amehoji kuwa kuna fedha zinazotokana na uchambuzi wa almasi, tunaomba Waziri atuelezee yafuatayo:-

(a) Ni kwa nini Serikali ilichelewa kujibu hoja hizi?

(b) Ni kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi katika matumizi ya fedha hizi?

(c) Ni hatua gani inayochukua Serikali katika kudhibiti matumizi ya fedha hizi zinazotokana na uchambuzi wa almasi?

Mheshimiwa Spika, suala la *TANSORT* limeshtua Watanzania wengi. Tunaitaka Serikali itoe ufafanuzi wa shughuli za *TANSORT* na wajibu wake kwa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inaonekana *TANSORT* ina salio la fedha zaidi ya shilingi bilioni mbili ambazo ziko kwenye *account*. Hii ni fedha kwa ajili ya nchi na kama ikitolewa itaziba mapengo mbalimbali ya bajeti ya Wizara hii. Kwani kwa kufuatana na *Controller and Auditor General's Report, TANSORT* kwa muda mrefu imekuwa na tatizo la kurejesha *sorting fees* kwa *Exchequer Account* kiasi cha shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, tunataka Waziri atujibu suala hili na kuamuru *TANSORT* warejeshe fedha hiyo kwa matumizi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunataka kufahamu, *TANSORT Office* iliyoko London imekuwa ikijiendesha yenyewe kwa muda mrefu sana. Leo katika bajeti imetengewa shilingi milioni 561 kama matumizi ya kawaida. Hii ina maana gani imeshindwa kujiendesha au vipi?

Tunaitaka Serikali itueleze ni lini Serikali itatoa ruzuku kwa wafanyabiashara wa madini wajenge *jewellery and cutting centres* ili madini yetu yauzwe nje *with an added value. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Naibu Waziri wa Fedha, aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa, hairuhusiwi kwa wafanyabiashara ya mafuta na wengine kupanga bei. Lakini hadi leo wanaendelea na bei ya mafuta inapanda sana. Waziri kama *in-charge* wa nishati, tunamwomba atoe tamko la kukomesha mtindo huu, kwani unaumiza Watanzania. Wakulima wa pamba ambao wanatumia matrekta na malori kwa kusomba pamba wanalalamika bei ya mafuta imepanda.

Mheshimiwa Spika, *cartel* ni mbaya na leo asubuhi nimesikia kule Mwanza makampuni yanayonunua pamba yamekaa wamesema bei ya pamba ya s hilingi 300/= ni kubwa mno wanashusha bei mpaka shilingi 250/=, hili ni pigo kwa mkulima. Tunaomba hizi *cartel* za namna hii ziweze kukomeshwa ili mkulima aweze kupata anachostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hii Wizara ya Nishati na Madini na nikiwa mchangiaji wa kwanza, baada ya Wazungumzaji Wakuu. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na watumishi wote, kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yake na kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya hapo na mimi ningependa pia kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wengine wote ambao wamepata matatizo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu katika Wizara hii nitaelezea mambo machache yanayohusu Jimboni kwangu Wilaya ya Chunya na mengine ambayo ni ya jumla.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nataka niongelee suala la mradi wa wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Chunya ambao unaitwa *Ganga Mining Company.* Mradi huu ulianzishwa kama miaka mitatu sasa imepita na mradi huu ulikuwa ni msaada kupitia *World Bank* na uligharimu fedha nyingi tu zaidi ya shilingi milioni 470 na ulianzishwa katika Wilaya ya Chunya kwa lengo la kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Mradi huo ulitazamiwa kwamba, ungetoa huduma kwa hao wachimbaji wadogo wadogo na

baada ya kufanikiwa katika Wilaya ya Chunya basi mradi huo ungeweza kuanzishwa tena katika sehemu nyingine hapa nchini hasa katika Ukanda wa Ziwa ambako pia kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya tangu mradi umeanza ile mashine iliyowekwa pale Kasakarawe katika Kijiji cha Matundasi mpaka leo haijaanza kufanya kazi kikamilifu. Kwa muda mrefu katika kufunga mtambo wa mashine hizo waliwaleta watalaam kutoka Zimbabwe kuja kufunga mtambo huo na walipokuwa wanafunga ule mtambo pale Kasakarawe wakaufunga vibaya, walipoondoka mtambo haukufanya kazi kwa muda mrefu. Hata mwaka 2003 nilimwalika Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuja kutembelea Wilaya ya Chunya na mradi huo na kwa bahati nzuri alikubali na alikuja mwezi Agosti,2003, tulifika huko kwa pamoja kutembelea mradi huo.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri wataalam wa Wizara kabla Mheshimiwa Waziri hajafika, walikwenda kuwaleta wale wataalam kutoka Zimbabwe kuja kuutengeneza ule mtambo. Sasa sina hakika kama walikwenda kutengeneza ule mtambo au walitaka kumwonyesha Mheshimiwa Waziri kwamba, wanaushughulikia ule mtambo. Kwa sababu wakati Mheshimiwa Waziri anakwenda ndipo tulipowakuta wale mafundi wanaendelea na kuufunga funga ule mtambo. Wakati ambapo Mheshimiwa Waziri alikuwa hajafika, wale wataalam walikuwa wameshaondoka na mtambo umeachwa pale porini. Kwa hiyo, mpaka sasa hata baada ya Mheshimiwa Waziri kuondoka ule mtambo utendaji wake wa kazi bado unakwama. Katika sehemu fulani ule mtambo ambapo mawe makubwa yanapotakiwa yasagwe yale ambayo yanapita bila kusagwa yanatakiwa yarudishwe tena yaanze *process* upya ili yaweze kuvunjwa vunjwa ile mashine haifanyi kazi. Kwa hiyo, mtambo mzima kwa kweli haujatoa manufaa kwa wachimbaji wadogo wadogo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa suala langu ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwamba, je, malengo na makusudio ya mradi huu wa *Ganga Mining Company* yamefikiwa au bado hajafikiwa na nini Serikali inafanya ili kuuwezesha mradi huu uweze kufanya kazi zake vizuri na kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kama vile ambavyo ilitarajiwa pale ambapo mradi unaanzishwa. Aidha, pia tunataka kujua kwamba ni vipi mradi huu ungeweza kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwa eneo la uchimbaji wa dhahabu katika Wilaya ya Chunya ni kubwa na mradi umewekwa katika eneo moja ambapo kutoka kwa baadhi ya wachimbaji wadogo wadogo ni zaidi ya kilomita 20, 30 mpaka 40, watafikaje katika eneo la huo mradi ili na wao waweze kufaidika? Ni vyombo vingapi ambavyo vimewekwa kwenye mradi huo vitakavyoweza kukodishwa kwa wachimbaji wadogo wadogo wanaovihitaji na vilevile gharama ya kuvikodi ni kiasi gani. Kwa sababu si vizuri kusema kwamba, mradi utawasaidia wachimbaji wadogo wadogo lakini gharama zake zikawa ni kubwa kiasi kwamba hawawezi kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la umeme katika Wilaya ya Chunya. Nashukuru Mheshimiwa Waziri tulimwambia kwamba, tulikuwa na mpango wa kupeleka umeme Lupatingatinga na Mheshimiwa Waziri alipotutembelea yeye mwenyewe aliona na akatoa ahadi kwamba, mradi ule utatatekelezwa. Kwa bahati nzuri

kweli tunawashukuru Wizara pamoja na *TANESCO,* ule mradi ukawa umeanza mapema mwaka huu. Lakini bahati mbaya sana wanakwenda pole pole mno, yale maendeleo ya mradi wenyewe ni pole pole mno, tungependa waongeze *speed* waende kwa haraka zaidi kuliko wanavyokwenda sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kinachotushangaza ni kwamba, wale wapimaji wamekuja Wilaya ya Chunya kupima, wamekaa muda mfupi halafu wameondoka tena kabla hawajamalizia kazi. Walipokwenda kilomita 13 wakaondoka na mpaka sasa hawajarudi. Hivi nilikuwa naongea na Meneja wa Mkoa wa Mbeya wa *TANESCO* kuona kama wale mafundi wanarudi lini tena kwenye eneo la mradi ili wamalizie sehemu iliyobakia, ilikuwa mwezi huu wa Julai, 2004 wangefika Lupa, mpaka sasa hawajafika mpaka sasa watafika lini? Kwa hiyo, tunataka tujue kwamba, ni lini watafika kwa sababu lengo la kufika Lupa ilikuwa kwamba wakimaliza ule mradi ingeliwawezesha kwenda kuendelea na kutoa umeme Mwambani kwenda Kanga ambapo ni karibu sana. Lakini hadi sasa hawajaanza kufikiria sehemu nyingine kwa sababu ule mradi wa kwanza hawajaukamilisha na kadri wanavyokwenda pole pole ndivyo hata gharama za mradi wenyewe zinavyoongezeka. Kwa hiyo, tungependa na ningeshauri sana Mheshimiwa Waziri atueleze na awahimize hao watu sasa waongeze *speed* au hatua za kutekeleza ule mradi ziongezwe ili mradi uweze kukamilika mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ambalo nataka kulizungumzia linahusu *TANESCO* yenyewe. Katika mazungumzo ya mwaka 2003 mpaka hata mwaka huu wa 2004, Serikali imekuwa ikizungumzia juu ya kuigawa *TANESCO* kwamba, wanataka waivunje *TANESCO* na kuigawa katika sehemu tatu. Yaani sehemu moja ya uzalishaji wa umeme *(Production),* sehemu nyingine ya kusafirisha *(Transmission)* na sehemu ya tatu ni ya kusambaza *(Distribution).* Wanataka kuwe na Makampuni matatu yanayofanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nataka pia watusaidie tatizo hasa ni nini? Ni kushindwa kuiendesha kampuni hiyo kama kampuni moja ama lengo hili ni kusambaza wawekezaji wawe wengi ndani ya Tanzania ama ni kutaka kwamba watu wengi waje wapate kazi hapa Tanzania au ni kupanua ajira? Kwa sababu bado tunataka tuelewe kuna makampuni mengi duniani makubwa sana na yanaendeshwa *as a single unit* yote kwa pamoja yanaendeshwa hapa duniani yapo makampuni makubwa sana. Sasa Tanzania inapokuja kushindwa kuendesha kampuni moja tu ambayo ina-*operate* ndani ya mipaka ya Tanzania na mpaka sasa inatoa huduma kwa watu wasiozidi asilimia 10 ya *population*, bado mnaona ni mzigo kiasi kwamba hamuwezi kuiendesha kama Kampuni moja? Inatutia wasiwasi na uwezo wetu wa kuendesha shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, kama Kampuni moja kama hiyo wanaona kwamba ni mzigo na sielewi na sina hakika sana kama ikigawanywa katika vipande ndiyo itashusha gharama za umeme kwa mtumiaji. Kwa sababu iwapo mzalishaji atamuuzia msafirishaji na msafirishaji atamuuzia msambazaji na msambazaji ndiyo amuuzie mtumiaji, hivi kweli gharama itakuwa ni ndogo kuliko ilivyo hivi sasa, hautakuwa mzigo mkubwa zaidi kwa watumiaji? Kwa sababu ili aweze kuwa-*sustain* hawa watu watatu huyo huyo mlaji

mmoja, mimi nina mashaka kwamba, huenda gharama inaweza ikawa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, labda tungemwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze tatizo hasa ni nini? Ni kushindwa kuendesha, ni uwezo wetu mdogo wa kuendesha ama ni kutaka tu kusambaza hizi shughuli ili watu wengi waweze kupata hizo shughuli na kwa hiyo, labda Watanzania waweze kubeba mzigo huo kuwawezesha watu hao kupata ajira na kupata mapato yao?

Mheshimiwa Spika, la nne, ambalo nataka nizungumze ni la Mradi wa *Mchuchuma Coal Mine*. Ninashukuru na ninafurahi katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, mradi huu sasa unaweza ukaanza hasa kwa vile mwekezaji amesema kwamba, yeye yuko tayari kuzalisha umeme na kutafuta soko yeye mwenyewe na kuuza ule umeme yeye mwenyewe. Hii labda inaondoa kikwazo kilichokuwepo hapo mwanzoni na kwa hiyo, kuruhusu mradi uweze kuanza na umeme uanze kutumika hapa nchini.

Lakini hata kabla mwekezaji hajatoa hii *offer* nyingine ya pili, pale awali waliposema kwamba, watazalisha umeme upatao megawati 400 na gharama yao ingekuwa ndogo kuliko *IPTL* na wengine wanaouza umeme kwa sasa. Ile gharama waliyokuwa wametoa kwamba wangeuza umeme kwa Serikali, wao walisema hiyo ilikuwa ni pendekezo la kuwezesha wao waweze kukaa na Serikali na kuzungumza. Kwa lugha nyingine, walikuwa tayari kulingana na majadiliano ambayo yangefanyika wangeweza kushusha hiyo gharama ili kuwawezesha mradi ule uweze kuanza na kwa hiyo, waweze kuzalisha na kuiuzia Serikali na Serikali iusambaze hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hiyo, kama hatua zimefikiwa hapo, tunachoomba sasa ni Serikali kuimarisha sasa hii *offer* iliyotolewa na wawekezaji na kuzungumza na wao wafikie makubaliano waanze kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Bado tuna mashaka na uzalishaji wa umeme kutokana na maji, kutokana na mvua ambazo zinazidi kupungua mwaka hadi mwaka na zinakuwa hazina uhakika. Mara nyingi katika miaka ya hivi karibuni tumekuwa na matatizo ya mvua. Kwa hiyo, umeme wa *Hydro* hatuna uhakika sana na wenyewe kwamba utaendelea kupatikana kwa hali ilivyo sasa. Kama Mtera mwaka huu imeshindwa kujaa maji, nina hakika inaweza ikawa mfululizo hata miaka miwili bila kupata maji na kwa hiyo likazidi kuwa ni tatizo kwa kutumia umeme wa *Hydro.* Kwa hiyo, imarisheni upatikanaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma ambayo ni mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu Mgodi wa *Kahama Gold Mine Corporation.* Serikali ilikuwa na hisa asilimia tano na mwaka 1999 Serikali ikaamua kuziuza hizo hisa asilimia tano kwa *Kahama Gold Mine Corporation.* Kwanza, nataka nijue kwa sababu Serikali ilisema kwamba, haina hisa kabisa katika mgodi huo. Lakini la pili, tunataka tujue kwa nini Serikali iliamua kutokuwa na hisa kabisa katika hiyo migodi ingawa katika mgodi wa Almasi wa Mwadui tunazo asilimia 25? Kwa nini katika mgodi mkubwa kama wa Kahama tuliamua kutokuwa na hisa

kabisa na wakati ule ule tulipokuwa na hisa asilimia tano nazo tukaamua kuziuza kwa mwekezaji huyo, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili katika kuuza hizo hisa kulikuwa na makubaliano ya nyongeza yaani *addendum* kwenye *agreement* ile ya utafutaji mafuta ambayo ilisema kwamba huyu mwekezaji atamlipa Waziri wa Nishati na Madini dola 100,000 kila mwaka, yeye au Kamishna wa Madini. Lakini hazilipwi kwenye *Treasury.* isipokuwa zinalipwa kwa Waziri. Vile vile inasema kwamba kila mwaka itabidi Waziri aombe hizo fedha ili apewe kiasi kile atakachoomba ili aweze kupewa na kama hajapewa kiasi kile basi anaweza kukipata mwaka unaofuata.

Sasa mimi nilitaka nijue nilitaka tupate *clarification* kama kweli *agreement* ya namna hii ipo na kama ipo hizi fedha mkizipata zinatumika vipi na mmeshazipata ngapi mpaka sasa na kwa nini mkataba unasema mpaka Waziri aziombe na atapewa zile alizoziomba na zile ambazo hakuziomba itabidi asubiri mpaka mwaka unaofuata, kwa nini?

Hili Mheshimiwa Waziri tungependa muyaeleze hayo ili kuondoa wasi wasi unaoweza kuwepo kwamba kuna baadhi ya fedha zinatolewa au kuna mikataba ambayo haieleweki vizuri au maudhui yake siyo kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri alifafanue hilo ili atuondolee wasi wasi wowote kutokana na mikataba ya namna hii katika hilo. Halafu la pili kama hamna Waziri atalieleza zaidi.

Ili kuondoa wasi wasi kwa sababu vitu kama hivi vinazungumzwa na vinapokuwa vinazungumzwa watu wanapovisikia pembeni pembeni wanachukua kwamba ni vitu vya kweli na vitu halali. Ni vizuri tukielewa mahali pa uwazi kama hapa ili kuondoa wasi wasi wowote ambao unaweza ukawepo katika masuala kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho kabisa katika hilo la Kahama huo mgodi umeleta walinzi kutoka nchi za nje kutoka *Nepal* kuja kuwa walinzi katika mgodi huo wa Kahama. Moja ya faida ambazo nilizoziona pale kutoka kwa wawekezaji ni kwamba zinatoa ajira kwa wananchi wetu. Sasa iwapo na walinzi watatoka nje na wapishi watatoka nje na bado wananunua mahitaji yao mbalimbali hata vyakula na kadhalika kutoka nje je bado faida yetu sisi kama Watanzania itakuwa ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi na pili niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa kufiwa na ndugu yetu, mpenzi wetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego. Naomba sisi pamoja na wafiwa Mungu atupe subira na wale wote wengine ambao tumepata misukosuko katika kipindi hiki basi Mwenyezi Mungu atujalie tuondokane na matatizo haya tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na timu yao ya Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa bajeti hii. Naamini Waheshimiwa Wabunge baadaye wataichambua na kuona kama wanaweza kuipitisha.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie tu ufafanuzi kwa baadhi ya mambo. La kwanza ni jedwali Na. 8 ambalo amelinganisha kodi na mrahaba kwa baadhi ya nchi za Amerika Kusini, Asia na Afrika. Sasa kwa mlinganisho huu nafikiri hatusaidii sana katika Bunge kujua ni nchi gani inafaidika na hii. Kwa hiyo ni vizuri akatuambia ni nchi gani inafanya vizuri zaidi na inapata mapato zaidi ili tuweze kuiga kwa sababu ukitoa mchanganuo namna hii tu peke yake hautusaidii kujua ni wapi hasa pana mafao.

Kwa mfano ukichukua Tanzania tunazungumzia kwamba tuna asilimia 5 ya mrahaba kwa almasi na asilimia 30 kwa dhahabu. Tuna *income tax* asilimia 30, tuna *dividend tax* asilimia 10 lakini hatujui tunapata nini katika hizo. Kuwa na figure tu hapa haijasaidia kama tunapata kitu. Kwa hivyo nafikiri ungetusaidia tunapata nini katika huo mchango wa madini.

Mheshimiwa Spika, halafu hili ningeomba vile vile atusaidie katika jedwali la Na. 10 amezungumzia mapato yanayotokana na madini. Jedwali la 10 kuna *diamonds* ukipiga *total* hapa ya *income* kwa muda wa miaka 5 ni dola 127.32 milioni. Sasa labda angetueleza katika hizi zimeisaidiaje Tanzania tumepata nini kwa Watanzania. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, lingetusaidia ni mradi gani uliochangia kiwango kikubwa cha mapato haya ya 127.32 bilioni kwa *total* ya hii miaka 5 uliyoiweka katika jedwali liko hapa. Nafikiri hiyo ingetusaidia sana Wabunge kujua kama kuna mapato yanayopatikana kwa Tanzania. Lakini vile vile ingetusaidia kuna mgao ambao unapatikana katika baadhi ya Makampuni hapa basi tungejua kama tunapata kiasi gani. Hilo ndilo lilikuwa jambo la tatu ningependa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, la nne ni uuzaji wa hisa za Serikali. Kama Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha alivyozungumza sasa hivi juu ya mgodi wa dhahabu vile vile nafikiri kuna *shares* zilizouzwa kwenye mgodi wa almasi. Basi ni vizuri tukajua je kwanza kwa nini Serikali haitangazi, wazi wazi katika kuuza hizi *share* zake zikatangazwa kwa watu wengine wote wakajua kwamba kuna hisa fulani zinauzwa. Badala yake anapewa yule yule ambaye yuko pale kwenye mgodi hata kama mkataba hausemi hivyo. Hiyo nafikiri hakuna uwazi katika hilo.

Lakini lingine kuna sheria nafikiri ya *Procurement Act* inayotutaka kwamba tutangaze kwenye kutumia tenda kwa kile ambacho Serikali inauza. Kwa nini sheria hii imevunjwa haikutekelezwa. Nafikiri hayo ni maelezo Waziri utatusaidia.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa anisaidie Mheshimiwa Waziri ni kwamba kuna wachimbaji wadogo wadogo na wachimbaji wa katikati na mpaka sasa bado hakujakuwa na sera madhubuti juu ya wachimbaji hawa wadogo wadogo na wachimbaji wakubwa na wa katikati. Hakuna mfuko wowote ambao wanaweza kupata mikopo. Je, kama Serikali ina mpango wowote ambao utaelezwa katika Bunge hili juu ya wachimbaji hawa wadogo wadogo na wa kati kuweza kuwasaidia kuanza kupata mikopo na misaada na utaalamu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kwamba hawa wachimbaji wa katikati ambao ndio hasa wengi wao ni Wazalendo ni Watanzania. Kwa mfano pale Chunya nilipokwenda kutembelea nikakuta kuna Kampuni moja inaitwa *Two Drums* ya Mzalendo kabisa na ametumia vifaa kwa juhudi zake mwenyewe na kuchimba mashimo lakini hana msaada wowote wa Serikali na wako wengine wa aina nyingi namna hii. Sasa je Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia hawa wachimbaji wa katikati kwa sababu na hawa ndio watakaoweza hasa kwa kweli kuineemesha Tanzania. Hivi sasa ukiangalia miradi mingi inayochimbwa na wawekezaji wakubwa basi tunakuwa tunapata ajira. Lakini ukiangalia ajira Mheshimiwa Waziri ukichukua wataalamu watatu tu wanaolipwa pale wanaweza kuchukua asilimia zaidi ya 90 ya Watanzania wanaolipwa.

Kwa mfano mtaalamu mmoja analipwa dola 10,000 kwa mwezi wakati Mtanzania analipwa dola 150 na 200 kwa mwezi. Sasa ukilinganisha utaona idadi kubwa ya Watanzania wameajiriwa pale. Lakini kipato chao ni kidogo sana kulinganisha na wale wageni. Katika mikataba yetu mingi utakuta tunazungumzia suala zima la kusomesha kwamba lazima wageni wawaridhishe Watanzania. Lakini inakuwa ni kinyume chake kabisa huwezi kukuta *top management* kuna Mtanzania amekaa pale na hiyo inakwenda kinyume na hata ile mikataba ambayo tunakubaliana. Kwa hiyo tungefafanuliwa idadi kubwa ya watu kuajiriwa lakini kama kipato chao ni kidogo mno na watu wachache wageni lakini kipato chao ni kikubwa hiyo bado haijatusaidia kwa sababu hizo fedha zote hazikai ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nafikiri ni la msingi sana ni kwamba hawa wawekezaji wakubwa wote wanakopa kwenye Mabenki ya nje lakini mikataba yao haiangaliwi na Serikali. Kwa hiyo ukweli hata kujua mikataba yao ya mikopo kule ndani ni siri yao wao. Kwa maana hiyo kama tunawaambia sisi watatulipa *Corporate Tax* au *Income Tax* baada ya kumaliza madeni huwezi kujua ni lini litamalizika maana hiyo ni siri yao. Na wakati mwingine wanakopa kwenye Makampuni yao wenyewe ndani kwa ndani. Kwa hiyo, huwezi kujua hasa kinachoendelea huko ndani. Tunasikitika hata tunapouliza Serikalini unaonekana kama watu hao wanapewa uhuru wa kuamua wenyewe wanavyotaka. Kwa hivyo pamoja na viwango vya kodi tunavyosema vitatozwa ni kama ndoto tu kwa sababu mpaka deni litakapomalizika ndipo huo mradi utaweza kuanza kutozwa kodi.

Sasa kwa misingi hiyo tunafikiri kwamba Serikali kwanza ifanye mambo yafuatayo. La kwanza hawa wawekezaji washauriwe watumie Mabenki ya ndani kukopa. Pia wawe na *account* hapa ndani ya nchi. Nyingi utakuta *account* zao ni zile tu za kuendeshea mambo ya *administration* kidogo kidogo. Lakini yale mapato hasa

hayaingii kwenye *account* zetu. Kwa hivyo, hakuna udhibiti wa haina yoyote. Lakini la tatu tushauri wakope kwenye Mabenki yetu na kama hakuna fedha Benki Kuu ya Tanzania ina uwezo wa kuingilia kati kuweza kuwasaidia hawa watu kupata mikopo kwa kutumia Mabenki yetu na hapo ndipo tutakapoona mzunguko wa fedha ndani ya nchi na sio kama hivi sasa ambavyo fedha zote zinatoka nje ya nchi. Hilo nafikiri tungeweza kulifanya na likatusaidia kukuza mapato kutokana na madini.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo Mheshimiwa Cheyo amelisema na naliunga mkono ni kwamba kuna nchi za *SADC* na nchi za Afrika kwa ujumla ambazo tunayo mazao ya aina moja. Tuna madini ya dhahabu na almasi.

Tunayo *NEPAD* nafikiri tungeitumia *NEPAD* tukashauriana hasa kama tunaweza tukaunda na sisi Umoja wetu wa Kiafrika kwa kutumia msingi huo ili tukadhibiti hawa wawekezaji wakubwa. Tukawadhibiti kwa maana ya kuwa na kauli moja kama wanakwenda Botswana basi kuwe na kauli moja na Tanzania, kama wanakwenda Afrika Kusini kuwe na kauli moja na Tanzania. Hiyo ndiyo kweli Afrika tunaweza kukomboka kutokana na raslimali yetu tuliyonayo vizuri. Vinginevyo bado Makampuni makubwa yataweza kutuchezea.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa utakuta Makampuni makubwa nchi nyingine wanawafukuza sisi bado tunawakumbatia huku. Sasa tungejifunza kwa nini wenzetu wanawafukuza sisi tunawakumbatia. Nafikiri hilo ni suala ambalo tunaweza tukajifunza na tukabadilika hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nashauri sana suala la kuitumia *NEPAD* na suala la kuitumia hizi nchi zetu za Kiafrika ambazo zina raslimali kama zetu tukashikana pamoja tukawa mtazamo mmoja tunaweza kabisa tukapata utajiri wa nchi yetu na tukafaidika katika Bara letu la Afrika. Huo ni ushauri Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri alitazame.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la watumishi. Katika madini kila ukizeeka ndipo unapokuwa na ujuzi zaidi. Madini ni kitu cha ajabu kidogo. Ukiwa na *experience* tu ndogo ndogo hivi kwa kweli huwezi kukomaa. Bahati mbaya mikataba yetu au taratibu zetu za sheria zinasema mtu akifika muda fulani apumzike. Sasa wakati anapumzika ndio *experience* tayari imekuwa amesha-*gain experience.* Kwa mfano leo ukimwita Mheshimiwa Lwakatare aliyekuwa Meneja Mkuu wa *Williamson Diamond* uzoefu alionao ni mkubwa mno. Lakini sasa ndio amepumzika. Mimi nafikiri nalo hili tungeliangalia kwa sababu *experience* ndiyo inaweza kutusaidia sana katika kujenga taasisi hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni yangu hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine nichangie hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa nitoe rambirambi kwa jamii, familia na wananchi wa Mbeya kwa kifo cha Mheshimiwa Ndugu yetu Mwalyego. Niwape pole wale wote waliopata mabaya na niwapongeze waliopata mema.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini mimi nashindwa kuipongeza kwa sababu mbili tu. Moja haijanionyesha tuko *serious* kiasi gani kutatua tatizo la *energy.* Suala la *energy* hapa limeongelewa kama mtu anayejipakapaka mafuta na akamaliza. Tuna tatizo kubwa sana la suala la mafuta hivi sasa na litaendelea. Samaki akimeza ndoano lazima atavuliwa. Na sisi kwa uchumi wetu na Wizara hii ya Nishati na Madini wametufikisha mahali ambapo matatizo katika mafuta tunayo.

Tuliishauri Serikali hapa ndani kwamba *TIPPER Refinery* isifungwe ila itafutiwe kila njia ipatiwe mwekezaji na wakati tunaposubiri mwekezaji Serikali iendelee maana ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na usalama wa nchi yetu. Lakini akaja mjanja kupitia hawa wenzetu wa Nishati na Madini akawadanganya kuwa eti ukiwa na bwawa la kumwagilia ukitaka umwagilie vizuri bomoa lile bwawa liondoke lakini ubaki na mfereji au mto unatiririka ndio utamwagilia vizuri. *This is what we are doing now with* mafuta. Ni upotovu ambao huhitaji mtu mwenye akili kuuelewa.

Hivi leo Zambia wana *refinery,* Kenya wana *refinery* sisi tumebaki tunangoja mafuta ya kwenye bomba, *and we are finished.* Hilo moja. Twende kwenye umeme. Umeme tunaelezwa hapa mambo kama mtu anayehubiri uzima wa milele. Hawa wahubiri wa uzima wa milele *I repeat again they know nothing about it* ila ndivyo wanavyoishi. Umeme tunaoelezwa sasa ni kichekesho sana. Tanzania tuna mabwawa *(ponds), you can call them ponds* kama unaongea bwawa la Kaborabasa au *Aswam Dam, Ghana* au mabwawa ya Brazil nchi ambazo ni ma-*hydro giants.* Mabwawa yetu ni *ponds.*

Miaka ya 1978 tulishauriwa tujenge bwawa ambalo ni *sustainable* kwa ajili ya umeme *Stigler's Gorge* tulikataa, hali ya fedha hairuhusu. Ukikataa kuwekeza wewe utakuwa maskini milele. Huwezi ukachuma usichowekeza. Leo tumefikishwa eti tunajivuna tuna umeme wa *Songas.* Umeme tutakaoupata kutokana na gesi mimi sijui *sustainability* yake na mfano wake ni nchi ipi duniani. Ninavyojua mimi umeme wa gesi maana gesi tunayo ungeweza kuwa wa maana kwa ajili ya ku-*sustain peak periods* mwisho. Ni lazima tuelewe hizi *gas turbines* haziko *manufactured* kufanya kazi na masaa 24. Ukiitembeza masaa 24 *maintenance cost* ina *shoot up.*

Lakini la pili, *life span* yake inakufa kwa *ratio* ya 6. kama ilikuwa liwe na uhai miaka 18 basi ukitembeza masaa 24 litakuwa na uhai miaka 3 badala ya 18. Tutaambiwa kila uongo hapa. Lakini nini wanachoelekea hao wanataka kutuuza. Wametuuza kwenye mafuta sasa wanataka kutuuza kwenye umeme.

Katika miaka 5 ijayo tutahitaji umeme mwingi zaidi ya huu. Lakini nini wamefanya hawataki Mchuchuma ambayo *is the only sustainable way* kwa nchi hii wamebaki kugusagusa mara gesi mara vibwawa maana sio mabwawa, vibwawa vya maji,

mara sijui mafuta ambayo wala hatunayo hayo mafuta ili waje watuunge kwenye *Southern grid* tuwe soko la *Southern grids.*

Mimi kama mwanataaluma nawaachieni sina tatizo kama nchi hii inaingia kwenye *Southern grid.* Bora mradi iingie ikiwa na umeme wa kutosha siku nyingine tukiwa na matatizo watuuzie na siku nyingine tuwauzie wao. Lakini Wizara ya Nishati na Madini inaendeshwa na watu utadhani ni mamluki kumbe ni Watanzania. Mimi nashindwa hata kuwaelewa. *(Makofi)*

Ninajua ni wasomi najua kila ninaloelewa wanalielewa, najua yako mengine wanaelewa kuliko mimi, sasa ni nguvu ipi inayowasukuma waihujumu Tanzania. Mimi najua *arrogance* ya Wizara hii niwaambie tu inawezekana wana-*rub shoulders* na *press and bosses* tutawaadhibu baadaye. *You will answer there is no way* nchi hii itaendelea kuteseka sababu mtu mmoja analeta maamuzi yanayoua wananchi.

Mheshimiwa Spika, uongozi tunapokezana, leo mimi kesho wewe, kesho kutwa yeye, mtondogoo wao. *I better warn you today comrades, you will not afford.* Hatutavumilia matendo batili ya makusudi kwa ajili ya starehe ya watu wachache. *(Makofi)*

Siku moja nilimwuliza Yona hivi ofisini kwenu *Minister* ni nani ni wale wengine nisiongea nao au ni wewe tunayeongea wote. Alisema kwani wewe hujui nani aliyeteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nikamwambia uliteuliwa wewe. *But you don't seem to be. Why do you understand me when we talk here together and when you go to your office you are powerless, what is wrong? (Makofi)*

Waziri tunamshauri tunatarajia aendeleze na kusimamia tunayoshauri. Leo wameanza kusema Mchuchuma ikizalisha megawatts 400 ni nyingi mno. Lakini utashangaa hawa watu. Ndio nasema utadhani ni mamluki. Tanzania leo wanaotumia umeme ni *less than 10 percent.* Ni nyingi mno ukilinganisha matumizi yako wewe au ukilinganisha na matumizi ya sisi Watanzania wote. *Which demand level* unatumia ya nyumbani kwako au ya nchi.

Leo Wananchi, Waheshimiwa Wabunge ukienda njia ya Tabora ukiona miti inavyokatwa *like nobody's business.* Huwezi kuamini ni nchi yenye Serikali tena Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Huwezi kuamini. Unaweza ukadhani ni Serikali imetoweka haipo sasa kila mtu anafanya anavyopenda yeye. Lakini sababu ni nini? Wizara ya Nishati na Madini ndiyo inayosababisha hali nzima ya uchumi na maendeleo ya nchi hii tuwe tunagongana. Wizara nyingine inatumia fedha kutunza mazingira, Wizara nyingine inatumia fedha kuharibu mazingira tutafika wapi? *(Makofi)*

Hakuna mahali popote katika kitabu hiki unaweza nikasoma au yeye Waziri akitaka baadaye anisomee kuwa mahali tulipoonyesha mkazo na nia yetu ya kuendeleza nchi hii katika *energy* ni sehemu ipi anaweza akaisoma tena pale. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wakasikia ili wajue Wizara yake kuna kitu cha maana inafanya

ila mimi bahati mbaya sikuona. Na nina uhakika kitakuwa hakimo katika kitabu hiki kitakuwa kipo mahali pengine.

Kwa hiyo, mimi nasema hali tuliyonayo sasa kama tunataka maendeleo ya kiuchumi na kijamii ni lazima tufanye mageuzi. Katika mafuta ni lazima kila njia itafutwe *refinery* ile ifufuliwe. Katika nishati ni lazima tuingie kwenye umeme wa Makaa ya Mawe. Hiyo gesi mliyoleta inatuua zaidi. Miaka ya 1970 na kitu pale Ubungo lililetwa lile li-*generator* kubwa *gas turbine* walishindwa hata kuweza kulitumia *it was economically not sustainable.* Nchi hii ni *a damping pit.* Kila anayefikiwa na mawazo akishawabana wenzetu wawili watatu anakuja anatupa takataka zake hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Waziri wa Nishati na Madini atakapotoa majumuisho atuambie vitu gani anadhani ndivyo yeye ameviweka visaidie nchi hii katika nishati. Akituambia masuala sijui ya umeme mwingi mno, sijui *IPTL* na nini mimi sitaki kuongelea *IPTL* mlikwisha ishughulikia mnajua mlichofanya. *Songas* mnashughulikia sasa.

Mheshimiwa Spika, watu tumekuwa limbukeni humu ndani tunadanganywa kama watoto. Sasa matatizo *load shedding* ni hadithi, hadithi ya nini sababu ya *Songas.*

Mheshimiwa Spika, nani anawadanganya. *Gas is not a sustainable power source for a country like Tanzania.* Hata wao waliofanya ile kazi wanajua sio kwamba hawajui. Lakini cha mlevi huliwa na mgema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaiomba Serikali suala la *energy* waache kucheza na Mchuchuma ndiyo *possible practicable source* ambayo ipo. Tunayo na itatuletea uchumi mkubwa kwa kuruhusu na maeneo mengine ya uchumi katika eneo lile yaweze ku-*take off.*

Mheshimiwa Spika, kwa Wizara hii mimi ninavyojua sasa hivi wanataka kuhangaika na Ruhuji, Rumakari hayo yote ni kutufunika tu *at the end of the day* watuunge tuwe soko la *Southern grid* ndiyo nia yao. *That's where we are leading to.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono wapewe bajeti lakini siwapongezi kwa kazi wanayofanya wanatuhumiza vibaya sana, *It is a shame.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii nikupongeze wewe kwa kuniteua maana nilikuwa na wasi wasi kwa sababu mwaka jana nilikosa hii nafasi watu wa Ludewa hawakunisikia kwamba nazungumzia nini kuhusu Wizara hii. Kwa hiyo nakupongeza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Awali ya yote naomba vile vile nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri ambayo ameileta katika Bunge hili lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, aidha leo kwa mara ya kwanza nitatoa kidogo *light* na nitatoa *light* kidogo kwa sababu katika hotuba yake amezungumzia mradi ule wa

Mchuchuma kwamba ziko hatua zimechukuliwa ambazo kwa kweli sio kwa manufaa ya Wilaya ya Ludewa lakini kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa sana kwa hiyo nawapongeza katika hilo angalau kidogo.

Lakini pamoja na pongezi hizi lazima niwapongeze sana Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu wao ndiyo wanasimamia ule mradi wa *NDC* na ndio wanaofanya kazi kubwa sana ya kutafuta hawa wawekezaji. Kwa hiyo nao nawapongeza. *(Makofi)*

Lakini baada ya hapo nafikiri ndugu zangu kule Ludewa wataelewa kwamba kwa kweli Serikali sasa ipo *serious.* Ninawaomba tu kwamba *follow up* ya mambo haya kwa sababu mambo mengi sana ya mradi huu yalikwama kwa sababu ya maamuzi.

Maamuzi ya mradi huu yalikuwa yanachukua muda mrefu sana na ndiyo maana pengine Waheshimiwa Wabunge hapa wanazungumzia habari hii kwa sababu utakuta *correspondence* kati ya uwekezaji zinachukua mwaka mzima, miezi sita sijui kwa nini?

Siku hizi kuna makompyuta na kadhalika mtu unachukua kufanya maamuzi tu. Nakumbuka tulikaa vikao vingi sana hata kile kikao cha *Mtwara Corridor* tulizungumzia mradi huu wa Mchuchuma ilionekana wazi kabisa mradi huu Wizara ya Nishati na Madini haiupendi. Maana walileta pale *paper* moja ya kutisha kweli kweli tukasema loo!! sasa huu mradi umekwisha. Lakini taratibu nadhani sasa hivi wana-*take off* kwa hiyo tunawatakia kila la kheri muufuatilie.

Kwa kweli vile vile tuwapongeze wawekezaji wenyewe kwa sababu ya kuwa kidogo wavumilifu wangekuwa wengine wangekwisha *withdraw* hii kitu wangekata tamaa. Kwa hiyo, kama wangekuwepo hapa tunawapongeza kwa kazi hii nzuri. Lakini baada ya hiyo kama ulivyosema ilikuwa ninatoa *light touch* tu nizungumzie kuhusu utafutaji wa madini katika nchi yetu.

Nimesoma katika ukurasa, nadhani ule wa *section 63* inayozungumzia Wizara kuandaa, kutayarisha takwimu za kitaalam kuhusu miradi ambayo baadaye inauzwa kwa wawekezaji. Sasa maandalizi ya namna hii pengine ingekuwa vizuri sana kama yangeingiza miradi kama vile ile ya Liganga kwa sababu mradi wa Liganga tatizo lake kubwa ni kwamba hakuna maandalizi ya data za kutosha kwa uwekezaji na pengine inahitajika ifanyiwe *final study* ili iweze kujulikana ni kiwango gani cha chuma kinaweza kupatikana. Katika kifungu hiki mmesema mtakuwa mnaandaa, mnatayarisha na kutafuta *data* za kutosha ili wawekezaji waweze kuridhika. Nadhani mradi huu ni mradi mzuri ambao ungeweza kusaidia nchi hii hasa ukioanisha na mpango wa Serikali wa *Mtwara Corridor.*

Mheshimiwa Spika, sidhani kama kuna kuna *Mtwara Corridor* bila mradi ule wa Liganga. Nafikiri mradi wa Liganga kwa sababu una *economic advantages* nyingi, una *backward and forward linkages* za *economy,* zinaweza kusaidia sana uchumi wetu. Tunatengeneza barabara kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay,* zibebe nini? Tutabeba

mizigo ya Malawi mpaka lini? Lakini tunaweza kubeba mizigo inayotokana na chuma cha Liganga ambacho kina *uranium* mle ndani na kadhalika. Kwa hiyo, kazi kubwa ya wataalam wetu siyo kutazama tu manufaa ya sasa, ni kutazama manufaa ya baadaye, yaani *economy* ya Mikoa ile ya Kusini inaweza kuongezeka kiasi gani. Nadhani hilo ndiyo kubwa. Lakini tukitazama kamradi kamoja kamoja hatuwezi kufaidika. Kwa hiyo, nafikiri kutakuwa na maandalizi haya ya mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Viwanda na Biashara alileta pale Wachina ambao kwa kweli walikuwa *impressed* sana na mradi ule chuma wa Liganga. Lakini vile vile, ningeomba Mheshimiwa Waziri pamoja na ofisi yako, pamoja na kuzungumza sana katika hii na kwa kweli katika Mabunge mawili yaliyopita ilikuwa ni *National concern* ya miradi hii. Lakini *nobody from your office went.* Naibu Waziri naona kidogo anataka kupanga safari sijui, karibu sana kule Ludewa. Mheshimiwa Yona ulifika mwaka mmoja nakumbuka, lakini wataalam wenyewe ambao wangetakiwa wafanye kazi ya ofisi hawajagusa kule maana tuna vitabu, hakuna. Aliyekuja pale ni Mheshimiwa Pawa kutoka Morogoro. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, tunawaomba mje, maana mnasikia tu. Wengine wanasikia habari ya chuma cha Liganga hawaelewi. Ni *outcrop* ya chuma kutoka chini iko mbinguni. Ndiyo maana tulimwomba hata Waziri wa Maliasili na Utalii alete watalii kuona, haijatokea katika dunia. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ilete ionyeshe basi *concern* angalau ya kuona tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile vile, kwa sababu nilisema leo ni *light touch,* nizungumzie kidogo kuhusu mambo ya umeme kupeleka Makao Makuu ya Wilaya. Kwa kweli hili jambo kwa sisi wa Wilaya ya Ludewa linatutisha sana katika mipango ya nchi hii. Wilaya ya Ludewa imeanzishwa mwaka 1975, lakini katika *program* ambazo tunaziona hapa zinazozungumziwa ni Wilaya ambazo zimeanza juzi miaka ya 2000, maana yake nini?

Katika Mkoa wa Iringa, Wilaya peke yake ambayo haijapata umeme ni Wilaya ya Ludewa, kosa lake ni nini? Kosa la Ludewa ni nini tunataka tuambiwe, kwa sababu tunaweza kupata umeme kutoka Makete. Sisi ni neighbours wa Makete, ni kwa nini tusipate kutoka Makete? Lakini hakuna hata mpango! Tunazungumzia 2005 hatupo, sasa tuko wapi? Labda Waziri angetusaidia, hivi hii miradi mnatekeleza mtu akisema sana, akiwa mkali Bungeni au vipi! Kwa sababu hatuoni, hebu tuambieni basi, Ludewa tuko wapi? Tuko 2020 au tuko wapi sisi! Tuambieni ili telewe kabisa kwamba tuko wapi. *(Kicheko)*

Kwa kweli inatisha, Wilaya kubwa ina uchumi mzito na madini haya yote tunayozungumzia. Siku zote tulikuwa tunasema labda tungoje hii miradi ya Mchuchuma, sasa miradi ya Mchuchuma yenyewe ndiyo kama hivyo. Tupeni haki yetu, hii ni haki yetu ya nchi hii, ni haki yetu kabisa. Toka Wabunge wote waliotangulia wamezungumzia jambo hili, nafikiri kipindi hiki ni kipindi kizuri kwa Serikali kutimiza ahadi zake kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumzia habari ya umeme kule Ludewa kwamba labda kunatakiwa hela nyingi sana kwa ajili ya gridi ya Taifa, sisi watu wa Ludewa tukasema basi tupunguze makali ya Wilaya yetu tuombe misaada pengine. Akaja mfadhili mmoja akatupatia jenereta kubwa tu zito. Mimi nikaongoza ujumbe wa Wilaya ya Ludewa pamoja na Mkuu wangu wa Wilaya, Mwenyekiti, Mkurugenzi nikaja Makao Makuu (Mheshimiwa Waziri unakumbuka) nikasema: "Mzee tumepewa jenereta kubwa hili linatutosheleza katika Wilaya Ludewa kwa *cooperation* yetu hii itatufaa. Sasa tunachokosa sisi ni *network.* Mtandao ule gharama zake ni kidogo." *Survey* tumefanya na nini, yaani hata kajibu ka kujibu tu kwamba: "Mheshimiwa Mbunge, juhudi zako hizi zimefikia hapa, hakuna!" Sasa maana yake nini? Watu wa Ludewa wanaona kwamba wamedharauliwa kwa kweli na Mbunge wao mimi wananiamini na wanataka wanirudishe tena mwaka ujao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nafikiri ni vizuri angalau tu tungejibiwa kwamba sasa hivi hatuna pesa. Mimi ningewaambia watu kwamba: "Jamani, Wizara inasema kwamba mwakani tutapata hii kitu."

Mheshimiwa Spika, tulifanya *survey* ya mradi wa Mto Mhangaja ambao una maporomoko pale, lakini bado hatujafanyiwa haki. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji watutendee haki sisi Wananchi wa Ludewa. Sasa Kusini wanatisha, kwa sababu watu wote wanazungumzia, vijana wanaokwenda huko wanasema "Ludewa hakuna umeme katika Mkoa mzima wa Iringa." Sasa aibu gani hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sina mengine zaidi, nilitaka Wananchi wa Ludewa wasikie kwamba ninaieleza Serikali ifanye kama inavyotakiwa, nchi hii ni yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia machache kuhusu Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Lakini kabla ya kuchangia, naomba nichukue nafasi ya kwanza kabisa kumpongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri na pia niwapongeze watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo inafanyika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kutoa pongezi za pekee kwa Naibu Waziri ambaye alitumia nafasi yake kufanya ziara katika Wilaya ya Kondoa na kukutana na Wananchi na kuhamasisha kuhusu matumizi ya umeme katika Jimbo langu. Kwa hiyo, napenda nimshukuru, ninampongeza kwa kuja kututembelea na ninamkaribisha na Waziri mwenyewe siku moja atembelee Wilaya yetu ili kuweza kuhamasisha Wananchi katika shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nichangie maeneo machache. Nianze kwa kupongeza sana Wizara ya Nishati na Madini kwa usimamizi mzuri katika utekelezaji wa mradi mmoja ambao ulikuwa unajulikana kama *Electricity IV,* Awamu ya Kwanza. Mradi huu ulisimamiwa vizuri sana na kwa taarifa nilizonazo ni

kwamba, mradi huu ulitekelezwa kwa asilimia 100. Katika Wilaya ya Kondoa nasi tulifaidika na mradi huu na kazi ambazo zilifanyika katika Wilaya ya Kondoa ni pamoja na Ujenzi wa Kituo Kidogo cha Kupoozea Umeme katika Mji wa Kondoa. Kupitia mradi huu, Umeme wa Gridi ya Taifa uliunganishwa katika Mji wa Kondoa na pia ulipelekwa kutoka Mji wa Kondoa hadi Kibaya, Kiteto.

Nashukuru kwa kazi nzuri ambayo ilifanyika na kwa kweli katika utekelezaji wa mradi huu sehemu kubwa ya njia kutoka Kondoa hadi Kibaya ilikuwa inapita katika Jimbo langu la Kondoa Kusini. Napenda pia niishukuru Wizara kwa uamuzi wake wa busara wa kuweza kuwapatia Wananchi umeme katika njia yote ambako umeme ulipita kutoka Kondoa hadi Kibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Vijiji ambavyo vilipatiwa umeme vikiwa ni pamoja na Mondo, Kelema Maziwani, Goima, Songolo, Chandama, Mrijo Juu, Mrijo Chini na Olboloti. Katika mradi huo wa Awamu ya Kwanza ya *Electricity IV,* pia Shule ya Sekondari ya Aya ilipatiwa umeme. Wananchi wanatoa shukrani za dhati kabisa kwa Serikali kwa ujumla na kwa Wizara kwa kuwapatia umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunafarijika kwamba kuna Awamu ya Pili ya Mradi wa Umeme ambao unajulikana kama *Electricity IV.* Nafarijika pia kusoma katika makabrasha ya Wizara kwamba Kondoa tutafaidika na mradi huu. Wakati Naibu Waziri alipofika na kutembelea Wilaya ya Kondoa alivitembelea Vijiji viwili katika Jimbo langu, Kijiji cha Soya na Hamai na aliwaahidi kabisa kwamba katika awamu hii Vijiji hivi vitapatiwa umeme. Lakini nasikitika kusema kwamba, tangu alipoondoka mwaka jana mpaka sasa utekelezaji haujaonekana. Utekelezaji uliofanyika mpaka sasa ni kufanya *survey* ya njia ya kupeleka umeme katika Vijiji hivyo, lakini baada ya kufanya survey mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Napenda nimkumbushe Naibu Waziri na Wizara kwa ujumla kwamba, aliahidi kuwa umeme utapatikana katika Vijiji hivyo katika mwaka huu wa 2004. Bila shaka kuna maandalizi yanafanyika, naomba basi kama alivyoahidi Wananchi wapatiwe umeme katika Vijiji hivyo viwili vya Hamai na Soya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, nina maombi mengine matatu kuhusu usambazaji wa umeme katika Jimbo la Kondoa Kusini katika hii Awamu ya Mradi wa *Electricity IV.*

Moja ni kwamba, wakati tunapeleka umeme katika Kijiji cha Soya, kuna Vijiji vya jirani sana pale hata kilometa moja au mbili haifiki, naomba na hivi Vijiji vifikiriwe kupatiwa umeme kwa sababu si busara kufikisha katika Kijiji cha Soya peke yake wakati kuna Vijiji vya jirani sana ambavyo havina umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba katika awamu hii basi Vijiji vya Mwailanje na Mwaikisabe viongezwe ili kuweza kupatiwa huduma hii muhimu. *(Makofi)*

Pia, wakati wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Hamai, naomba na Vijiji vifuatavyo vifikiriwe kupatiwa umeme navyo ni Churuku, Jinjo, Kinkima, Jangalo, Itolwa na Mlongia. Kama nilivyosema kwa Kijiji cha Soya, Vijiji hivi navyo viko karibu sana na Kijiji hiki cha Hamai ambako huduma ya umeme itafikishwa katika mradi huo. Kwa hiyo, naomba Vijiji hivi nilivyovitaja navyo vifikiriwe kupatiwa umeme. Itakuwa si busara kupeleka umeme Hamai peke yake wakati Vijiji vya jirani havina umeme kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali wakati wa utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya *Electricity IV* nimesema kwamba, sehemu kubwa ya njia imepita katika Jimbo la Kondoa Kusini na pamoja na shukrani zangu, lakini Vijiji vingi sana viliachwa katika njia hiyo.

Baadhi ya Vijiji viko katika njia hiyo hiyo ya umeme, lakini havikupatiwa umeme na tuliahidiwa kwamba katika hii Awamu ya Pili ndipo Vijiji hivi vitapatiwa umeme.

Sasa napenda nikumbushie kwamba, basi kwa sababu Awamu ya Pili ndiyo imeanza, Vijiji hivi vya jirani ambavyo ndiyo njia ya umeme kutoka Kondoa kwenda Kibaya imepita, basi vipatiwe umeme. Labda nivitaje na hivi Vijiji, ni vingi kidogo.

Hivi ni pamoja na Waida, Pongai, Dalai, Sori, Cheku, Kelema Balai, Tandala, Jenjeluse, Mirambo, Makamaka, Igunga, Madaha, Mapango, Isusumya, Songambele, Nkulari na Magasa. Ni vingi, lakini viko karibu karibu tu. Kwa hiyo, sidhani kama gharama itakuwa kubwa sana. Naomba Vijiji hivi vipatiwe umeme katika Awamu hii ya Pili ya Utekelezaji wa Mradi wa *Electricity IV. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia juu ya Mradi wa *Electricity IV* Awamu ya Pili, naomba sasa nitumie muda mfupi kuzungumzia juu ya nishati mbadala. Nchi yetu ya Tanzania ni kubwa sana, tukiendelea kutegemea mradi huu wa Gridi ya Taifa kuvipatia Vijiji vyetu umeme hatutafika. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie na nishati mbadala ambayo inaweza kupatikana na ambayo inaweza kusambazwa katika Vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ama hotuba za Waziri wa Nishati na Madini huko nyuma aliwahi kuahidi kwamba ataangalia vyanzo vingine vya umeme licha ya chanzo hiki kikuu ambacho kinatokana na umeme wa maji tuweze kuwapatia Wananchi wetu umeme ambao ni wa mbadala. Vyanzo ambavyo vilikuwa vimependekezwa kwamba vitafanyiwa kazi ni pamoja na siku hizi wanaita umeme nuru ama umeme unaotokana na jua.

Pia, tuliahidiwa kwamba umeme unaotokana na upepo nao unaweza kusambazwa katika maeneo ya Vijiji ambako Gridi ya Taifa si rahisi kupita hivi karibuni. Pia, chanzo cha *biogas* ama umeme unaotokana na vinyesi vya wanyama inaweza kutumika katika kusambaza umeme katika Vijiji ambavyo viko mbali na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, mwaka 1999/2000 katika hotuba yake aliwahi kusema yafuatayo, na naomba ninukuu kwa ruksa yako: "Katika kipindi cha mwaka 1999/2000 Serikali itafanya mazungumzo na Kampuni ya Umeme ya Afrika ya Kusini *(ESKOM)* juu ya kuendeleza teknolojia ya kutumia mionzi ya jua vijijini." Hii ilitolewa katika bajeti ya mwaka 1999/2000, lakini mpaka leo sijaona utekelezaji wake.

Naomba niulizie ahadi hii imefikia wapi katika utekelezaji? Tunaomba basi kama kulikuwa na ahadi ya namna hii, Serikali iangalie hivi vyanzo vya nishati upepo, jua na hii ya *biogas* ili maeneo yale ambayo hayapitiwi na Gridi ya Taifa basi navyo viweze kunufaika kwa sababu kama tusipofanya hivi hayo maeneo yatabaki nyuma sana. Yale maeneo ambayo yamepitiwa na Gridi ya Taifa katika Vijiji vyetu wananufaika kupata umeme, lakini yale ambayo hayapitiwi hawataweza kupata umeme kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, naomba basi mradi uanzishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafarijika kuona pia kwamba katika Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini ametenga pesa Sh.632,960,200/= kwa ajili ya kazi hiyo. Lakini kitu kinachosikitisha kama ilivyokuwa imetaarifiwa katika Taarifa ya Kamati iliyopitia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba, hizi zote ni pesa za nje, Serikali kwa maana ya kwamba sisi hatujatenga pesa za ndani. Maana yake ni kwamba, hatuthamini basi kuwapelekea Wananchi umeme hasa Wananchi wa Vijijini. Tunathamini zaidi kupeleka umeme Mijini, lakini tunawasahau wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na pesa hizi milioni mia sita na kitu ambazo zimetengwa kutokana na vyanzo vya nje, basi pesa hii itumike kuweza kuwapatia umeme. Inaonekana kwamba kazi ambayo imekusudiwa kufanywa hapa ni kufanya utafiti. Binafsi sielewi tunafanya utafiti wa nini, maana umeme wa jua tunafahamu ni suala la kutega vifaa ili tuweze kupata umeme na kusambaza.

Sasa unafanya utafiti upi tena! Inawezekana unaweza kufanya utafiti kuhusu upepo, kwamba sehemu gani hasa kuna upepo mwingi wa kuweza kuendesha mitambo inayoweza kuendeshwa na upepo, lakini sioni sababu ya kufanya utafiti wa umeme wa jua, ama sioni sababu ya kufanya utafiti wa nishati ya biogas kwa sababu maeneo ya wafugaji tunayafahamu, ni suala la kwenda kuhamasisha, ni suala la kupeleka teknolojia katika maeneo hayo ili waweze kupatiwa umeme huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuzungumza zaidi ya hapo isipokuwa natoa ushauri tu kwamba Serikali ifanye haraka kusambaza umeme vijijini kwa lengo la kuwapatia maendeleo Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii na ninaunga mkono hotuba ya Waziri. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na

Madini. Kwanza kabisa, nimeshawahi kuzungumza hapa na nimeshawahi kutoa rambirambi zangu kwa wote, nafikiri nijielekeze tu katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki nafikiri naweza nikatoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali hasa baada ya kuona ukurasa wa 44 ambao unazungumzia fidia kwa Wananchi wa Geita. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa ambalo tulikuwa tunalizungumza hapa. Nafikiri Serikali imeweza kusikia na kuelewa tatizo tulilokuwa nalo katika Wilaya ya Geita na mpaka sasa hivi ninavyozungumza Wananchi wameshalipwa fidia yao. Tunaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya kuweza kuondoa kero na lawama kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pili, napenda nimshukuru Waziri Mkuu, alikuja Geita akatoa hotuba nzuri sana ambayo inawatia moyo Wananchi wa Geita, walishukuru na napenda kabisa nitoe shukrani zangu kwa niaba ya Wilaya ya Geita ambayo ina Majimbo matatu, Jimbo la Busanda, Jimbo la Nyang'wale na Jimbo la Geita kwamba wanashukuru kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali kuweza kuwaondolea kero hiyo ambayo ilikuwa imewasumbua kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna tatizo moja, ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameumba mambo mawili mawili. Kuna kizuri na kibaya, kuna kitamu na kichungu. Kwa hiyo, kama kuna zuri basi ujue pia kuna baya. Napenda kusema tu kwamba, pamoja na yote mazuri yaliyozungumzwa, kuna sehemu moja ambayo mpaka sasa hivi haijatekelezwa.

Alisema kwamba Wananchi wote watalipwa fidia yao na wale waliohusika basi watashughulikiwa ipasavyo, lakini mpaka sasa hivi wale waliohusika katika kuwaondolea haki yao wale Wananchi bado wamo mitaani na hatuoni juhudi zozote za Serikali zinazofanywa ili kuweza kuwaweka katika hali ambayo na wenyewe wajue kwamba walichokitenda siyo kizuri.

Kwa hiyo, hilo ninataka kuelewa kwamba, kama hawajafuata amri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu watafuata amri ya nani? Naomba sana hilo litekelezwe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ninataka kuzungumzia ni kwamba, mara nyingi Serikali inatuambia hasa tunapowaomba shughuli za maendeleo katika maeneo yetu, sisi ambao tunataka katika sehemu za machimbo, wanasema kwamba tuzungumze na wawekezaji.

Sasa sisi huwa tunajiuliza, hawa wawekezaji wameletwa na Serikali na Serikali ndiyo inayojua mipango yote na ndiyo inayochukua kila kitu pale, sisi hatuna lolote tunalolichukua pale ila tunaambiwa tu kwamba tukazungumze nao. Kwa kweli mimi hicho nakiona kama ni kitendawili. Serikali ndiyo yenye wajibu wa kuwaambia hawa wawekezaji kama ni kitu gani walete katika maeneo yale. Unaponiambia mimi niwaombe wawekezaji walete maji pale katika Mji wa Geita, basi utakuwa kama umenionea kwa sababu ninyi Serikali ndiyo mliokaa pamoja mkajua mikataba na

mnaijua na masharti gani yapo. Sasa mimi unaponipeleka pale ni kama unanionea. Naomba kabisa kwamba Serikali ilione hili kwamba kama ni kuwaambia wawekezaji kuleta huduma katika maeneo yale, basi ijaribu kwa nguvu zake zote. *(Makofi)*

Lakini katika upande wetu Wananchi wa Geita, tungependa tuifahamishe Serikali kwamba kumbe tatizo lililopo katika hawa wawekezaji siyo uwekezaji, bali tatizo liko katika upande wa Serikali kwani Serikali ndiyo iliyoingia mkataba na hawa wawekezaji.

Tumejaribu kuliangalia na kuona kwamba ni sawa sawa na mfano mmoja ambao mara nyingi huwa nautoa. Unakuwa na binti yako mzuri, unapokuwa naye unaona kwamba huyu ndiyo binti yangu, lakini anakaa muda mrefu bila kuolewa.

Ukikaa naye kwa muda mrefu basi unaona kwamba aah, ngoja basi na yeye aolewe tu, akipatikana bwana yoyote basi unamsukuma tu, anaondoka. Sasa akishaondoka na akikaa kule kwa muda wa miaka miwili, mitatu akazaa watoto wazuri ukaona aah kumbe mtoto huyu ni mali kabisa unasema aah, basi ongeza mahari. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunakuwa mfano kama huo. Serikali imeamua kutoa maeneo bure ya machimbo ya dhahabu au katika machimbo yote. Imekaa imeona wawekezaji ndiyo wanazalisha kwa wingi zaidi sasa hivi inasema ibadilishe mikataba yao na inaunda Kamati. Sasa mimi siwaelewi, kwa hili siwaelewi kabisa. Kwa hiyo, naomba Serikali wakati inapoingia katika mikataba basi iangalie masuala ya undani zaidi ya leo na kesho, siyo kwamba mtu aangalie leo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyimbo hapo amesema, amesema kwamba watu tutakuja kuhukumiwa. Ni kwa sababu watu wengi ambao mnaingia mikataba au ambao wanaingia mikataba hapa wanajali maslahi yao binafsi, hakuna anayejali maslahi ya Watanzania kwa ujumla!

Hii ndiyo kama mfano nilioutoa wa kutoa binti yako bila hata kutolewa mahari unamtoa bure na unamwongezea mwoaji mahari tena ili binti yako aondoke na baada ya kufika kule unamwona kwamba ni wa maana. Hivyo, ninaiomba Serikali iangalie sana katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo nazungumzia katika Wilaya yangu ya Geita ni kuwa, niliuliza swali hapa katika kipindi kilichopita kwamba hebu nielezeni mipaka ya Mgodi wa Geita iko wapi na mkaniambia kwamba kuna maeneo ambayo yamewekwa mawe. Maeneo yale yamewekwa mawe baada ya kuuliza hilo swali mwezi wa tano. Sasa, hebu niambieni, wakati ule wa nyuma Wananchi walikuwa wanajuaje mipaka yao? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuweka hayo mawe basi kumeonekana kuna migogoro mpaka sasa hivi kwa sababu Wananchi walikuwa hawajui kama kuna mpaka pale na wengi walikuwa wanaishi pale.

Kwa mfano, Wananchi wa sehemu za Mine Mpya; Wilayani Geita, sehemu za Nyamalembo, Nyakabale na *Copcot* wote wale walikuwa hawajui mipaka yao iko wapi, lakini leo hii mnatuambia kwamba mipaka imewekewa mawe.

Hayo mawe mmeweka juzi. Je, mpaka halali ulikuwa sehemu gani? Hilo ndiyo nataka kuuliza tu. Kama Mji wa Geita wote uko katika leseni ya wawekezaji basi mtuambie na mtufidie sisi tuondoke, mtujengee Mji mwingine mpya. Lakini kuwa mnatuambia tu kwamba kuna mawe ambayo yamewekwa na mmeweka juzi, mimi hilo silielewi!

Ninaiomba kabisa Wizara kama kuna uwezekano basi yale mawe yasogezwe kwa sababu mmewakuta Wananchi pale sasa hivi. Kama hakuna uwezekano muwafidie hao Wananchi waweze kuondoka ili waishi kwa amani na usalama katika nchi yao. *(Makofi)*

Hilo nilikuwa naliomba kabisa liweze kueleweka na ninajua kabisa kwamba maeneo kama hayo ya sehemu ya migodi ni magumu na itahitaji pesa nyingi. Mimi siwashiki wawekezaji, naiambia Serikali, Serikali ifanye juhudi za hali na mali kuweza kuwaondoa watu hawa kama sehemu ambazo mmeweka ambayo sasa hivi kuna migogoro. Hilo ndiyo lilikuwa ombi langu katika upande wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, kuna eneo moja ambalo liko sehemu za Mugusu, sehemu inayoitwa Rijeti namba 3. Rejeti namba 3 kuna wananchi wanakaa kule, muda mrefu tu, lakini leo hii kwa sababu ya uelewa mdogo walikuwa hawajui kwamba eneo lile ni la mgodi, wamekuja kuvamiwa tu na kuambiwa wahame.

Nilikuwa naomba wananchi wale waachwe kama, kuna uwezekano basi mpime sehemu nyingine. Wilaya ya Geita, Wilaya nzima ina madini sehemu zote ukichimba utapata madini tu. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba kabisa Serikali kama uwezekano basi sehemu ambayo wananchi au wachimbaji wadogo wadogo walipogundua madini yao waacheni waendelee katika kuishi maeneo yale.

Pimeni sehemu nyingine mtapata madini kwa sababu wawekezaji hawa wana vyombo vya hali ya juu, kwa hiyo, wanaweza wakachimba katika kina chochote kile na wakayapata hayo madini. Wilaya ya Geita, tumejaliwa kwa madini na kwa kila hali. Hilo nilikuwa naomba Serikali ilishughulikie kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo naomba lishughulikiwe, natoa kama ushauri tu, wameunda kamati ya kudurufu sheria ya madini, lakini naiona kama inachelewa na sijui kwa nini inachelewa, huenda ikawa inaweza kuwa ikaishia hata Bagamoyo tu ikaja ikatuambia kwamba tumeshamaliza shughuli kwa kupewa kidogo kidogo na Serikali, ili sisi wananchi wa maeneo husika tunyimwe haki yetu ambayo tunaidai kila siku.

Nafikiri mnajua kabisa kwamba sisi tunadai mrahaba tu. Hilo, nilikuwa naiomba kamati ilizingatie jambo hilo kwamba sisi wananchi tunaotoka maeneo ya madini

tunahitaji mrahaba na hilo kama mpo nawapeni hilo mliangalie na liwe ni pendekezo mojawapo katika maeneo yale. *(Makofi)*

Lakini ushauri mwingine niliokuwa nauomba waambieni Serikali ipunguze misamaha ya kodi imezidi mno katika madini. Kila mnapoangalia kuna misamaha ya kodi, mafuta yanaingia, misamaha yake ni mikubwa mno. Afadhali mngeacha kuwasamehe hiyo misamaha, basi hata mrahaba wasichukue, lakini unakuta kwamba mrahaba unakuwa mdogo kuliko misamaha inayotolewa na Serikali. Naiomba kabisa Serikali ijitahidi kwa nguvu zote kuangalia hilo au kamati hii ambayo imeundwa itoe ushauri huo kwamba misamaha ya kodi iondolewe katika mikataba ambayo Serikali inaweka na wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema kwamba Mwenyezi Mungu, ameumba vitu viwili, huwezi ukasema kwamba kuna kibaya na kizuri lazima kuwe na vizuri. Napenda kuishukuru Wizara hii kwa kuweza kutekeleza masuala mengi hasa katika upande wa nishati. *(Makofi)*

Wilaya ya Geita tulikuwa hatuna umeme, lakini wamejitahidi wameweka umeme katika Wilaya ya Geita, mpaka sasa hivi wananchi wa Geita wako katika hali ambayo siyo kama ilivyokuwa maeneo mengine. Lakini naomba kuna vijiji ambavyo bado sasa hivi havijapata umeme. Kuna Kijiji cha Kasamwa, kuna Kijiji cha Katoro, kuna Kijiji cha Karumwa, Nyakagwe na maeneo mengine mbalimbali.

Nilikuwa naomba Serikali katika mpango huu wa umeme wa majaribio ambao mmesema mtaupeleka Mkoani Mwanza, basi huo umeme muupeleke katika maeneo hayo. Jana nimeuliza kwamba je, Serikali itawawezeshaje wachimbaji wadogo wadogo?

Basi umeme ule upelekwe katika machimbo hayo madogo madogo ya Geita ambayo yamejaa, muupeleke kule mkajaribie ambayo inaweza ikatuletea tija na faida kwa wananchi wetu na kuweza kuonekana kwamba kuna wananchi ambao wanaweza wakafanya kazi hii. Lakini mkiupeleka umeme Mjini Mwanza haitaonekana hiyo. *(Makofi)*

Pia nilikuwa napenda kuwashukuru kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya kupeleka umeme Sumve na Malya, ni mpango mzuri kabisa ambao mmeuweka pale, mmeweza kuongeza maeneo ambayo yalikuwa yameachwa lakini sasa Serikali imeona katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sitaki niseme mengi nasema kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Yona na Dr. Msabaha kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii nyeti na kwa bajeti nzuri waliyotuletea. Naomba kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la mafuta. Katika hotuba ya Waziri Mramba nilichangia suala la mafuta na matatizo yaliyopo. Lakini leo naomba nitoe taarifa ndani ya Bunge hili kama mdau wa sekta hii ya mafuta kwamba hali ya mafuta katika taifa letu ni mbaya. *Diesel* iliyopo katika bohari zilizopo Dar es Salaam ni mbaya na wakati wowote kuanzia kesho taifa litakumbwa na uhaba wa *diesel* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nitaje na *data* zenyewe. *THA* wamewaandikia barua au wamewapa *notice* waagizaji wa mafuta, *notice* hiyo, imetolewa tarehe 25/6/2004 kwamba kuanzia kesho *THA* wanafanya maandalizi ya kufunga *flow meter* katika Bandari ya Dar es Salaam. Wakati wanafanya maandalizi ya kufunga *flow meter* kwenye Bandari ya Dar es Salaam, meli zote hazitaruhusiwa kushusha mafuta. Wakati meli hazitaruhusiwa kushusha mafuta tayari katika *reserve* ya bohari hizo mafuta yaliyopo ni kama ifuatavyo; BP hadi jana walikuwa wana *cubic meter* 1700 sawa sawa na 0. *ORYX* walikuwa wana *cubic meter 1280* sawa sawa na 0, *Oilcom* walikuwa wana 0. *GAPCO* walikuwa wana 7,000 itaendelea mpaka kesho kwa maana hiyo kama zoezi hili litaendelea kwa maana hiyo Dar es Salaam kutakuwa hakuna *diesel* kuanzia kesho mpaka Jumatano ijayo.

**MBUNGE FULANI:** Haijapata kutokea.

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nilieleza na niliomba Serikali itupe jibu kwamba hivi nchi yetu inasimamiwa na chombo gani katika sekta hii ya mafuta? Mafuta kama kitu adimu katika Taifa letu, hivi leo kuna chombo gani cha Serikali kinasimamia mafuta? Kitakachotokea katika wiki hii itakuwa ni tatizo kubwa la kitaifa na ni janga kubwa. Tunasema biashara ni huria wanaoagiza mafuta waagize. Lakini katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 27 amesema Wizara kuhakikisha kwamba nchi inakuwa na akiba ya kutosheleza matumizi ya mafuta ya nchi kwa muda wa mwezi mmoja kwa wastani. Sasa leo hatuna akiba hata ya wiki moja, wastani wa mwezi mmoja uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi? Tuliomba *flow meter* zifungwe kwa sababu ya kuongeza mapato ya taifa kuondokana na udanganyifu. Lakini *flow meter* wakati zinafungwa na maandalizi yanafanya ilikuwa ni vyema kuwapa *notice* waagizaji ili wajiandae mapema lakini *notice* ile ni ya muda mfupi na lolote linaweza kutokea kesho. Ningeishauri Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Yona suala la *flow meter* lingeanza tarehe 1 mwezi 8 ili meli zilizoko bandari jana, leo na kesho zishushe *diesel* ambayo tayari kuna upungufu mkubwa. Nikiwa ni mdau wa eneo hilo suala hili nalizungumza kwa uhakika, nazungumzia tatizo la mafuta jinsi lilivyokuwepo. *(Makofi)*

Lakini pia ningeomba Serikali iangalie uwezekano wa kufufua *TIPER.* Suala la *TIPER* nilizungumza sana katika hotuba ya Waziri wa Fedha na nikaelezea tatizo lililopo, majanga yanapotokea, bahati mbaya ikitokea vita, kikitokea chochote ambacho kinaweza kikatokea suala la mafuta itakuwa ni tatizo. Lakini leo Mheshimiwa Waziri, ukifuatilia malalamiko ya waagizaji wa mafuta utagundua haya niliyosema yanahitaji maamuzi ya Serikali ya haraka. Tatizo la nchi yetu kwenye maamuzi tunapata kigugumizi. Zipo

Wizara mpaka leo kuna vigugumizi sana kwenye maamuzi. Hebu tuangalie maamuzi haya kwa nini tunapata vigugumizi? Wapo Waheshimiwa Wabunge, wakati wanachangia kwenye Wizara mbalimbali, walieleza pale bandarini kuna mchele kutoka India tani 5000, unga tani 5,000 leo ni miezi miwili vitu vile havijagawiwa Serikali inapata kigugumizi kutoa maelekezo au kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo letu kubwa katika taifa hili ni maamuzi na utekelezaji na usimamizi. Sasa leo litakalotokea kwenye mafuta ni hatari kwa taifa letu. Naunga mkono hoja ya kufunga *flow meter* kwenye bandari, naunga mkono hoja ya Serikali kuweka *flow meter* kwenye bandari zingine. Lakini kwa kuanzia hili la Dar es Salaam, ningeomba Tume maalum ilishughulikie maana tayari sasa hivi *diesel* imepanda bei kwa shilingi 30 kwa lita leo kutokana na tatizo ambalo limejitokeza jana na leo. Kwa hiyo, ni kazi ya Serikali kufuatilia na sisi Wabunge, ni wajibu wetu kuikumbusha Serikali na kuiomba Serikali kufanya kazi kwa faida ya wananchi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili nimalizie kwa kuomba Serikali iunde chombo maalum cha kusimamia suala la mafuta, kuanzia ngazi ya mwanzo hadi ngazi ya mwisho pamoja na udhibiti wa bei katika vituo vya mafuta, pamoja na soko huria lakini Serikali ina *data* mbalimbali. Leo Waziri atakuwa amepata *fax* kutoka Dar es Salaam kuelezea tatizo jinsi lilivyo na mimi niliwashauri wale wadau wapeleke *fax* hizi kwa Waziri pamoja na Serikali ili suala hili lisukumwe kwa uharaka wake ili kuondokana na tatizo ambalo liko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niingia katika suala la umeme, katika suala la umeme katika Mkoa wa Morogoro, naomba nianze kumpongeza Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro kwa kazi nzuri anayofanya kupeleka umeme katika vijiji mbalimbali katika Mkoa wa Morogoro. Ninampongeza sana meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Morogoro. Lakini ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, inipe jibu ndani ya Bunge hili, kuna mradi wa umeme Tarafa ya Mgeta. Mradi wa Umeme Tarafa ya Mgeta ulianza mwaka 2002 nguzo zimewekwa, nyanya za umeme zimetandikwa kufika katikati ya eneo ya mradi, mradi ule ukasimama. Katika kufuatilia kwangu kama Mbunge wa eneo hilo nikaambiwa kwamba nguzo zilikuwa zimeisha na zimeagizwa tokea mwaka jana. Hadi leo ninapozungumza Serikali, imeshatumia mamilioni ya fedha ili kuanza kwa mradi ule wa umeme Mgeta. Fedha zile hadi leo hazijafanya kazi kwa sababu mradi haujakamilika. Wananchi walipoona kwamba mradi wa umeme Mgeta umeanza wananchi wananchi wametumia gharama yao wameweka waya katika nyumba zao, wameanza kurekebisha nyumba zao kwa kuupokea mradi ule kwa mikono miwili.

Wamenunua vifaa vya umeme, wamejiandaa wanasubiri mradi leo miaka miwili mradi haujakamilika, mamilioni ya fedha yameshatumika. Naomba Waziri, wakati akifanya majumuisho yake atoe tamko ndani ya Bunge hili, kwamba mamilioni ya fedha zile zilizoanzisha mradi ule, je, lini mradi utakamilika?

Nimesoma ukurasa wa tisa kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona kwamba kuna miradi mipya ya umeme, nimeona mradi wa kupeleka umeme Wilaya ya Kilindi,

umeanza kutekelezwa kwa awamu, nimeona mradi wa umeme unavyoshughulikiwa Sumve na Malya, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hayo. Lakini mradi wa Umme wa Mgeta umeshagharimu mamilioni ya fedha, sijaona kwenye hotuba yake. Miradi mipya hii ya Kilindi na Sumve ameitaja ninaomba Mheshimiwa Waziri umeme Sumve na Mvomelo ziende sambamba. Ninaomba kabisa kwa heshimu kubwa nitasubiri kauli ya Waziri kwa sababu tuokoe fedha ambazo zilianzisha mradi huu. *(Makofi)*

Wilaya ya Mvomero ni Wilaya mpya, inayojengwa katika eneo la Wami Sokoine. Eneo lile limetengwa maalum kwa ajili ya kujenga Mji wa Kisasa. Zamani kulikuwa na *transformer* kabla ya Wilaya kugawiwa, transformer ile ikaendolewa na *TANESCO* kwa maana kulikuwa hakuna watumiaji. Ninaomba *TANESCO* sasa warudishe *transformer* ile Wami Sokoine kwa ajili ya maandalizi ya kujenga Wilaya mpya ambao ujenzi wa Boma la *DC* na ofisi mbalimbali unaanza mara moja. Tunaomba Wilaya ya Mvomero ianze kupatiwa umeme kwa maandalizi ya kujenga mji wa kisasa na tayari line ya umeme ipo tatizo letu pale ni transformer. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekondari ya Mvomero iko ndani ya Kata ya Mvomero, Kata ya Mvomelo kuna umeme, lakini hatua chache kutoka pale kuna sekondari ambayo haina umeme. Waziri Mungai, kila siku anazungumzia umuhimu wa umeme katika sekondari, anazungumzia masuala ya kompyuta, anazungumzia mambo mengi tu. Tumuunge mkono Waziri Mungai kwa kupeleka umeme Sekondari ya Mvomelo. Sekondari ya Mvomero mwaka jana imefaulisha wanafunzi wa *division one* wanafunzi 8 leo tukipata umeme tunaweza tukafaulisha hata darasa zima kwa sababu kutakuwa na mambo mengi pale. Lakini umeme upo ndani ya Kijiji cha Mvomero ni hatua chache. Kwa kazi nzuri ya Bwana Kamoleka Meneja wa *TANESCO Morogoro* nina hakika tukimwunga mkono anaweza akafanikisha kupeleka umeme Sekondari ya Mvomero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaomba pia umeme upelekwe kwenye Kijiji cha Kidudwe kinachopakana na Kiwanda cha Sukari Mtibwa. Mtibwa kuna umeme, Lusanga kuna umeme, Madizini kuna umeme ni hatua chache kutoka Mtibwa, Lusanga, Madizini kwenda Kidudwe. Wananchi wa Kidudwe wameomba umeme muda mrefu ni wakulima wa miwa, wanapata mapato mazuri na makubwa. Wamejenga nyumba bora za kisasa, ni vema tukawaunga mkono kuondokana tatizo hili la umeme wanashindwa hata kujikwamua katika wimbi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yangu kwa leo yalikuwa ni hayo naomba tena kuwapongeza watendaji wote wa *TANESCO,* niwapongeze tena *TANESCO* lakini bado Morogoro kama Manispaa ya Morogoro kuna tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika Manispaa ya Morogoro. Suala hili tumeambiwa ni suala nyeti, linahitaji fungu kubwa. Kwa hiyo, Manispaa ya Morogoro kama kuna bajeti yoyote basi nguvu zielekezwe tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika Manispaa ya Morogoro liondokane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru tena wewe binafsi kwa kuniona na nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucas Selelii, hayupo kumbe, anayefuata ni Leonard Shango ingawa naye hayupo. Basi anayefuata ni Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ingawa kuna dakika kumi tu, lakini ukijipanga vizuri utachangia. Nina maombi mengi kwa hiyo, ningependa kutumia kila muda uliopo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kahumbi tafadhali toa mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupewa nafasi hii, ingawa muda wenyewe ndiyo kidogo lakini nafikiri utaniongezea baadaye. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda niseme kwamba naunga mkono hoja hii. Ninazo sababu tatu za kuunga mkono hoja hii. Sababu ya kwanza ni kwamba pamoja na kwamba kwa miaka 15 nimekuwa nikiomba umeme katika jimbo langu sikufanikiwa kupata. Lakini safari hii Mheshimiwa Naibu Waziri, alitembelea Wilaya ya Nzega, nikamtembeza sehemu nyingi.

Lakini kana kwamba haitoshi, Mheshimiwa Waziri, akatembelea Wilaya ya Nzega, akatembelea mahali pengi. Katika kutembea kwake kunajitokeza sababu ya tatu ambayo inanifanya niunge mkono hoja. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri, alipewa na akapokea zawadi ya koroboi kule Ndala. Sababu hizi tatu zinanifanya niunga mkono hoja hii kwa kufuata tu msemo wa Waswahili. Waswahili wanasema ukitaka kumuua nyani usimwangalie usoni. Lakini ukimtazama utamhurumia. Kwa hiyo, ujio wao kuja huko walikuja kututazama kwa hiyo, hawako tayari kutuua. Kwa kuwa hawako tayari kutuua, basi tunawaunga mkono. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo wana matatizo, matatizo haya ningeomba niwasaidie. Mheshimiwa Nyimbo amesema kwa hali ya juu sana, alikuwa anazungumza na watu wasomi kabisa. Sasa mimi nataka nizungumze kwa hali ya watu wa kawaida kule kijijini. Sera ya *TANU* pale mwanzo ilikuwa ni kudai uhuru. Sera yetu ya leo ni kuimarisha uhuru kwa kupiga vita ujinga, umaskini na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zana muhimu ya kupiga vita umaskini ni nishati. Sasa inashangaza, Bwana Nyimbo amesema kama watu hawakusoma maana wanafanya mambo kienyeji sana. Katika sera kubwa ya nchi hii ni kuondoa umaskini, visera vingine vidogo vidogo vipo ni kama mikakati ya kuitimiza sera hii. Sera kubwa kabisa na Rais wa Nchi hii, akasema amechagua *cabinet* akaipa jina zuri kabisa askari wa miavuli kuondoa umaskini. Kama hawa watu watakuwa maskini basi uhuru huu hauna maana. Sasa mkubwa wa kuondoa umaskini ni Yona, sasa huondoi umaskini, unafanya kazi kama *adding machine,* maana adding machine ukijumlisha mbili na tatu na wewe ulitaka kujumlisha tatu na tatu itatoa jibu tano, lakini wewe ulitaka sita. Sasa wewe umeambiwa kwamba kisera hiki kidogo peleke umeme Wilayani, Mikoani na kwenye mashirika, lakini huo siyo uchumi. *(Makofi)*

Kuna Wilaya zingine hazijajenga hata jengo moja. Sasa mimi ningoje umeme mpaka wajenge Wilaya iishe ndiyo nianze kusema na Bukene pelekeni umeme? Tumesema tutahamia Makao Makuu Dodoma, basi miradi mingine yote isimame mpaka

tuhamie Dodoma? Tutajenga nyumba jengo la Ukumbi wa Bunge, tuliambiwa linajengwa hapo nje tunapo-*park* magari, tukaacha na ku-*park* magari, leo tuna-*park* pale. Sasa ninyi kama watalaam, kama askari wa miavuli mtazame uchumi ili ukue.

Wewe Mheshimiwa Waziri, ulipopewa koroboi na wale watu wa Ndala ulielewa wanakuambia kwamba ukumbuke kwamba umeme Ndala haupo, siyo hivyo tu, walitaka umulike uone hivi mnavyofanya ni sawa? Sasa hivi hapa mzee wangu wa Kondoa alikuwa akisema vijiji vingi orodha kubwa, Wilaya ya Nzega ina vijiji viwili tu vyenye umeme. Umeme ulitelemka mimi nikiwa Mbunge hapa watu wa Nzega walikuwa wanafungua nati *(bolt)* zile kwenye nguzo za umeme wanatengenezea *ox-cut* wakawakamata, tuko kwenye Bunge hapa Dodoma. Nikaletewa watu ma-*ox cut* karibu watu 30 wako polisi, nikawaambia waacheni kwa sababu zile *bolt* wakifungua *ox - cut* wanaelewa zina faida. Lakini ikipita tu utosini hapa lina faida gani? Wakaawachia na ndipo wakatelemsha umeme katika kijiji kimoja cha Nata mpaka leo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, juzi Wilaya mpya ya Igunga wamepeleka umeme kutoka Nzega shahidi Mheshimiwa Omar Kwaangw' nimempeleka mpaka pale. Wametelemsha umeme katika kijiji kimoja cha Nzega ndogo hawakukipa umeme kile kijiji ukapelekwa Igunga mbio tu. Pale pana kijiji, kuna kituo cha afya, kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao walianza kabla ya Lusu, wakaacha. Wamepeleka Igunga kule wamepeleka mpaka vijijini, sera ya Yona, inasema upeleke umeme kwenye viwanda vinavyosindika mazao ya wananchi, Makao Makuu ya Wilaya na kwenye vijiji kando ya njia hiyo. Lakini wamepeleka mpaka kilometa 40 nje ya ile njia. Sasa ndiyo watu wa Ndala wakakupa koroboi kwamba hivi kuna nini huko kunakopelekwa umeme? Maana Ndala kuna hospitali kubwa haijapelekewa umeme, huko kunakopelekwa umeme kijijini kuna nini? *(Makofi)*

Juzi Naibu Waziri, alikuwa akilalamika hapa Mlalo kuna wateja 200 tu hivi kule mlikopeleka umeme, hata wateja 20 hawafiki. Sasa mtuambie kuna nini? Mheshimiwa Waziri pale Ndala kuna wastaafu, mimi nilikuwa Mbunge wa Wilaya nzima, kile kijiji kilikuwa na wastaafu 27 ambao ni Maofisa wa Serikali wasomi ndiyo hao waliokupa koroboi umulike uone hivi kuna nini? Kwa nini, kama unapeleka umeme kule kilometa 40 kwenye kijiji kuna *secondary school* moja, kule Bukene kuna viwanda, nilitaka kuleta kiloba cha mchele hapa wa tule na bwana kwenye Bunge, kuna kiwanda kikubwa kinasindika mchele tunapeleka mpaka Zaire, Burundi, Rwanda, Uganda hakuna umeme. Nilimpeleka Naibu Waziri pale akakiona kile kiwanda akachukua na takwimu leo unapeleka umeme kwenye kijiji halafu mje msingizie ni wale makaburu ndiyo wanahujumu uchumi wa nchi hii. Makaburu wana akili tusiwasingizie, ni ninyi mnahujumu uchumi wa nchi hii. Hivi kweli mtainua uchumi wa nchi hii kwa kupeleka umeme kwenye kijiji kimoja? Si afadhali mpeleke kule Bukene ambako kuna viwanda, kuna *secondary school* mbili, kuna *health center* tatu, kuna *railway station,* kuna polisi, kule ni mbali kilometa 40, kule kilometa 40 mlizopeleka kuna nini? Hii inasikitisha lakini mimi nawaunga mkono. Mtajionea wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wa kuahirisha Bunge umefika. Nilikutahadharisha kwamba una dakika kumi tu.

**MHE. STEPHEN KAHUMBI:** Kwa hiyo....

**SPIKA:** Kwa hiyo, unaunga mkono hoja. Ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, sasa lazima Bunge likapumzike. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Asubuhi ilibaki dakika tano kwa Mheshimiwa Stephen Kahumbi. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Stephen Kahumbi atafuatia Mheshimiwa Omar Oscar Mloka, halafu Mheshimiwa Charles Kagonji, pia ajiandae na Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniongezea dakika zangu tano na nitafupisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nilieleza labda nikazie tu kwamba ndugu zetu wa Nishati wakumbuke tu kwamba nishati ndio msingi mkubwa wa kuleta maendeleo na kuufukuza umaskini katika nchi hii. Kwa hiyo ningewaomba wasifanye kazi kama mashine, wafanye kazi kwa kutumia elimu ya uchumi kwamba mahali ambapo wanaona ukipelekwa umeme utaleta tija wapeleke, wasing'ang'anie tu kwamba tulisema tunapeleka Wilayani. Nilisema kwamba kuna Wilaya nyingine kati ya Wilaya 18 nyingine ni za zamani sana kama Nkasi.

**MBUNGE FULANI:** Na Biharamulo

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Na Biharamulo. Wilaya hizi tangu enzi za Wakoloni hazijapata umeme, lakini nyingine hazijajenga hata nyumba moja. Ndio nikasema sasa tukizingoja hizo mpaka tujenge ndio tupeleke na umeme kwa sababu huko Bukene sio Wilaya, tutakuwa hatutendi haki kwa sababu tutazame *viability,* umeme ukipelekwa mahali fulani ule mradi utakuwa *viable?* Ndio misingi ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa umeme ningependa niishie hapo, niseme kidogo tu kuhusu madini. Tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu kwamba sehemu zinazopata madini zenye migodi tukiomba tupewe pesa kidogo, nashukuru sana Wizara hii na naipongeza imetuonesha hapa nchi mbalimbali za Afrika na dunia zinavyogawa mapato yake yanayotokana na madini. Mahali pengine sijui vizuri, lakini ninapopajua vizuri ni Ghana. Ghana mimi nilikwenda kwa shughuli ya machimbo ya madini tu, nikakuta kama inavyoonesha hapa kwamba wanatoa *royalty* asilimia 12 na *income tax* wanatoa asilimia 35. Pesa hizi zinakusanywa na *Mineral Commission of*

*Ghana.* Halafu *Commission* inagawa, sehemu fulani inapelekwa Serikali Kuu na sehemu fulani inapelekwa kwenye Serikali za Mitaa na nyingine inapewa Machifu kwa sababu wenzetu bado wana Machifu. Tunachokiomba sisi ni kwamba Serikali ikusanye mapato hayo lakini Serikali za Mitaa ambazo ni sehemu ya Serikali yenyewe nao wapate kidogo kuliko Serikali inaonekana kwamba ni *greedy* inachukua kila kitu wakati watu walioko kule wanahitaji maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba Serikali kwamba Tume iliyochaguliwa ambayo mmoja wa Wabunge ni Mjumbe hatuwezi kuingilia kwa sababu haijatoa taarifa yake, lakini itakapotoa izingatie kwamba hatuhitaji zile pesa zigawanywe na viongozi wa Wilaya, zinatakiwa zitumike kwa maendeleo ya sehemu ambako migodi ipo kuliko Wabunge kulalamika hapa wanaleta mavumbi kwamba niyamwage huko mbele muyaone kitu ambacho sio kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nilikatizwa sana, nimevurugikiwa sana. Naomba niishie hapa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote ningependa na mimi niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu Yete Mwalyego, ambacho kilitokea wakati Bunge lako likiendelea hapa Mjini Dodoma. Niwatakie kheri wapigakura wake wa Jimbo la Mbeya Vijijini wawe na moyo wa uvumilivu kwa tukio hili lililowapata.

Pia niwape pole ndugu zangu ambao wamepatwa na misiba, Mheshimiwa Abdallah Kigoda na dada yakeDr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao na Mzee wangu Lawrence Gama na ndugu yangu Parmukh Singh Hoogan ambao wamefiwa na watoto wao siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe pole kwa Wabunge wenzetu ambao walipatwa na mikasa ya ajali wakati wakielekea hapa Dodoma kwenye Bunge lako Tukufu ambao ni Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Makongoro Nyerere ambaye bado yuko Hospitali na ndugu yangu Estherina Kilasi. Mwenyezi Mungu awape afya njema.

Napenda kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga ambaye alipata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mdogo uliopita safari hii akiwa amegeuka akigombea kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Ningependa sana nimpongeze na nimkaribishe huku tulipo ili aweze kuongozana nasi katika jahazi ambalo liko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo basi, ningependa sasa nichukue nafasi hii nijielekeze kwenye hoja ambayo ipo mbele yetu. Kwanza kabisa pengine nisije nikasahau niseme naiunga mkono hoja mia kwa mia. Kama yapo nitakayochangia ni kwa maana ya kuboresha na si kwa maana ya kutaka nikosoe. Hivyo basi, nampongeza Waziri

wa Nishati na Madini, Naibu wake na viongozi wote ambao wamesaidiana katika kuweka sawa mpango mzima wa bajeti na ufafanuzi wa kina katika kuelekeza Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nianze na Sekta ya Madini. Mkoa wa Morogoro umebahatika sana kuwa na utajiri mkubwa wa madini chini ya ardhi yake. Inaelekea kila utakapojaribu kuchimba huwezi kukosa kama sio dhahabu basi ni *ruby* au madini ya namna moja au nyingine yanayopatikana humu nchini mwetu. Ni bahati mbaya tu kwamba madini haya pale Morogoro yanagunduliwa na wananchi wa kawaida tu ambao hawana utaalamu wa kutambua au kubainisha hayo, umekuwa ni wa kubahatisha tu. Nafahamu kuwa Wizara ina Watendaji wengi wenye taaluma hii na waliobobea lakini nadhani bado hawajatumika ipasavyo katika kuainisha madini ya aina gani yako wapi katika nchi yetu na pembe zake zote ukiachilia mbali maainisho yaliyoachwa na Wakoloni waliotutawala siku za nyuma kama Wajerumani na Waingereza ambayo kwa kweli ni sehemu chache tu ambazo zinaonekana na ni zile ambazo sasa tayari zinafanyiwa kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2003 wakati nachangia hoja hii nilimwomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam wake waje kuangalia dhahabu iliyogunduliwa na wananchi wa pale Mjini Morogoro kwenye maeneo ya Mindu na Merera ili kubaini kuwepo kwa mwelekeo wa mkondo wa dhahabu hiyo ili wakazi wa Mji huo waliovamia kwa kuchimba holela maeneo hayo waweze wakahamishiwa huko. Pia niliwahi kuleta swali ambalo lilitazamiwa kujibiwa Jumatatu ijayo, lakini nimelazimika kuliondoa lile swali baada ya kuona kwamba inawezekana kabisa likaleta hisia tofauti kwamba mimi naungana na watu wengine kusababisha maafa katika Mji wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji unaofanywa pale unahatarisha maisha ya wakazi wa Manispaa ya Morogoro kutokana na kutumia *mercury,* nadhani kwa Kiswahili inaitwa zebaki ya kusafishia hii dhahabu ambayo baadaye hutiririka na kuingia katika Bwawa la Mindu ambalo kwa hakika ni tegemeo kubwa sana la chanzo cha maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro wapatao asilimia 75 wanatumia chanzo hiki cha maji. Kwa hiyo kitakapokuwa kimeathirika kwa namna yoyote ile, mimi nitakuwa nakosa hata kura kwa asilimia hiyo niliyoisema. Sasa nitakuwa mtu wa ajabu sana kama na mimi nitashiriki kuweza kukubali uharibifu huu uendelee kufanyika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa kinatuzuia pale ilikuwa kwa kweli ni kigugumizi cha kuwahamisha wananchi ambao wako katika Kijiji kile cha jirani, lakini kwa bahati nzuri wao wenyewe wameona uchafuzi ambao unaendelea na kwa bahati nzuri kabisa wamekubali kuondoka, kusogea wawe nje ya mipaka ya lile bwawa. Sheria ya kuwepo kwa bwawa au chanzo cha maji inataka kusiwe na shughuli za kibinadamu zinafanyika katika umbali wa mita 500 kutoka kwenye kingo za bwawa au ziwa.

Mheshimwia Naibu Spika, baada ya kuweka vipimo vile, kwa roho moja wamekubali kutoka nje ya mipaka hiyo. Kwa hiyo, hiyo imekuwa ni faraja sana kwetu sisi. Hivyo juzi siku ya Jumamosi tumekaa kama uongozi wa Mkoa, Wilaya, wote kwa

upande wa Chama na Serikali na tulishirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, tukakubaliana kimsingi kabisa kwamba shughuli za uchimbaji pale ziondoke kwa sababu baada ya kukagua eneo lile imeonekana kwa kweli hata bomba la mafuta lililopita pale kwenda Zambia tayari lilikuwa limetoswa sululu.

Kwa hiyo, likishapasuka, maana yake hata bwawa lenyewe litakuwa halipo. Hivyo, kwa hali ya namna yoyote uongozi na Serikali imesema kwamba ulinzi lazima uwepo kwa namna yoyote ile na sasa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Manispaa ya Morogoro imilikishwe eneo lile ili waweze wakalilinda wao badala ya kuliachia tu likakaa kama halina mwenyewe. Kwa hiyo, hii ni faraja nimeona basi niliseme hapa na kila mmoja afahamu kwamba kuna madhara ambayo yalikuwa yanatuelemea kutokana na matumizi ya chanzo kile cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kile chanzo cha maji usanifu umekadiria kwamba kinaweza kikatumika kwa miaka 50 inayokuja, lakini kwa uchimbaji ule unaoendelea na shughuli za kibinadamu zinazoendelea kando kando ya bwawa lile, sio ajabu hata miaka kumi inaweza isifike bwawa lile likawa limejifukia na hatimaye tukakosa kabisa chanzo ambacho kinaweza kikatupa huduma zipasazo katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupata chanzo mbadala tunahitaji si chini ya Shilingi bilioni 100 ili tuweze kutafuta chanzo kingine ambacho ni cha Mto Wami au Mto Mgeta ambao uko katika umbali karibu wa Kilomita 50 kutoka katika Mji ule wa Morogoro. Hivyo mimi niombe tu Wizara tuwaombe sana wasimpe mtu yeyote leseni ya kuchimba katika eneo lile. Madini yako mengi katika maeneo mengi ndio maana nimesema ni vyema wataalam wakatumika ili yabainike maeneo hayo na wanaohitaji kujipatia kipato kwa kupitia mkondo huo, basi waelekezwe kule na sio pale katika bwawa lile la Mindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda nigusie na upande wa Sekta ya Nishati kwamba niliwahi kutoa ombi kwa Wizara kunisaidia katika usambazaji wa umeme katika Manispaa yangu kwa maeneo ya Bigwa na Konga ambako pia tunacho Kituo cha Afya pale chenye umuhimu wa namna yake. Nilipewa masharti kwamba tutazame ni wateja wangapi ambao wanaweza wakarudisha gharama zile zitakazokuwa zimeingiwa na *TANESCO*. Nilifanya kazi ile na kwa bahati nzuri baada ya kuiwasilisha, kwa eneo la Bigwa tayari wameshaweka transformer na wanasambaza nguzo za umeme, lakini mradi ule sasa ni mradi ambao unafuata barabara tu, hauingii waliko wananchi ambako wanahitaji huduma hiyo. Watahitajika wengine kuvuta kwa nguzo nyingi sana hadi uweze kuwafikia katika maeneo yao. Watu wameshalalamika, hivyo nimeona nilete ombi rasmi kwa sababu mradi ndio bado unaendelea basi wasogeze angalau nguzo mbili mbili kwenye barabara ambayo inaingia ndani ili angalau uvutaji wa umeme uwe wa gharama nafuu hasa ukizingatia kwamba na fedha nyingi zimekwishatumika, ni sawa na ng'ombe umekwishamla umebakiza mkia. Basi, tuweze kuwapatia wananchi hawa waingize umeme hatimaye gharama tulizozitumia zinaweza zikajirudisha kwa ukaribu zaidi. *(Makofi)*

Kwa Kijiji cha Konga bado kazi hii haijaanza, hivyo nasubiri kwa hamu kuona ahadi hiyo inatekelezwa hasa baada ya kuifanyia kazi haja ya kuona kwamba ni wateja

wangapi walioko katika mkondo ule au eneo lile ili waweze kupata huduma ya umeme na kwa kweli nimepata idadi ya watu kama watu 85 ambao nadhani wanatosha kabisa kwa *transformer* moja kuweza kuwekwa pale ikateremsha ukizingatia kwamba tayari umeme wa Msongo wa Kati wa *Kilovolt 11* umepita pale Konga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa nichukue muda mrefu, maana naona kengele imelia, basi napenda nirudie tena kwa kusema kwamba sina sababu ya kutokuunga mkono hoja hii, ipite mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya pili leo jioni ili nami niungane na wenzangu Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi hizo kutoa mchango wangu katika hoja ambayo iko mbele yetu. Lakini kabla sijaendelea naomba nifanye kazi moja nyingine kama nilizozifanya wakati wa Bajeti, lakini nifanye moja inayohusiana na msiba mkubwa uliotupata hapa Bungeni wa Ndugu yetu, mpendwa wetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Napenda kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mlalo, tutoe rambirambi zetu za dhati kwa familia yake na wale wote aliokuwa anawawakilisha katika Jimbo lake. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimesimama hapa kusema machache kuchangia, lakini ningependa awali ya yote kabisa kumwondoa wasiwasi Mheshimiwa Waziri Yona na ndugu yangu, rafiki yangu Dr. Msabaha kwamba hoja hii ninaiunga mkono. Nitasema machache ya kuboresha hapa na pale na yale ambayo ninayaona sikubaliani nayo nitasema lakini kwa ujumla naiunga hoja mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni kubwa sana, kazi ya kusambaza umeme nchini pamoja na kazi ya kusimamia Sekta ya Madini ni kubwa zaidi pia, lakini pesa za kusimamia na kutekeleza shughuli za Sekta hizo mbili ni chache sana.

Lakini niseme tu kwamba nafarijika sana kwamba Wizara hii inajitahidi kwa uwezo wake pamoja na hali duni na mazingira magumu wanayofanyia kazi. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watalaam wa Wizara hii kwa jitihada wanazotuonyesha kwamba kwa kweli wanatupa nguvu tusikate tamaa tuamini tu kwamba siku moja haiwi haiwi itakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze zaidi ndugu Msabaha kwa kazi nzuri anayoifanya ya kujibu maswali ya Wabunge hapa Bungeni. Kusema kweli anajibu maswali ya wananchi kupitia kwa Wabunge wao vizuri sana kiasi kwamba anatupa matumaini hata pale ambapo tunakaribia kukata tamaa lakini anasaidia kutuongezea matumaini. Sasa niseme kwamba pia wao wasikate tamaa, waendelee kujitahidi pamoja na kubanana na yale mengine ambayo nitasema ya kuwaomba wanisaidie zaidi kwenye Jimbo langu, nitaomba wasinune wala wasichukie kwa sababu kazi ya Ubunge ni ngumu wote mnafahamu. Ukienda huku unaminywa, ukienda huku unasukumwa, ukienda huku

unabanwa, kwa hiyo kwa yale ambayo nimetumwa itabidi na mimi niyazungumze na nitaomba wenzangu wanivumilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na machache sana ya upande wa madini. Ningependa kuzungumzia kuhusiana na wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Hivi Wizara yetu hii ya Nishati na Madini inawasaidiaje wachimbaji wadogo wadogo wa madini? Hivi inawaandalia utaratibu gani wa kupata nyenzo za kufanyia kazi zao? Hivi inawasaidia vipi waweze kupata mikopo ili na wao wajisukume mbele zaidi? Hii ni kazi ya Wizara hii, ni muhimu kabisa itusaidie kutuonesha ni namna gani wachimbaji hawa wadogo wadogo wanaweza kusaidiwa na hatimaye baadaye wasiendelee kubakia wachimbaji wadogo, nao wakue basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti mdogo niliofanya ni kwamba wachimbaji hawa wadogo wadogo wanasaidia zaidi kuwekeza mali zao hapa nchini kuliko wachimbaji wakubwa. Pale Arusha ukipitapita utaona kuna uwekezaji mwingi sana wa vijana wetu ambao wanafanya kazi ya kuchimba madini pale Mererani. Kuna estates za majumba pale, kuna hoteli, kuna majumba ya starehe, kwa hiyo hawa wanawekeza zaidi nyumbani kuliko hata hawa wageni ambao mnawapa na mnawaita wachimbaji wakubwa wakubwa. Kwa hiyo naomba tuwasaidie hawa ili nao waweze kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninaomba Wizara hii inayohusika na wachimbaji hawa wadogo wadogo, basi isimame imara kuwasaidia na kuwatetea. Hivi karibuni yameonekana manyanyaso mengi makubwa kwa hao wachimbaji wadogo wadogo wakiwa wanagusana na wachimbaji wakubwa. Juzi, rafiki yangu Kone alisema yale yaliyotokea kule Mererani. Ninaomba mtusaidie yale yaliyotokea kule yasiendelee kutokea. Ni mambo mabaya sana ikiwa wawekezaji wageni wataanza kutumia silaha kuwamaliza vijana wetu wanaotafuta riziki yao katika eneo lile. Mbaya zaidi, nchi hii ni nchi ya amani ambayo hata mtu akifanya makosa mchana hastahili kuuawa wala kunyanyaswa, anastahili kuchukuliwa hatua za kisheria. Ninaomba tafadhali Wizara hii ituonyeshe njia katika kuwaonya wakubwa hawa wabadili mtazamo wao, vinginevyo msije mkatukumbusha mbali. Maana mnafahamu alisema hapa juzi Rais Nujoma kwamba nchi hii ndio ilikuwa kitovu cha wapigania uhuru. Kwa hiyo msitukumbushe mbali tukaja kufikiria mabaya zaidi kwa mahusiano haya yanayoanza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niendelee kuzungumzia suala la umeme. Kuna kitu wanaita Wakala wa Umeme na Mfuko wa Nishati Vijijini. Wametaja tu kwamba Serikali inakusudia kuanzisha; Je, vitaanzishwa lini? Utaratibu wake wa fedha utakuwaje? Utaratibu mzima wa kuwahudumia wananchi Vijijini kwa kuwapelekea umeme kwa Wakala huu na Mfuko huu utakuwa vipi? Ninaomba tusaidiwe maelezo ili tupate kauli ya kusema tukirudi kule nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushe tu kwamba tarehe 30/6/2004 tukiwa hapa Bungeni bahati mbaya nilikwenda kumzika Mwenyekiti wangu lakini bahati nzuri pia Ndugu yangu Singo akaniulizia swali Na.157. Swali hili lilijibiwa vizuri sana na Naibu Waziri wa Wizara hii na katika kujibu akatuhimiza Waheshimiwa Wabunge

tujitahidi kuhamasisha wananchi katika maeneo yetu, wengi wajiwekee umeme pale ambapo umeme umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliendelea kusema kwamba kule kwenye Jimbo langu ni watu 229 tu ambao wameweka umeme tangu umefikishwa kule. Nashukuru ni kazi ya Serikali ni kauli ya Serikali wala siipingi, lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutambua kwamba yapo malalamiko ya wateja wao wa umeme kule Vijijini na nchi nzima, malalamiko ambayo kwa bahati nzuri ameyataja baadhi katika ukurasa wa 13 ile *paragraph* ya 23.

Kwa ruhusa yako, malalamiko haya ni pamoja na yale ambayo wanalalamikia wale wanaotaka kuwekewa umeme na wale ambao tayari wameshawekewa umeme. Yanasema hivi: "Wateja wamekuwa wakilalamikia *TANESCO* kwa kero mbalimbali zikiwemo kukatikakatika kwa umeme, matukio ya moto yanayotokana na umeme, bei kubwa ya umeme, kuungua kwa vifaa kutokana na umeme kuwa na nguvu kubwa kupita kiasi na kuchelewa kufungiwa umeme baada ya kukamilisha taratibu zote."

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema nashukuru sana kwamba Mheshimiwa Waziri ametueleza baadhi ya hizo kero. Lakini ziko kero zaidi ya hizo. Kwa mfano kule kwangu wako watu wengi wanataka kufungiwa umeme, lakini inachukua muda mrefu sana hadi kufungiwa umeme. Wakiomba kufungiwa umeme wanaambiwa hakuna nyaya, hakuna mita, hakuna nguzo na hali hii wanadai pengine zaidi ya miezi sita, miezi saba mpaka mwaka mmoja na wakati ikipatikana pengine mita moja, analetewa mmoja kwenye bahasha, bwana imepatikana hii anafungiwa.

Kwa hiyo, hali ya namna hii inatuchelewesha sana kwa watu wengi kuomba kuwekewa umeme kwa sababu ya masharti yalivyo magumu ya kuweka umeme. Ninaomba Wizara hii iangalie eneo hili. *(Makofi)*

Lakini la pili, ninashangaa mradi mzima wa umeme unaweza kuwa wa kilometa 200, 400,1000, nguzo, vikombe, nyaya zote ziko kwenye mradi. Lakini wanapopeleka umeme wakifikisha pale Kijijini kila nguzo inauzwa. Hebu tuambieni hali hii itakuwa vipi? Umeme umefika pale, watakaowekewa umeme ni wale wachache sana ambao nguzo zile za mradi zimepita. Ukiwa umbali wa nguzo moja, basi kule kwangu watu wanalipishwa Sh.500,000/=. Hebu niambie, Sh.500,000/= kwa nguzo moja, hii ndio bei kweli ya nguzo? Lakini ndiyo hivyo. Umeme utapanukaje kule Vijijini? Nani ataweza hiyo kazi? Badala ya kupunguza umaskini kule Vijijini unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna maeneo yangu mengi sana zikiwemo Shule za Sekondari wanahitaji kupelekewa umeme, lakini watafanyaje kama wako mbali, mpaka wapate nguzo mbili au tatu watazipataje? Inakuwa ngumu! Mimi naomba waondoe habari hii ya kulipia nguzo hasa kule Vijijini kwa sababu umeme tusifikirie ni kitu cha starehe leo au cha anasa. Umeme ukitaka leo, upambane na utandawazi, ukitaka leo ujihami na utandawazi lazima upate nishati ya umeme.

Kwa hiyo, msifikiri kwamba kitu hiki ni cha anasa, kusema kweli naomba kabisa Wizara hii isimamie hili kuondoa gharama za nguzo kule vijijini, zote ziingizwe kwenye utaratibu wa mradi. Kwa hiyo, baada ya miezi sita, mwaka mmoja, Mlalo itakuwa na watu zaidi ya 1,000 ambao watakuwa wamefungiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tunayo *Kwemaramba Secondary School,* inahitaji nguzo nane zifike pale, shilingi milioni 4 tunaambiwa tulipe. Tutatoa wapi? Kuna shule ya sekondari ya Lukozi inahitaji nguzo nne, shilingi milioni 2, tutapata wapi kupeleka huko? Pale Kwevigingi kuna nyumba nzuri sana, vijana wamejenga pale. Kuna Zahanati ambayo tunataka tuipandishe daraja, nguzo kumi, shilingi milioni 5, tutawezaje kuweka hiki kitu?

Pale Tiku, umeme uko Lukozi, umeme uko Viti hapa katikati, robo kilometa tu, unahitaji nguzo nane, shilingi milioni 4. Hivi hii kazi mkitulaumu sisi tufanyaje sasa? Haiwezekani, naomba Serikali iondoshe vitu hivi ili wananchi wengi waweze kufaidika na kuwekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili tuna tatizo la *transformer.* Sijui nani anawaangalia hawa watu kule Vijijini. *Transformer* zikiharibika hakuna anayetengeneza, pale Malindi, Mwangoi, Viti, ziliharibika *transformer* miezi saba, mpaka wakati natoka nyumbani bado hazijatengenezwa wala kupatiwa nyingine. Sasa jamani mnapotulaumu, tunaomba tusaidiane hizi gharama tuzibebe wote, kazi hizi zifanywe kwa haraka ili tuweze kusonga mbele. Gharama za umeme ni kubwa sana, zimeelezwa na wenzangu wamezisema nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme kwamba mara kadhaa nimesimama Bungeni hapa kuipongeza Wizara hii na Serikali kwa kweli kwa mzigo mkubwa na kazi nzuri wanayoifanya nchini. Nchi ni kubwa sana, umeme kuupeleka kila mahali ni ngumu. Lakini palipo na nia pana njia ninyi mnajitahidi.

Sasa nikimaliza kusifu na kupongeza, naomba nirudie tena maana hata leo mkinipa chakula kizuri, pilau na viungo vyote kesho bado nitahitaji kula. Kwa hiyo, jamani nina maeneo ambayo tayari kabisa yamekamilika. Nafahamu kwamba hapa nchini ziko Wilaya zingine hata mashine ya kusaga na kukoboa pengine moja au mbili hakuna. Mimi maeneo haya ambayo nimekuwa nikiyasemea kila siku ndani ya Jimbo langu, kama pale Kijiji cha Lukozi ninapokaa, kuna mashine za kusaga na kukoboa 10. Maeneo ya kule Sunga ninayoyasema ni viwanda vya kupasua mbao. Kule Irangwi, Gologolo, Manolo mpaka pale Mnazi ukivihesabu hivyo vyombo peke yake kwa kweli ni zaidi ya 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mnataka vigezo gani ili mpeleke umeme? Namshukuru Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ameeleza. Yapo maeneo ambayo yamepelekewa umeme, watu hata wawili hawana uwezo wa kuingiza umeme ndani ya nyumba zao. Sasa tunasema tunaangalia masuala ya uchumi basi tuangalie kule vijijini kwa wale ambao wako tayari kupelekewa na wana uwezo kiuchumi tusaidieni, msiwagandishe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Bungeni hapa tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba yale maeneo ambayo yamechelewa kupata Shule za Sekondari basi Serikali ifanye hiyo kazi. Nashukuru sana kwa haya ninayoyasema naomba niletewe umeme. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia na kabla sijasema lolote na mimi nitoe rambi rambi zangu na kwa niaba ya wapiga kura wangu kwa Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye tulikuwa naye Kamati moja. Kwa kweli tumesikitishwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tangu mwanzo kwamba siungi mkono hoja hii na ninasema hivyo siyo kwa sababu ya uadui wowote na ndugu zangu Mawaziri wa Wizara hii. Najua wanajitahidi kufanya kila waliwezalo kwingineko. Tatizo langu ni Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alikuja mpaka Kigoma Mjini tukakaa naye na akatuambia maneno mengi mazuri na mimi nikasema pale kwenye Kikao kuwa Mheshimiwa Waziri tumechoka na nikamtuma nikasema Mheshimiwa Waziri na umwambie Mkurugenzi wa *TANESCO* alinidanganya *Airport,* alisema dokta kuanzia sasa umeme kukatika kwako ni nusu saa. Yupo pale *Net Group,* sisi tukaambiwa tunaletewa umeme kupitia Urambo na Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye *speech* hii ukurasa wa 7, *paragraph* ya 11 naomba ninukuu: "Hapo awali ilitarajiwa kuwa mradi wa kupeleka umeme Urambo na Kaliua ungehusisha mpango wa kupeleka umeme Kigoma. Hata hivyo, ili kutocheleweshaumeme wa Urambo na Kaliua imeonekana bora mradi mahsusi wa umeme wa Kigoma uandaliwe."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tumo kwenye maandalizi, tukisema barabara, maandalizi watu wa Kigoma, umeme, maandalizi, maji, maandalizi, mashine zinatoka Australia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miji mikuu ya Mikoa tumesema hapa Songea, Mtwara na Kigoma yenyewe haina umeme wa uhakika. Lakini faraja ipo kidogo kwa wenzetu wa Mtwara. Wameambiwa wameshawekewa jenereta megawati 1.8. Tunashukuru ndugu zetu wale na wa Songea wao wameambiwa wao wamo katika utaratibu na kwa kweli ni utaratibu unaotegemea nia iliyoonyeshwa na wahisani. Hatujaambiwa wahisani watatoa hela ngapi na kwa nini miundombinu muhimu kama umeme uwe kazi yake ni kungojea watu wa Sweden, nchi ya watu milioni 7. Sisi tunakusanya mapesa chungu mzima hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Charles Kagonji, ametoka kusema sasa hivi hapa, kuwa gharama watu wanalipa. Mimi mwenyewe nina nyumba mbili nataka ziunganishiwe umeme. Moja nguzo mbili hapa Dodoma milioni moja na laki mbili na

nyingine nguzo mbili Kigoma Mjini milioni moja na laki sita. Lakini tunapotaka kuweka umeme tunangoja Sweden wao wameonyesha nia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme hapa kwamba mnatufikisha mbali katika nchi hii. Maana inaonekana ni dhahiri kabisa kuna raia *first class* Tanzania na raia *second class* na Kigoma ndiyo raia *second class,* hawana chochote katika Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu sijui wanatuonaje? Sijui! Sijui tuliwakosea nini Serikali?

Mimi ningependa kwanza Serikali ituambie kwamba kule Kigoma tulichowakosea nini? Lazima turekebishe mtusaidie, maana yake haiwezekani. Wabunge juzi hapa wametoka kwenye Kamati wanasema wamelala siku tano bila umeme Kigoma Mjini achilia mbali ndugu zangu wa Wilaya ya Kasulu, wala katika kitabu hiki haitajwi kwamba na yenyewe ni Wilaya inayofikiriwa wala Kibondo hawatajwi kabisa, inatajwa Rufiji, wapi wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi sio Watanzania, tuambiwe hapa, zamani alikuja Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, pale *stadium* na mimi nikiwepo na Mkuu wa Mkoa alikuwa Ndugu Semvua. Wazee wakamwambia, Mwalimu tuambie sisi ni watu wa Kongo au wa hapa, tuachane. Maana yake ni vurugu sasa. Sisi tunakaa katika nchi mpaka mwaka 2004 watoto wetu hawajui kompyuta, hawana umeme, hawana chochote ili keshokutwa waje kuwa watumishi wa Watanzania wengine si ndio maana yake? Sisi tubebe mizigo. Lakini hii pesa ni ya kwetu wote. Sisi wengine tunahangaika tunakwenda mpaka Burundi, Burundi wanasema, wako tayari kuunga, tunaambiwa kuna vita kule. Tanzania tumefanya kazi ya kusuluhisha vita Burundi, tunawaambia hata waasi wasipopenda, wakipenda, washiriki kwenye Serikali.

Sasa huo woga wa vita ni upi na umeme ukitokea kule Burundi, umeme huo utaanzia Wilaya ya Kasulu na Kibondo kwa mpigo na ufike Kigoma kilometa 40. Tunaambiwa Burundi bwana kuna vita kule. Wana umeme mdogo sana, lakini Kagera wameungiwa umeme wa Uganda megawati 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi mnatufanya nani? Mnatufanya nani sisi bwana? Kwanza sisi tunawasaidia kama ni hiyo CCM. Mkitaka kushinda kule, mkiwawekea watu wa Kigoma umeme, hata mimi mtaniondoa Ubunge wangu. Kwa sababu mmefanya kazi ya kuwafurahisha watu wa pale. Lakini kwa hali hii hata mtu awe na ndoto za namna gani, mnawaudhi watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli jambo hili linanitia uchungu sana. Basi angalau na sisi tungekuwa kama Ruvuma, tungepelekewa hata kabarabara kamoja ka lami. Tungesema jamani labda na mengine yanakuja. Lakini hakuna barabara, maji, umeme. Ni ahadi tu, kuna jenereta zinatoka India bwana.

Sasa tumechoka, mimi napenda na najua, tumechoka na sisi. Tumeanza kuwa hata na mawazo kwamba isije kuwa wenzetu wa Mikoa hii ndiyo wenye viwanda na umeme wanaona woga na sisi Kigoma tukipata umeme wa uhakika si ajabu wawekezaji wengi wakaja pale na nani asiyejua kwamba viwanda vya Tanzania vingi tegemeo lao kubwa ni masoko ya *Eastern Congo,* Burundi na kwingineko. Sisi hapa tumeshatekwa nyara na viwanda vya Kenya. *Colgate* nzuri inatoka Kenya, siagi nzuri inatoka Kenya. Sasa viwanda vya Morogoro na Tanga vitauza wapi kama siyo kule. Kwa hiyo, wanaogopa. Umeme ukija kwetu sisi tutapata mashine tutatengeneza vitu viuzwe kwenye soko halali la Tanzania. Wao watu wakubwa wenye nchi hii watakosa ajira. Watu wa Kigoma kukosa ajira ni jambo la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule peleka tu misako ya Polisi, singizia tu kila mtu si raia. Nenda Umasaini huko, kuna Mmasai wa Kenya na Tanzania. Nenda huko kwingine kuna Mfipa wa Zambia na Watanzania. Nenda Uhayani, kuna Wahaya wa Tanzania na wa Uganda. Hakuna matatizo. Matatizo ni Kigoma na misako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kweli tunaona ni jambo gumu sana na tungependa ieleweke. Mimi nimekwenda Burundi, nimekwenda Kongo. Nimezungumza na watu wa Serikali kule. Wanasema sisi tuko tayari. Tulipokuja hapa Bungeni, tunauliza jamani mbona hamtuwekei umeme kutoka Kabimba mpaka Kigoma ni kilometa 45 *nautical miles* tuwekeeni basi waya mmoja kutoka Kongo ushuke utokee pale Kigoma tupate umeme wa uhakika. Tunaambiwa hapana bwana, pale pana kina kirefu sana, kushinda Bahari ya Hindi tulikopeleka umeme mpaka Zanzibar? Inashindwa kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukamwuliza Mheshimiwa Waziri hapa, umefanya utafiti. Sasa aah, sijafanya, akasema ameshakufa yule bwana, maskini ya Mungu tumwombee, Mheshimiwa alishafariki. Anasema hawakufanya utafiti, ila anajua ni bei kubwa sana. Sasa pale Kigoma kuna wakazi milioni 1.7 wanafanya kazi, hatujapewa chakula cha njaa sisi tangu Uhuru wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka tuna ziada ya chakula tani 600 na watu wanakufa njaa kwingineko. Tunaambiwa hakuna uzalishaji. Uzalishaji gani sasa? Sisi tunasema jamani msituanzishie siasa za chuki. Kongo wanazalisha umeme megawati 3,500, ndiyo nchi ya kwanza, hakuna *South Africa* wala nini na wanauza Afrika nzima, Kongo wako *SADC,* tumekwishatiliana mikataba sisi nchi zote za *SADC* ku-*share* umeme. Tunaambiwa kuna vita kule, mbona umeme haukatiki Kongo unakatika Dodoma siku za Bunge hapa hapa unakatika tunaona. Mbona umeme haukatiki Bujumbura, mimi nakwenda kila siku kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza na watu kule. Wanatuonea imani na wao wameshaingia sasa, wanataka kuingia *East African Community.* Hiyo vita mnayokataa ya kuleta umeme kutoka Burundi kuja Kigoma wakati huo huo mmewakubalia Burundi waingie kwenye *East African Community* sasa sijui na Rais wa Burundi atakuwa anapigana na ma-Rais wetu kwenye mikutano, hatuelewi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nisingependa kusema mengi. Mimi ningeshauri iundwe Bodi kwanza ya umeme mijini. Ni aibu mnapojitia ninyi ni mji na mji hauna umeme, ni aibu. Hakuna, dunia nzima mji wa namna hiyo usiokuwa na umeme, Mji wa Kigoma - Ujiji. Ujiji ndiyo iliyokuwa kijiji kikubwa cha kwanza Afrika nzima siku tunapata Uhuru hapa, cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unamwambia peleka umeme vijijini bwana. Ndiyo kijiji kikubwa Afrika nzima, Ujiji. Nani asiyejua hii? Mji wa tangu mwaka 1,500. Hapana hii Dar es Salaam ya mwaka 1,860. Lakini sisi tunaachwa nyuma, tunaonewa na sisi tunasema jamani, tuwe waangalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ambalo mimi ningependa nisemee, juzi juzi hapa tuliona kwenye ripoti za magazeti kwamba Kigoma wamegundua madini ya *Coltan* ndiyo madini yanayotengeneza simu za mikononi. Ni madini ambayo nadhani sasa hivi yanashinda thamani ya Almasi kwa sababu hivi ni vitu *industrial* zinatumika kila siku na sote tunanunua simu hizi na dunia nzima inazitaka.

Mimi ningependa Wizara hii iangalie kwa haraka sana uwezekano wa kuanza kuya-*exploit* madini hayo kwa sababu haya madini yako Kongo tu na Australia na inawezekana kesho, keshokutwa, yakagunduliwa madini ya aina nyingine yanaweza kuchukua nafasi hii na sisi tukawa tumekosa chakula ambacho kwa kweli ni kuweza kuyachukua kutoka Kigoma na kuyauza katika soko la ulimwengu. Ni madini mazuri kilo moja ni dola 400, sidhani, kama kuna madini mengine yanashindana na haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi baada ya kusema hivyo, napenda dhana nzima ya Kigoma kuwa *second class* ifutwe na sisi tupewe haki yetu. Nakushukuru tena Mheshimiwa Naibu Spika na ninakataa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niungane na wenzangu katika kuchangia hoja ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na Taarifa nzuri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Taarifa ni nzuri yenye matumaini ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Ninachosisitiza ni usimamizi na ufuatailiaji, ni kitu ambacho kinakosekana. Ni dhana ambayo tunaipoteza. Kwa hiyo, narudia kusisitiza kwamba ili mipango iende sambamba ni budi wajipange, wafanye ufuatiliaji, kusimamia na kuona malengo yanatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, nataka nimweleze kwamba matatizo ya kukosa umeme Kigoma siyo CCM, ni matatizo ya nchi. Kwa hiyo, naomba aelewe hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa jinsi alivyomsaidia Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa homa

ambayo alikuwa anaumwa kuweza kupata nafuu. Sasa tunazidi kumwombea amtie nguvu, ili aweze kuendelea na shughuli za ujenzi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo langu ninakotoka ambako walipata ajali, walifariki watu 12 sehemu ya Nangoo na bado kuna wengine majeruhi wamelazwa Hospitali ya Ndanda. Waliofariki namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema na wagonjwa Mwenyezi Mungu awajalie waweze kupona haraka na wale wanaowauguza wawe na imani kwamba Mungu atawasaidia kupata nafuu ili na wao waendelee na ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ndicho kitu kilichonifanya nisimame kutoa shukrani zangu kwa Waziri Mheshimiwa Daniel Yona. Mwaka 2003 wakati nachangia Bajeti, nililalamika kuhusu umeme katika mji wa Mtwara. Namshukuru aliniandikia kwa kunifariji kwamba matatizo yatakwisha. Mimi nimekitunza na ni kweli ni makini kwa sababu wengine wanaweza wasikuandikie na wengine wanaweza wakasahau kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yeye amekumbuka ahadi yake na nataka niseme kwamba umeme tumeupata namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote. Mtwara sasa hivi umeme unawaka na ni shukrani kwa wanawake wa Mtwara kwa sababu wanaweza wakafanya biashara ndogo ndogo jioni kama kuuza *ice cream* na kuchangamka. Kwa hiyo, nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Mtwara ilikuwa ngumu, hata kwa watumishi walikuwa saa nyingine wanakimbia. Wakitembea sokoni wanazomewa, wakitembea mitaani wanazomewa, haoo, haoo, kwa sababu ya nini, kwa sababu umeme ulikuwa haupatikani na unakatika kila mara. Lakini walikuwa na moyo walishirikiana na Meneja wao yule wa Mkoa hawakukata tamaa wakati mafundi wanajaribu kurekebisha, jioni umeme umekatika. Lakini mimi nataka niwapongeze kwa kazi ile ya kujipa uhodari wa kazi na kwamba sasa hivi hawazomewi, wanatembea kifua mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba iendelee na taratibu hizo ikiongozwa na Waziri wetu Mheshimiwa Daniel Yona na safu nzima. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani zangu ziko, matatizo hayakosekani katika maeneo mengine na nalazimika kuzizungumza kwa sababu kati ya miundombinu nyeti ni pamoja na umeme. Umeme kama unakosekana kwa hiyo maeneo hayo maendeleo yatakuwa hayapatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara Vijijini juzi niliuliza swali hapa Bungeni, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, alinijibu vizuri akasema kwamba Nanyamba watapata umeme. Hilo ni tatizo la Serikali. Sasa lini? Kwa sababu haya ni maneno ambayo siku zote yamekuwa yanazungumzwa na kile ni kijiji cha zamani. Tangu Uhuru ulipopatikana mpaka sasa hivi haujapatikana umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni maelezo mazuri yenye matumaini na yenye kufurahisha. Sasa tunataka maneno hayo yaishe na Nanyamba wapate umeme tena ikiwezekana haraka iwezekanavyo. Kwa sababu wana vituo nyeti, pale kuna Kituo cha Polisi, kuna Hospitali ambayo watu wanaitegemea na kuna shule ya Sekondari ambayo watu wanaitegemea. Sasa hilo nilitaka niseme kwamba Bajeti ndiyo hii leo tunaipitisha. Fanyeni kila linalowezekana Nanyamba wapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na kwa mifano iliyo hai, wiki iliyopita niliuliza swali kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, kuhusu sekondari zilizoko ndani ya Mkoa wa Mtwara ambazo hazina umeme. Nataka nirudie na sisemi kwa furaha, nasema kwa uchungu kabisa kwamba hivi Sekondari ambazo zinatumia vibatari, Sekondari inatumia kandiri, sekondari zingine pengine hutumia kuni. Unafungaje *Internet?* Ataniambia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sisi tumeshindwa maana tunasikia sasa hata shule za msingi wanatumia *Internet.* Sekondari wanatumia *Internet* na isitoshe hapa hapa tukajifunza Tovuti. Sasa hebu niambie hawa watu ambao hawajaona mahali pa kufunga *Internet* anafanyaje ili na yeye aende na wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hiyo sikati tamaa kwa sababu leo si atahitimisha? Atahitimisha taarifa zake, atakapokuwa anahitimisha basi nipate majibu tunafungaje *Internet* ili hao watoto wanaosoma na wenyewe waende kwa wakati? Tunataka watoto wa Shule za Sekondari na wenyewe watumie umeme. Shule ya Sekondari ipo, pamoja na hiyo niliyoitaja ya Nanyamba, iko Shule ya Sekondari Kitangari, iko Shule ya Mnyambe, ipo shule ya hapo Nanyamba na zingine zote hazina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nikisema nitakuwa labda Mheshimiwa Naibu Waziri ananiangalia hanielewi. Lakini ninachosema katika sehemu ambazo watoto wetu wanasoma wanaachana mno. Kuna *gap* kubwa kutoka katika Mkoa wa Mtwara aje amfikie mwanafunzi anayesoma Dar es Salaam, anayesoma Arusha, anayesoma Moshi. Siyo rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa nilikuwa naangalia *television* nimeona kuna kipindi cha watoto wanashika *microphone,* hebu fikiria kweli mtoto wangu mimi wa kule kijijini ninakotoka ukimpa *microphone* sasa ataweza kuishika kweli, si ataogopa. Lakini mtandao ndiyo unaomnyima yeye na kubaki amedumaa. Mtandao ndiyo unamnyima yeye asiende na wenzake na wakati. Kwa hiyo, hili suala si la mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Yona, wewe ni msikivu, nimekwishakusifia kule nyuma na nadhani umenisikia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wawekezaji ni tatizo nyeti katika Mkoa wa Mtwara na nadhani hatuna wawekezaji na katika maswali, mlolongo niliokuwa nauliza majibu yanayotokea yanasema kwa sababu ya miundombinu na sababu nyingine anasema

wawekezaji wana hiari ya kuchagua. Mimi hapo ndiyo wananichanganya kabisa sielewi kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ikiwa Serikali yetu hii iliyopewa dhamana ya nchi, dhamana ya kusimamia mipango inamkubali huyo mwekezaji eti aridhike yeye aende wapi? Basi aende Mtwara, tutamwonyesha kuni zinapatikana wapi. Maana ndiyo hiyo hali iliyofikia sasa hivi. Sasa kama umeme upo ndiyo kipindi ambacho wawekezaji wanakuja sasa hawaji kwa sababu ya hiyo ili na sisi twende na wakati hilo ni suala lenyewe ambalo nalikabidhi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba hakikisha umeme unakuwa wa kutosha na maeneo mengine ili wawekezaji waje na wawekezaji wanapokuwepo maendeleo yatapatikana kwa vijana wetu ambao sasa hivi tunaambiwa vijana wa Mtwara wanakimbia kuja Dar es Salaam. Watakimbia kwa sababu hali siyo nzuri imedumaa, Dar es Salaam anajiona na yeye anaungana na wenzake anakwenda na wakati.

Kwa hiyo, hakikisha wawekezaji wanakuwepo, akinamama na wenyewe waendeshe miradi au akinamama waungane na wenzao katika sehemu ya uwekezaji kupata ajira. Sasa hivi hakuna ajira na kuna mengi ambayo yanahusu katika Wizara yaani matatizo yamewazunguka, wanayavaa kama nguo. Sasa tunaomba Wizara hii itutatulie matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri kuhusu suala la umeme. Barabara kwa mfano kutoka Masasi mpaka Tandahimba walikofunga umeme ambako nawashukuru kwa jitihada walioifanya, kuna vijiji ambavyo umeme wanauona unapita. Sasa kwa nini vituo vile vinavyopita umeme wasiwateremshie pale kwenye vijiji? Yeye anaangalia nyaya tu zinapita eti zinakwenda Makao Mkuu ya Wilaya. Kweli huu ni uungwana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme uteremshwe kwenye vijiji vile vikubwa, kwenye vituo vile na wenyewe wajisikie huru. Inawezekana kukawa madhara, mimi siombei. Lakini ni kwa sababu vijana wataona uchungu kwa nini umeme sisi hatuupati? Unapita tu wanaangalia tu nyaya huko juu na kwa bahati nzuri *Celtel* imeweka milingoti na kila penye mlingoti wamejitahidi kutelemsha jenereta. Kwa mfano, kama Kijiji cha Nambunga, Mtimbwilimbwi, na niishauri Wizara muongee nao ikiwezekana sehemu zile zenye hii minara ya *Celtel* au *Vodacom* ikiwezekana kama ni ndugu zetu ambao wako katika nchi hii ya Tanzania wawasaidie wananchi wale walioko karibu angalau na wenyewe wapate umeme, kuliko sasa hivi vijiji utakuta chote ni giza hakuna umeme, lakini inawaka pale penye kituo cha Posta na ndiyo mnara uko pale hilo jambo ambalo nashauri na nina hakika Serikali yetu ilivyo sikivu na askari wa miamvuli tunao wazuri, mnaweza kabisa hili mkalitekeleza na sisi tukajisikia tunaporudi kwamba tulizungumza Bungeni, leo linatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba niunge mkono Bajeti hii kama nilivyosema kule mwanzo kwamba nia ilikuwa kuishukuru Serikali kwa jinsi ilivyotuletea umeme na kupeleka kilio kwa maeneo mengine kwamba watusaidie umeme

kwa yale maeneo mengine ambayo umeme haujafika. Naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea machache jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki zangu wasiwe na wasiwasi kwa hotuba yao hii au kwa hoja yao waliyoitoa kwani ni hoja nzuri na inaelekeza nchi yetu tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzangu, jirani yangu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na pole kwa Waheshimiwa Wabunge wengine ambao walipata matatizo mbalimbali aidha, kwa kufiwa na watoto wao au kupata ajali mbalimbali na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaleta maendeleo, umeme unazuia vijana kwenda mjini kwa wingi kwa sababu wangeweza kukaa kule vijijini kama umeme ungekuwepo. Lakini hali ya maeneo mengi nchini ambayo yako pembezoni na mengineyo umeme unakopita bado wanahitaji nishati hii ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado napata matatizo kujua kama kwa kweli hawa *NetGroup Solution* walipopewa madaraka walipewa maeneo haya madogo madogo ambayo yalikuwa na *on going projects* wamefanya nini mpaka sasa? Inawezekana tukawalaumu hapa kumbe wenyewe wameingilia kukusanya pesa nyingi tu pale Dar es Salaam na maeneo mengine wakasahau zile *projects* zilizokuwa zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu eneo langu ni mojawapo ambalo limepata nguzo mwaka 2000 na nilitegemea kufikia, sasa ningekuwa nimepata umeme lakini mpaka sasa umeme haujafika. Ndio maana nasema pengine malengo ya hawa wenzetu tuliofikiria wangeweza kuboresha *TANESCO* hawakupewa tangu mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi wanazozifanya pamoja na *management* ya Mkoa wa Mbeya kwa kusambaza umeme katika Mkoa wa Mbeya. Pamoja na kwamba yako maeneo ambayo bado hayajafikiwa pengine ni kwa sababu kama nilivyosema hapo mwanzo *connection* ya wale viongozi hawajajua maeneo haya nayo yalitakiwa yafikiwe na yapate umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi Mbunge mwenzangu wa Lupa, Mheshimiwa Njelu Kasaka, ameongelea juu ya upelekaji wa umeme kule Lupa. Pia ameongelea juu ya upelekaji umeme kule Jimboni kwangu katika eneo la Kanga na natarajia kwenye majumuisho Mheshimiwa Waziri atatueleza kama maeneo haya yatapatiwa umeme kwa sababu yeye mwenyewe alitoa ahadi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na hiyo kwa siku chache hizi amekuwa akifuatilia sana suala hili la kuhakikisha kuwa umeme unafika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo kwa mfano ya Lupa kuna migodi midogo midogo na kuna Shule ya Sekondari na vitu vingine ambavyo kwa kweli ingefaa watu wapate umeme. Haya maeneo ya Kanga kuna shule na vitu vingine ambavyo kwa hivi sasa ilipaswa wapatiwe umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kuzungumzia ni maeneo yaliyochukuliwa na wenzetu katika sehemu mbalimbali ambapo bado hawajaanza kuchimba madini. Mwaka 2003 katika hotuba yangu nililizungumzia, lakini narudia tena kuwa yapo maeneo watu wamezuia na pengine sheria zinawaruhusu lakini hawajaanza kuchimba madini na Mheshimiwa Waziri alisema wangeweza kutunga sheria ya kuhakikisha maeneo haya yanaachiwa na watu wengine wakachimba madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lipo Shirika la *STAMICO* ingawa limeelezwa kwenye kitabu hiki vizuri zaidi kuwa linaendelea, mwaka 2003 alituambia lingeweza kufufuliwa, nalo lina maeneo kwa mfano kule Chunya ambapo limezuia wananchi ambao wangeweza kuendelea kuchimba madini pale.

Naiomba Serikali yale maeneo ambayo yamebanwa bado na wenzetu ambao hawawezi kuyahudumia wananchi wengine wangepewa ili waweze kuendeleza familia zao kwa kuchimba madini yale na kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kama wenzangu walivyosema kwamba kuna nyaya zinapita mahali pengine na vijiji havipati umeme kwa mfano Matundasi, Patamela kule Jimboni kwangu na hata mahali pengine kwa mfano kijiji cha Kapeta kule Ileje wanalalamika umeme umeanzia pale kwenye machimbo ya makaa na hakuna umeme. Hili ni jambo ambalo nasema pengine wakati wa kupewa haya maeneo wenzetu hawakuelezwa wafanye kitu gani. Naiomba Serikali kwa Bajeti hii, Waziri anatusikiliza waweze kuwapa programu nzuri zaidi ili maeneo kama haya yanayolaumiwa yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu gharama za umeme. Gharama za umeme zimepanda sana na mfanyakazi wa kawaida au mtu anayeanza kazi ni vigumu sana kuzimudu. *Sometimes* imefikia mpaka mtu wa kawaida analipa shilingi 40,000/= ambayo ni kama kima cha chini cha mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia gharama hizi za umeme zimepanda toka *service line* shilingi 90,000/= mpaka karibu shilingi 200,000/=.

**MBUNGE FULANI:** Duh!

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ongezeko kubwa sana wanasema *service line* ni shilingi 140,000, *VAT* ni shilingi 28,000, *deposit* ni shilingi 30,000 pamoja na kupandishwa kwa bei za nguzo. Nasema sijui wale wananchi kule vijijini ambao wangependa kuweka umeme kama gharama hizi wataziweza. Gharama ni

kubwa na afadhali wale waliopata umeme mapema wamefaidika lakini hawa wa sasa hivi itakuwa ni ngumu sana kuweza kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla gharama za umeme zingeangaliwa upya na hasa *VAT*. Sioni kwa nini tuna-*charge VAT* kule vijijini ambako kwa hivi sasa tunapeleka umeme.

Naomba sana sisi tusiopata umeme au maeneo ambayo umeme haujafika gharama hizi ziangaliwe upya na ziboreshwe kulingana na gharama za sasa hivi ambazo zinapanda ili nalo shirika lisipate hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NetGroup Solution* imeelezewa kwenye kitabu hiki ukurasa wa 13, mkataba kati ya *NetGroup Solution* na *TANESCO* uliisha muda wake wa miaka miwili mwezi Aprili, 2004. Ili kutoa nafasi ya kuandaa mkataba mpya, *NetGroup Solution* imeongezwa kipindi cha miezi mitatu hadi mwezi Julai, 2004.

Aidha Serikali ya Sweden imekubali kuendelea kulipa *management fee* ya *NetGroup Solution* iwapo Serikali itaamua kuingia mkataba mpya. Mimi sina matatizo lakini kwa *trend* hii, kama tutaenda namna hii sioni haja ya kuendelea kuwa na *NetGroup Solution* na ningekuwa na uwezo ningeweza ku-*convince* Bunge tukakataa hii au nikaiomba Serikali kwa nguvu zote *NetGroup Solution* wasiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesema pengine ni kwa sababu hawakuainishiwa majukumu ambayo walipaswa wayafanye wamekabidhiwa tu, hawakujua zile *projects* ambazo zilikuwa zinaendelea, kweli hizi *projects* zina matatizo kwa wananchi wetu, wana-*query* sana kwa nini hazijamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuweka nguzo kwangu kule Wapinzani wameunguza nguzo 40, sasa sijui walikuwa wanaikomoa Serikali au wananikomoa mimi, lakini hii yote imesababishwa na tatizo la kukaa sana kwa mradi bila kumalizika.

Naiomba *TANESCO* ihakikishe mradi ule sasa nguzo zinasimamishwa toka Mwambani kama mwenzangu alivyosema asubuhi kwenda Mbala walipounguza nguzo zile chache kwenda Kanga na kufikia Galula kwa sababu kama alivyoeleza mwenyewe Waziri alisema tungeweza kupata umeme tangu mwaka jana lakini mpaka leo hii hali ni kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Serikali kupitia Shirika la *NDC* kuangalia tena upya madini ambayo yako katika Wilaya ile ya Chunya. Wilaya ile imekuwa na *potentials* tangu zamani ilikuwa ni *restricted area* ambapo wenzetu Wazungu walikaa kule. Siamini kuwa madini yamekwisha kabisa kule, yapo madini ya Chuma, Almasi, Dhahabu na vitu vingine.

Naomba sana Shirika hili kwa kushirikiana na Wizara liendeleze utafiti zaidi ili na sisi kule tuweze kupata mwekezaji mkubwa katika maeneo ya madini ya chuma ambayo

yapo au almasi. Zamani ilikuwa baada ya Mwadui ni *Ngwala Mines* kule sehemu za Gua ambapo ndio kulikuwa kunachimbwa madini haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia kwa nguvu sana kama nilivyosema mwanzo naiomba Serikali isione kuwa kuna sehemu ambayo umeme hautoi faida. Naomba Serikali iangalie maeneo yote kwa usawa uliokamilika na ijaribu kusambaza umeme sehemu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika unasema hakuna faida halafu sehemu nyingine nyaya zimepita juu, umepeleka sehemu nyingine umeme nyumba zenyewe au hali ya kupeleka umeme kule hairidhishi. Sasa tuleteeni umeme kwenye maeneo ambayo tunafikiria yanaweza kuboresha maisha ya wananchi na yanaweza kusukuma maendeleo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu amesema kule Kigoma kuna Ujiji, lakini hata sisi Wilaya zetu ni za siku nyingi tumepata umeme juzi, asiwe na wasiwasi CCM ni Chama madhubuti, kitapeleka umeme kule Kigoma na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda baadaye kupata majibu kwa haya niliyosema juu ya upelekaji wa umeme Lupa na Kanga na hasa upatikanaji wa umeme pale Kapeta katika Jimbo la Ileje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kuchangia kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba sina matatizo na Bajeti yake na hasa ukizingatia kwamba Kamati yetu ndio tulikaa nao na tukaipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, naomba nizungumzie suala la utunzaji wa mazingira kutokana na uchimbaji wa madini. Wizara ya Nishati na Madini ina wataalam au Maafisa Madini ambao wamesambazwa Kikanda au Kimkoa. Katika Ibara ya 82, Wizara imezungumzia suala la utunzaji wa mazingira. Lakini naona kama vile Wizara bado haijalishughulikia kikamilifu hasa kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo ambao wengi wanapochimba hawafukii yale mashimo ambayo wamechimba. Kwa hiyo, mazingira yanaharibika kama miti ilikatwa inakuwa imeshapotea lakini vile vile vile ile ardhi huwezi kuitumia kwa matumizi mengine kwa sababu inakuwa imejaa mashimo ambapo mengi yanaleta hatari.

Namwomba Mheshimiwa Waziri awasimamie Maafisa wake walioko Mikoani katika Kanda, wahakikishe kila mahali ambapo kuna machimbo basi baada ya kuchimba hawa wachimbaji wanafukia mashimo hayo ili tuweze kuipata ardhi hiyo kwa ajili ya matumizi mengine kama vile kilimo na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, naomba nizungumzie bei za nishati kwa maana ya umeme pamoja na mafuta. Leo hii katika nchi yetu na Waheshimiwa Wabunge wamedhihirisha katika hili Bunge lako Tukufu, wengi wamezungumzia juu ya suala la umeme kupanda bei, wamezungumzia suala la mafuta kupata bei. Sababu zinatolewa nyingi tu kwamba vita vya Iraq, China wanatumia sana mafuta wamepandisha bei na katika suala la umeme tumeambiwa kwamba kuna gharama na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Wizara imezungumzia juu ya hawa watu wa *NetGroup Solution* kwamba baada ya kupewa mkataba wa kazi wameonyesha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, wamezungumzia juu ya upunguzaji wa upotevu wa umeme. Kweli tunakubaliana lakini wananchi wengi walichokuwa wanakitegemea kama hawa watu wakiweza kuingiza ufanisi katika shirika hili ni bei ya umeme angalau ingeshuka lakini haijashuka. Hapo kwa kweli huu ufanisi kidogo tunaweza kuutilia mashaka. Nafikiri huu ufanisi ili uweze kuonekana kwa wananchi hasa watumiaji wa umeme ni pale bei ya umeme itakapokuwa imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi umeme umepanda bei hasa kwa watumiaji wadogo na leo Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba sababu ya kupandisha umeme ni kwamba wenye viwanda wamepata nafuu ili waweze kushindanisha bidhaa zao katika soko la utandawazi au huria kwa sababu umeme ulipokuwa na bei kubwa ulikuwa unafanya bidhaa zao ziwe juu, kweli. Lakini kama hawa wafanyabiashara tumeweza kuwafikiria kwa hilo ili waweze kuuza katika masoko hayo ambayo wanakusudia kuuza hizo bidhaa zao, kweli ni jambo zuri, linasaidia kuleta mapato ya nchi na kuingiza fedha za kigeni lakini vile vile na watumiaji wadogo na wao wangefikiriwa kwa mtazamo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Kagonji, amezungumza vizuri sana na nampongeza kwa hoja zake na Mheshimiwa Paul Ntwina, vile vile amezungumza vizuri, sehemu nyingi vijijini wanaotaka kupatiwa umeme kati ya mambo wanayolalamikia ni pamoja na gharama za uunganishaji *(service line)* zimekuwa kubwa mno kwa sababu wanaambiwa wanunue au wagharamie nguzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipato cha Mtanzania tunaambiwa shilingi ngapi kwa mwaka, ni dola 200. Sio ndio Mheshimiwa? Nafikiri ni kama dola 210 ambazo ni sawasawa na shilingi 210,000/= halafu huyu mtu unamwambia agharamie nguzo ya shilingi 500,000/= ataweza kweli? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawezi.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Sasa hapo naomba hawa watu wa vijijini na wao watizamwe kwa mtazamo wao maalum. Wabunge kweli tunawapigania wananchi

wapate umeme lakini vile vile jamani lazima tuelewe kwamba umeme ni maendeleo, mahali ambapo umeme umefika huwa unazalisha ajira katika maeneo yale. Mahali popote umeme ukishafika watu wanapata hata uwezo wa kubuni shughuli za kufanya na wanafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Shirika letu lifikirie uwezekano wa kutoa hizi nguzo kwa wananchi hasa vijijini ipeleke tu kama mradi. Naamini hata humu mijini ambako wengi tunaishi na wao wangetakiwa wagharamie nguzo kwa shilingi 500,000/= wengi wangeendelea kuishi na vibatari au na kandili. Naomba Wizara yetu ya Nishati na Madini iangalie uwezekano wa kupunguza au kuondoa kabisa hizi gharama za nguzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze na kuishukuru Wizara kwa kuamua kuendeleza ule mradi wa Mchuchuma. Kuendeleza mradi wa Mchuchuma kwa kweli kutasaidia nchi hii kuwa na chanzo cha umeme wa kuaminika na inawezekana kabisa watu wengi wakaweza kupata umeme hasa katika maeneo ya Kusini ambapo wenzetu kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali wa kusema kwamba wanakubali mwekezaji aiuzie *TANESCO* umeme kiasi kile ambacho *TANESCO* watakuwa wanahitaji na kingine wauze mahali popote ambapo wanataka na wamesema kwamba wako tayari kutafuta masoko wao wenyewe, huu ndio mtazamo wa kibiashara. Nawapongeza sana hawa wawekezaji na naomba Serikali iwaunge mkono ili wafanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine labda Serikali itusaidie kutupa maelezo katika kubinafsisha Shirika la *TANESCO* tunaambiwa litagawanywa liwe katika sehemu tatu, moja ya uzalishaji, nyingine ya usafirishaji na nyingine ya usambazaji.

Mimi ninavyoliangalia hili kama leo tunalalamika bei ya umeme imepanda, bei ya kuunganisha imepanda na tunaambiwa bei ya nguzo iko juu, hivi tutakapokuwa tumeligawanya hili Shirika katika vitengo hivi vitatu hivi hatuongezi *cost centers* ambazo nazo itabiti ziwe *reflected* katika bei ya mtumiaji wa umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wawekezaji wa Mchuchuma watakapokuwa wameanzisha huu mradi wao kama utafanikiwa utasaidia kuleta ushindani kati ya *TANESCO* na wao. Siamini kama hawa watu watakaowekeza katika mradi wa Mchuchuma watakuwa na mfumo kama huu wa *TANESCO* wa *production, transmission and distribution.* Hawa hawataweka huo utaratibu wao ina maana kwamba umeme wao utakuwa na uwezekano wa kuwa na bei ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo ya kama Kusini kwa yale ambayo yatakuwa karibu karibu kwa wale wanaopata umeme wa *TANESCO* na wale wanaopata umeme wa hawa wawekezaji wa Mchuchuma kama wa Mchuchuma utakuwa chini basi watakuwa na uwezo wa kubadilisha wachukue umeme kutoka kwa nani. Lakini sasa katika kuwekeza katika umeme, miundombinu yake ni tofauti husafirishi umeme na

malori au na treni kusema kwamba hii *means* ya usafiri hii ni ngumu basi nitabadilisha hii, unakuwa na nguzo ambazo zimeshajengwa toka zamani.

Kwa hiyo, tunaweza kuwa na ukanda wenye umeme bei yake ghali na kanda nyingine umeme wake uko chini. Naomba hili labda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* ajaribu kutuambia katika kuligawanya shirika hili wakati wa kubinafsisha hivi halitazidi kuongeza bei kubwa za umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba katika ule Mfuko wa Uendelezaji Umeme Vijijini, Wizara ijaribu kuharakisha upelekaji wa huo umeme vijijini kwa sababu huko ndiko kuliko na wananchi wengi zaidi. Ile dhana ya kusema kwamba tunapozalisha mazao yetu tujaribu kuyasindika ili yaweze kupata bei kama hatuwezi kufikisha huo umeme vijijini suala la kubadilisha haya mazao yaweze kupata bei nzuri halitaweza kutokea.

Kwa hiyo, naomba Wizara huu Mfuko wa Uendelezaji Umeme Vijijini kwa kweli ushughulikiwe haraka sana ili hawa wananchi na wenyewe waweze kupata umeme na kufanya shughuli zao kama wengine wanavyofanya hasa katika maeneo ya mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la bei ya umeme na kile chombo cha *EWURA,* kwa kweli tunaomba kianzishwe upesi kwa sababu kitasaidia katika kulinda maslahi ya walaji wadogo wadogo vinginevyo tutakuwa tunaacha upande mmoja unapanga bei kadri unavyotaka na kutakuwa hakuna usimamizi kwa upande wa walaji watakuwa hawana mtetezi. Kuanzishwa kwa chombo hiki kitasaidia hawa watumiaji wa umeme kuwa na mtetezi katika upande wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. LAWRANCE M. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa wale wote ambao walinipa pole kwa kifo cha binti yangu Victoria Gama, ambaye alikuwa ni *Regional Local Government Officer* wa Iringa tarehe 26 Juni, 2004. Hapa naishukuru sana Serikali na Rais wetu kwa shughuli na vitendo vyote vilivyosaidia katika kumzika binti yangu huko Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana viongozi na wananchi wa Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Meja Jenerali Mstaafu James Luhanga katika mazishi haya ambayo Wakuu wote wa Wilaya walishiriki na viongozi wengi tu walishiriki kwa michango na rambirambi, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa nyumba hii kwa rambirambi walizozitoa, kwa michango waliyotoa na kwa kadi mbalimbali za pole walizoniletea mimi mwenyewe. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma kwa jinsi walivyonipa pole na kuja nyumbani kwangu na kunipa *encouragement* ili niweze kuwa na nguvu zaidi. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kurudi kwenye *agenda.* Mwaka 2000 wakati Rais anachagua *cabinet* alisema kwamba hii *cabinet* yangu ni askari wa mianvuli. Kwa wanajeshi, askari wa mwamvuli maana yake akishadondoshwa tu basi kazi zinaanza pale pale na ni balaa tupu. Sasa ni miaka mitano imepita nafikiri tumeweza kuona kazi za wenzetu hawa na mimi naweza kusema kwa kweli kwa wale wote ninaowafahamu na nimeona vitendo vyao wamethibitisha kwamba ni askari wa miamvuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napenda nimtaje Mheshimiwa Basil Mramba, huyu ameleta mabadiliko makubwa sana ya kilimo katika Mikoa ya Kanda ya Juu Kusini na Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula, ambapo wote kwa pamoja wameleta mabadiliko makubwa sana ya kilimo ambayo hayajapata kutokea kwa miaka 20 iliyopita. Haidhuru hatujaridhika sana lakini hatua hizi zimeweza kusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kutuwekea soko lililoungua moto pale Songea, sasa tuna soko la Kimataifa. Huo ndio uaskari wa mwanvuli ninaosema mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Edward Lowassa, namshukuru sana kwa sababu kwa miaka 20 tumejaribu kutafuta maji Mkoa wa Ruvuma au hata pale Songea Mjini hatukupata, lakini nafikiri sasa hivi mradi ule unakwenda vizuri chini ya usimamizi wake na nasema ahsante sana.

Napenda sasa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Katibu Mkuu wake Ndugu Patrick Rutabanzibwa na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi nzuri kwanza kwa kutuandalia hotuba hii nzuri sana ambayo ina mwelekeo, malengo na inatoa matumaini kwa sisi wananchi wa Tanzania huko tuendako.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni kigezo kikubwa sana cha maendeleo. Unapotaka kuzungumzia masuala ya maendeleo, kwa kilimo kigezo kikubwa ni Mbolea. Ukitaka kujua watu wanalima wewe uliza ni mbolea kiasi gani wanatumia, basi.

Hivyo hivyo kwa upande wa umeme, ukitaka kuona Mkoa au nchi inaendelea, ulizia ni kiasi gani cha umeme wanatumia. Ukitazama Mikoa yetu ya Ruvuma, Lindi na Mtwara tumekwama kimaendeleo. Ukichunguza kwa makini utakuta ni kwa sababu ya matatizo ya umeme katika Mikoa hiyo. Kwa hiyo, suala la umeme ni suala zito na ni zito kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi kwa kweli nisingependa kuzungumzia mambo ya Ruvuma pekee, lakini kwa leo naomba nizungumzie juu ya Ruvuma peke yake kwa sababu ya tatizo hili la umeme.

Mkoa wa Ruvuma kwa miaka mingi sana umekuwa na matatizo ya umeme. Sasa miaka mitatu iliyopita, Mkoa wa Ruvuma ulipata mradi wa *NAKATUTA Project* ambao tungeweza kupata *megawatt* 13 na zingeweza kutosheleza kwa miaka 50 inayokuja na Wajerumani walifanya utafiti na wenyewe walikubali kuufadhili mradi huu, lakini wakasema sisi tutaufadhili mradi huu ikiwa Serikali itatutafutia mtu mwingine wa kutusaidia. Ndio masharti yao waliyotoa na ule mradi uli-*cost* kama dola milioni 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana Serikali ilishindwa kutafuta *partner* wa pili wa kwenda na Mjerumani, *as a result* baada ya miaka miwili Mjerumani ali-*withdraw.* Kwa hiyo, ilibidi sasa tuanze upya kabisa na ndivyo sasa hivi tunahangaika na kuanza upya. Hili tatizo lilikwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukitazama Ilani ya Uchaguzi, Ibara ya 5(3), utaona inasisitiza kwamba ifikapo mwaka 2005, basi Makao Makuu ya Wilaya zote yawe yamepatiwa umeme. Kwa mfano, ukitazama Wilaya ya Mbinga, Namtumbo, Tunduru unaona kabisa mbele huoni, ni giza tu. Sasa unapofikia hali kama hii lazima mtu uwe na wasiwasi sana.

Sasa pengine ningenukuu kidogo hapa juu ya hotuba hii ya Waziri ukurasa wa saba inasema hivi, nanukuu: “Wakati Serikali ikitafuta namna ya kupeleka umeme wa uhakika Songea na Kigoma, jenereta mpya zitafungwa katika Miji hiyo.” Ikaishia pale haiendelei zaidi. Halafu *item 11* inasema hivi: “Kuhusu Mkoa wa Ruvuma tayari Mkataba umetiwa saini wa kujenga kituo Makambako cha kupunguza nguvu ya umeme kutoka kilovoti 220 hadi kilovoti 132 na kilovoti 33. Mradi huo unafadhiliwa na Serikali ya Sweden.” Anamaliza pale, anatuacha na maswali mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hapa rafiki yangu Mheshimiwa Daniel Yona kama anatupiga chenga hivi maana yake hatuambii waziwazi sasa anataka kufanya nini na mimi namwelewa sana yeye huwa ni mtu *straight to the point.*

Sasa mimi nafikiri hapa Mheshimiwa Waziri itabidi katika kujibu atueleze vizuri anataka tufanye nini au mradi ukoje na unakwenda wapi ili tuweze kuelewa. Ninachojua mimi ni kwamba umeme unaoshushwa Makambako unakwenda Njombe, huo wa gridi na huenda ukafika wakati wowote ule katika muda mfupi tu ujao. Sasa kama umeme huu unafika Njombe, kwa nini umeme ule usipelekwe mpaka Mbinga hadi Namtumbo kupitia Songea maana yake itakuwa ni rahisi na ni vizuri zaidi na kazi hiyo inaweza kufanyika kwa sababu utakuwa umeshafupisha urefu wa mradi huu. Utakuwa umeshafika Njombe tayari, sasa kutoka Njombe kwenda mpaka Songea kwa kunyooka moja kwa moja ni kilometa kama 100. Kwa hiyo, bei lazima itakuwa nafuu sana. Mheshimiwa Waziri mimi nina *interest* kubwa sana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tunduru, mimi nafikiri wenzetu wa Lindi na Mtwara wanapozungumzia mipango yao wasisahau Tunduru. Pale ni karibu zaidi kupeleka umeme Tunduru kuliko kuutoa Songea kwenda Tunduru. Sisi ni watu wamoja na mipango yetu lazima iwe pamoja, hakuna kutenganisha. Kwa hiyo, mimi nina mategemeo sana wenzetu mnapolisukuma suala hili basi mkumbuke kwamba na Tunduru imo. Sisi Tunduru hatutaiacha mbali, hapana, tutafanya kwa pamoja tu. Kwa hiyo, nilifikiri suala hili ni la muhimu sana kwa upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme ni kero kubwa sana hasa baada ya kukaa miaka 40 tangu tumepata Uhuru wetu na Mkoa ule wa Ruvuma kama unavyojua tunazalisha Kahawa tani 12,000 kila mwaka, tunazalisha Tumbaku tani 8,000 mpaka tani 9,000 kila mwaka na hiyo yote inataka umeme ili tuweze kufanya kazi yetu vizuri zaidi. Siyo hiyo tu tunazalisha chakula vizuri tu mpaka tukawahi kuitwa *big four. Big four* bila umeme, ni *big four* gani? Sasa ningeomba tafadhali sana katika suala hili la umeme tunaomba Mheshimiwa Waziri alisimamie. Naamini kabisa akiamua kulifanyia kazi na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, ni mtu *very active* na ni mfuatiliaji wa hali ya juu kabisa. Mimi naamini kabisa mwaka huu hadi kufika mwaka 2005 tutakuwa na umeme wa gridi katika Mkoa wetu wa Ruvuma na hapo sisi tutafurahi kwamba kwa kweli sasa tunakwenda pamoja, lakini sasa hivi hatuendi pamoja hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kusema kweli leo niliamua kusema haya ya umeme tu na ningemwomba kabisa Mheshimiwa Waziri wakati wa ku-*wind up* atuelekeze hapa hasa mpango ukoje wa kupeleka umeme huko Ruvuma. Sisi hatutaki kusambaza nguvu, sisi mipango yetu katika Mkoa wa Ruvuma ni kukusanya nguvu. Kusambaza nguvu maana yake nini? Kusambaza nguvu maana yake unazungumzia juu ya miradi mingi, mara huu, mara ule. Tunataka mradi huu wa gridi kutoka Njombe mpaka Songea, hilo tu tunalotaka sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa langu lilikuwa ni hilo tu, basi napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia na nategemea Mheshimiwa Waziri atatuelimisha zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuongea jioni hii. Naomba na mimi niungane na wenzangu kwa niaba ya wananchi, wapiga kura wa Jimbo la Kasulu Mashariki kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijiji, Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego na nawapa pole wapiga kura wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme machache kuhusu bei za mafuta. Hivi tunavyoongea bei ya lita ya dizeli Kasulu ni shilingi 1,200/=, bei ya lita ya petrol kama utaipata ni shilingi 1,700/=, mafuta ya taa lita moja ni shilingi 800/= mpaka shilingi 900/=. Sasa kutokana na bei hizo ni kwamba sisi Kasulu tunanunua mfuko wa saruji kwa shilingi 15,000/= ambapo Dar es Salaam ni shilingi 7,200 ikizidi sana ni shilingi 7,500/=. Gharama ya usafiri inatisha. Ukipanda basi kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam ambapo ni kilometa mia mbili unalipa shilingi 2,000/= tu na siku nyingine ukikuta

mabasi yameongezeka hata kwa shilingi 1,500/=. Lakini bei au nauli kutoka Makere mpaka Kasulu, kilometa hamsini tu ni shilingi 2,000/=.

Sasa mimi naomba kuiuliza Serikali, hivi inataka kukwepa wajibu wake wa kusimamia bei za mafuta? Huu ni wajibu ambao Serikali haiwezi kukwepa hata mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali inaweza kuhangaika tunapopata njaa kupata chakula na kuhakikisha bei za chakula hazipandi sana, mafuta nayo ni sehemu kubwa sana na ni msingi mkubwa sana kwenye uchumi wetu. Sasa Serikali inapoacha tu kwamba mafuta yatajipangia bei yake yenyewe, kwa kweli Serikali haiwatendei haki wananchi wake, haiwezekani kabisa. Kwa mfano, sisi tunaotoka Mikoa ya pembezoni tunaadhibiwa kwa vile tunatoka Kigoma kwamba Dodoma bei ya dizeli lita moja shilingi 800/=, mimi kwa vile nakaa Kasulu nilipe shilingi 1,200/=, yaani naadhibiwa kwa vile nakaa Kigoma au Kasulu.

Serikali inafanya nini kuhakikisha kwamba hata huko Kasulu wananchi wanatakiwa kuendesha maisha kama wale wa Dar es Salaam. Dar es Salaam watu wa daladala walivyojaribu kupandisha nauli mara moja Serikali ilisimamia, nauli haikuongezeka ikabaki shilingi 150/= kwa safari. Sisi Kasulu kila inavyowezekana tu bei inapanda na mambo yanakwenda. Hivi ina maana kwamba Kasulu sio sehemu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwauliza hawa wanaohusika, ina maana sisi tunaendelea kuadhibiwa tu kwa vile tumezaliwa Kasulu, basi tutaadhibiwa mpaka tunakufa, ndiyo sawa! Ndio sawa naiuliza Serikali?

**MBUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba kule Kigoma siyo sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Kama ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi Serikali inatakiwa ichukue hatua ihakikishe kwamba bei za mafuta Dar es Salaam na Kigoma zisitofautiane sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi *EWURA* iko wapi? Ni miaka miwili tangu ipitishwe hapa Bungeni Sheria ya *EWURA,* lakini mpaka leo hakuna *EWURA,* hivyo sisi tunaendelea kuumia. Mimi nadhani ni vema kabisa Serikali isikwepe wajibu wake wa kusimamia bei za mafuta. Kama inavyosimamia bei za vyakula na vitu vinginevyo ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu hauathiriki, Serikali lazima ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba bei za mafuta hazipandi kiholela na hasa katika Mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaongelea juu ya mradi wa majaribio ya nishati ya jua Vijijini. Hongera sana kwa mradi huu, lakini sasa nashangaa, mradi huu eti unaanzia Mwanza. Huko Mwanza ndiko kuna

umeme, mimi nadhani kwamba tunaposema nchi hii ni moja, basi tuwe tunaangalia, kama Mwanza wana umeme basi huu mradi wa majaribio ya nishati ya jua vijijini si mngejaribia hata Kigoma jamani, kwa sababu Kigoma hatuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niwaeleze tu kwamba vile vyote ambavyo tunapewa na binadamu, Kigoma havipo, hatuna umeme, barabara, hatuna kila kitu, lakini jua tunalo na maji tunayo. Sasa mradi huu kwa kweli namwomba sana Mheshimiwa Waziri upelekwe Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee kukosekana kwa umeme Mkoa wa Kigoma. Nimeshaeleza mara kadhaa hapa kwamba Mkoa huu una matatizo makubwa ya ajabu na ni Mkoa ambao hauna umeme. Kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, umeme upo Makao Makuu ya Mkoa tu Mjini Kigoma-Ujiji lakini hata wenyewe ni umeme wa wasiwasi. Kasulu na Kibondo tunausikia tu.

Naomba nikumbushe tena Kasulu ni Wilaya iliyoanza mwaka 1919. Kwa hiyo, Kasulu, miaka 42 ya kipindi cha ukoloni ilikuwa gizani, miaka 43 leo hii ya kipindi cha Uhuru, Kasulu ipo gizani. Ni miaka 85 Kasulu ipo gizani. Wilaya ya Kibondo ni miaka 58 ipo gizani, miaka 15 wakati wa ukoloni na 43 wakati wa Uhuru. Hivi tunawatendea haki kweli wananchi wa Mkoa wa Kigoma, nauliza tunawatendea haki? Kwamba watu waishi miaka 85 gizani, mtu anaishi miaka 58 gizani, halafu mnasema nchi inakwenda pamoja na bado tunasoma kwenye kitabu hiki kwamba mwaka jana tu Vijiji hamsini na mbili vimepatiwa huduma ya umeme. Vijiji 52, sisi Makao Makuu ya Wilaya hayana umeme! Kwa nini tusisimamishe mradi wa kupeleka umeme Vijijini mpaka tuhakikishe kwanza Makao Makuu ya Wilaya zote yamepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba hii tunaona Makao Makuu ya Wilaya kumi na nne, ifikapo mwaka 2005, yatakuwa yamepata umeme. Kwa hiyo, zitakuwa zimebakia Wilaya nne ambazo ni Kasulu, Kibondo na nyingine mbili, sijui wenzetu wenye bahati mbaya ni akina nani, sitaki hata kuwajua. Lakini ni kwamba Kasulu na Kibondo mpaka mwaka 2005 tutakuwa hatuna umeme. Hivi naomba niulize, mnavyopanga kutekeleza miradi, mnachukua ramani ya Tanzania, ukishafika Kaliua unafunika, unasema kwamba huku siyo sehemu ya Tanzania, sijui ni Kongo, sijui ni Burundi au Rwanda! Ndio mpango huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ukisoma hata hapa *paragraph* ya 11 ukurasa wa saba alishasema ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, alisema: "Ili tusicheleweshe umeme wa Urambo na Kaliua, hili suala la kupeleka umeme wa Kigoma liangaliwe kama mradi mwingine kabisa." Halafu anaendelea anasema: "Aidha, Serikali hiyo ni Serikali ya Sweden imeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa kupeleka umeme wa gridi Mkoani Kigoma." Imeonyesha nia, nia yenyewe ya namna gani sasa? Sasa kila mwaka tutakuwa tunaambiwa tu, Serikali inaonyesha nia, Serikali ina mkakati, Serikali ina mpango, Serikali inajitahidi, ni kila mwaka tunaambiwa hivyo kweli? Jamani na sisi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali sana naomba kaka yangu Mheshimiwa Daniel Yona atusaidie, kwa kweli tumechoka. Sasa labda mnaweza kuelewa lugha nyingine kwamba kama mimi ambaye natokea Kasulu, tutishie kuwaloga au tufanyeje sasa? Maana kila mwaka tunawaeleza hivyo, lakini hakuna lolote lile. Mheshimiwa Waziri, mimi uchawi sinunui, kwa hiyo, nitaweza kuutumia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma uliwekwa kwenye eneo la *EPZ* miaka mitatu iliyopita. Nimeshauliza swali hapa Bungeni ni wawekezaji wangapi wameonyesha nia ya kuwekeza katika Mkoa wa Kigoma, hakuna mwekezaji atawekeza mahali ambapo hakuna umeme. Sasa hiyo kutuiweki Kigoma kwenye mpango wa *EPZ,* ilikuwa ni danganya toto au ulikuwa ni mpango gani jamani? Miaka 43 baada ya Uhuru bado mtu anadanganywa kwamba tunakuweka na wewe kwenye *EPZ* kweli kabisa? Sijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee machache kuhusu mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Katika Jimbo langu tunachimba sana chokaa. Chokaa imekuwa ikichimbwa tangu mwaka 1933, walianzisha Mapadri wa Kikatoliki mpaka leo uchimbaji uliokuwa unafanyika mwaka 1933 ndio huo huo, yaani wa kutumia sululu, sepeto, kubeba magogo kichwani, kuchota maji kwa ndoo au kwa mtungi yaani bado tunatumia zana duni. Sasa kila mara tunapopata hotuba ya Wizara hii tunaambiwa Serikali inaangalia uwezekano wa kuwapa mikopo wachimbaji wadogo sijui kuwawezesha, sijui kufanya nini, lakini wanawezeshwa vipi? Ni fedha kiasi gani inatolewa kwa ajili ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo wadogo ambao wanachangia kwa kiasi fulani kwenye uchumi wa nchi yetu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja. Hawa wakipata hizo hela wanawekeza hapa tofauti na hao wengine wakubwa ambao wakipata hela wanazipeleka nje ya nchi. Naomba tuwaangalie hawa ndugu zetu ambao ni wazalendo, ni wazaliwa wa nchi hii tuwawezeshe ili waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumalizia kwa kuiomba Serikali iangalie bei za vifaa vile ambavyo havitumii umeme. Vifaa vinavyotumia kama huu wanaita umeme nuru, vitu kama *solar equipment,* sisi Kigoma kabla ya vita ya Burundi tulikuwa tunapata *solar panel* ya kuwezesha kuwasha nyumba ya vyumba sita kwa shilingi 350,000/=. Leo hii nenda hapa Dodoma, kuna duka moja linauza vifaa vya namna hiyo, kifaa cha kuweza kuwasha nyumba ya vyumba sita, utakinunua kwa shilingi milioni 1.7. Huo uwezo wananchi wanao? Sasa Serikali ingechukua hatua kuhakikisha vifaa vya namna hii vinaletwa hapa nchini na vinaondolewa kodi ili wananchi waweze kuvipata na kufunga kwenye nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nisigongewe kengele ya pili, naomba niseme kama nilivyoongea kwenye hotuba ya Bajeti kuu kwamba naunga hoja hii mkono kwa shingo upande. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye hoja iliyo mbele yetu ya

Wizara ya Nishati na Madini. Naomba nianze kwanza kuwathibitishia uaminifu wangu na heshima kubwa niliyonayo kwa viongozi wote wa Wizara ya Nishati na Madini tukianzia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Kamishna Ndugu Mrindoko na Kamishna Ndugu Mwakalukwa. Nawaheshimu na kiwango changu cha heshima kitabaki vile vile baada ya hotuba yangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze sehemu moja tu kuhusu umeme wa Mikoa ya Kusini. Muda mrefu tumekuwa tunapiga kelele kutaka tupatiwe umeme wa gridi lakini haikuwezekana. Kwa bahati nzuri gesi ikagunduliwa Songosongo, gesi ambayo moja ya kazi yake ni kuzalisha umeme. Nasikitika kusema kwamba gesi ile ya Songosongo, sisi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara hatupati umeme kutokana na hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza kwamba *World Bank* walitoa pesa, zile pesa zikawa hazikutimia kukamilisha mradi, zikabidi zichukuliwe kwenda Dar es Salaam kuokoa hali ya pale wakati ule wa ukame. Hatuna pingamizi na hatua hiyo, Serikali tunaipongeza, lakini Mheshimiwa Waziri hakusema katika mradi huu wa Songosongo ziko fedha zilizobaki katika mradi ule zaidi ya shilingi bilioni 60, pia hakusema ni kwa nini fedha zile hazikutumika kupeleka umeme Kusini. Ameongelea za *World Bank* peke yake, hizi hakuzizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, azma imetimia, gesi Dar es Salaam imefika, hongereni sana, tumieni vizuri na Mungu awajaalie. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Sasa unawaapiza?

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, wala siwaapizi, lakini nasema tumieni umeme wenu, ninyi mstarehe sisi tubaki na kiza chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri, *page 23* ibara ya 37, anasema, naomba ninukuu: “Serikali ina matumaini makubwa kuwa mradi wa *Mnazi Bay* utafanikiwa.”

Mimi natoka Pwani, najua Kiswahili, kuwa na matumaini ni kwamba huna uhakika sawasawa. Lakini anaendelea: “Endapo matokeo ya uhakika wa gesi hiyo ya *Mnazi Bay* hayataridhisha, Serikali inakusudia kutumia njia nyingine ya kuwa na umeme wa uhakika katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Njia hiyo ni kujenga kituo kikubwa cha umeme Somanga Funga kwa kutumia gesi ya Songosongo na njia ya umeme ya kV 132 kupeleka umeme kutoka Somanga hadi maeneo husika.” Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba Serikali inakubali kwamba umeme wa uhakika ni umeme wa Songosongo. Hilo haikatai, lakini haitaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haitaki leo kufanya jambo la uhakika? Sababu zake ni kwamba lazima kwanza wabahatishe, washindwe, ndiyo wafanye la uhakika. Sasa hii sababu yake ni nini hasa? Wananchi wangu wanasema kwamba huu ni mpango wa makusudi wa kutucheleweshа.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kutumia mbinu kumcheleweshа mtu bila mwenyewe kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi naishi mbali na mzazi wangu, mzee ananitumia barua anasema mwanangu ninunulie viatu. Nikitaka nimcheleweshe, napeleka barua, namwuliza mzee namba ngapi? Kwa hiyo, kwa miezi miwili barua ipo njiani. Atanijibu namba nane. Namwuliza tena, rangi gani, miezi miwili mingine. Sasa sijakataa bado kumpa viatu, lakini navuta muda kwa mpango. Serikali twambieni ukweli tatizo la kupeleka umeme Kusini ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapoamua kupeleka umeme Kusini watapata fedha wapi? Naomba ninukuu majibu ya Serikali humu Bungeni: " Kwa kuwa suala la Songosongo nalo pia lilielezwa na Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu maswali kwamba kweli kwa *design* ya ule mradi wa umeme ambao unatolewa katika vituo vile vya njiani, ni Muhoro (kwao Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha), Bungu na njia ya kuja huku Dar es Salaam. Gesi nyingine inakuja Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli hizi zingine kama vile kutumia kwenye viwanda, kwenye nyumba hata pia kuzalisha umeme ndivyo mradi uliobuniwa tangu mwanzoni.

Kwa hiyo, nadhani la msingi kama bado gesi ipo ni kubwa kama inabidi kuelekezwa Kusini basi inabidi kutengeneza mradi mwingine upya. Haya ni majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni yapo katika *Hansard* ya tarehe 23 Juni, 2004 *page 198,* tushike lipi sasa? *Mnazi Bay* ya lini? Songosongo kwa nini hamtaki zile fedha zilizobakia zimekwenda wapi na kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wazima huambiana kweli. Sisi ni viongozi na wananchi wetu wametutuma hapa tuje tuwawakilishe tuseme maneno yao, mnapotujibu sisi mnawajibu na wao. Tuambiane yale ambayo kweli ndiyo mpango wa Serikali, lakini tunapozungushana tu *Mnazi Bay* matumaini, inawezekana, huenda, baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli *Artmus* wamepewa miezi 15 au 18 tuweze kupata umeme maana yake mwakani Desemba ni miezi kama 18 hivi kuanzia leo. Nchi ya Tanzania, *Artmus* hawana fedha hivi sasa, kwanza waweke gesi kwa kiasi gani, waambiwe ipo ya kutosha, warudi sasa wakaombe fedha au waandike mradi wao kwamba mradi wetu ni huu huu tupeni fedha, wapewe fedha waje wajenge miezi 18 kweli kweli kabisa hiyo ni miujiza! Mimi siamini hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine viko vijiji vikubwa vya miji midogo kwa sababu umeme huo wa *Mnazi Bay* kama utakuwa ni wa kweli utaishia Lindi hautafika Mchinga, hautafika Kitomanga, wala Kilangara wala Madawa. Sehemu hii tayari inawa-*cut off* *North* ya Lindi na *South* ya Kilwa.Kwa mpango huu sielewi utakuwaje umeme

wake. Umeme unaozungumzwa huu unapita Ikwiriri, Bungu, Muhoro lakini sijasikia humu Kipatimo wala Chumo maeneo ya Kilwa hapo hapo ambapo vile vile ni Miji mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine naomba niulize hivi sasa kuna tatizo la bei ya umeme wa *IPTL* kwamba ni ghali sana na Serikali inaombwa inunue ule mradi, lakini je, umeme huo kama utakuwepo wa *Mnazi Bay,* gridi ya Wilaya ya nane maana itakuwa Kilwa haimo bei ya umeme huo itakuwaje? Yaani umeme wa kutumia Lindi, Tandahimba, Newala, Masasi, Nachingwea, Rungwa na Liwale basi maana yake Tunduru hiyo haimo kwenye mradi wa *Mnazi Bay* huu, Songea kule haupo, huku Tunduru na Mtwara haupo, kazi kwako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema bei yake itakuwaje nina wasiwasi kama kweli utakuwepo kwa sababu ata-*invest* fedha nyingi sana mwekezaji na mtu binafsi angependa fedha yake irudi na angependa apate na faida kwa sisi peke yetu tutamudu kununua umeme huo? Nitaomba maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli yangu inaonyesha nimeunga mkono au sikuunga mkono, kauli yangu nilivyozungumza. Lakini nasema kesho nitaomba Mheshimiwa Waziri tena ajibu mwenyewe, najua Mheshimiwa Naibu Waziri ni mjanja, janja, ana kona kona itakuwa hatuelewani vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kesho maelezo ya kina sababu za msingi kwa nini Serikali mpaka sasa haitaki kupeleka umeme Kusini kwa gesi ya Songosongo? La kwanza, kwamba kwa nini fedha za Songosongo ambazo zilikopwa *World Bank* shilingi bilioni 60 zilizobakia zisitumike kupeleka Kusini kwa nini haikuwa hivyo? La mwisho, ni hili kwamba je, ule umeme utakaokuwepo kweli tutamudu kuulipia kwa sisi Mikoa miwili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba hotuba yangu nimemaliza. Nataka kusema kwamba kiwango changu cha heshima kwao kiko pale pale, nitaendelea kuwaheshimu kama nilivyowaheshimu jana na juzi, lakini naomba maelezo ya kutosha ili nielewe kweli kama nia ya kweli ya kupeleka umeme Kusini ipo au ni kiini macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi usiku huu. Zamani sana Waswahili walitutania sisi Wanyamwezi wakisema, mzigo mzito mpe Mnyamwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini usemi huu unaelekea kujithibitisha kwenye mambo mawili ambayo nitayasema usiku huu. La kwanza, madini ni bidhaa ambayo haipandwi, ni bidhaa ambayo haihamishwi, ni bidhaa ambayo haioti, ni baadhi ambayo huwezi ukaichukua ukaisafirisha ukaipeleka au ukaileta au ukaihamishia au kwa vyovyote vile. Bidhaa ya madini ukishachimba inakwisha kama vile unavyong'oa jino la

gego imetoka na hasa ukiwa na umri mkubwa, ukiwa mtoto uking'oa jino linaota tena lakini baadaye uking'oa halioti tena ndiyo madini. Kwa hiyo, madini ni bidhaa nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebahatika kwa kudra za Mwenyezi Mungu kuwa na utajiri wa madini *Alhamdulillah* tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia hivyo. Lakini cha ajabu haijabahatika kuwa na bahati nzuri ya viongozi ambao wanaona mbele kuangalia kwamba madini haya yatatunufaisha. Maana yake Mungu ni mjanja sana, Mungu anaweza kukupa lakini hawezi akakupa vyote. Ametupa madini lakini hakutupa ujanja wa kuyatumia madini hayo yatutajirishe, badala ya madini hayo kukutajirisha sisi wananchi tunaozungukwa na migodi au sisi wananchi wachimbaji wadogo wadogo au wananchi wa Tanzania madini hayo yameturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Mheshimiwa Waziri anajisifu kwamba madini yamekuwa yakiingiza fedha nyingi za kigeni, lakini ukiangalia fedha nyingi zinazoingia za kigeni siyo za nchi, asilimia 97 ya hizo fedha zinazoingia za kigeni ni za wawekezaji, sisi wanatupa asilimia 3. Sasa hapo utaringa kwamba umepata fedha, utaringa kwamba una kitu cha kukupeleka kwenye utajiri na kukuondolea umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo tumelipata kwenye madini ni juu ya sheria zetu sisi wenyewe na mikataba ambayo tunaingia, tumetunga sheria na tunaingia mikataba ambayo kwa kweli haina manufaa kwa Watanzania na kwa kutumia mikataba hiyo ambayo tumeingia hiyo, kwa kweli niseme tumeingia kwenye mkenge, badala ya kunufaika sisi wanaonufaika ni wawekezaji na ni wageni na hawana faida wala hawana uchungu na nchi yetu. Kwa sababu nia ya mfanyabiashara yeyote ni kupata faida tena faida maradufu au zaidi ya maradufu ndiyo anafurahi. Sasa sisi tumeingia kwenye mikataba, tumepitisha sheria hizi lakini manufaa yake kwa kweli hakuna. Mheshimiwa Waziri ametuonyesha muunganisho wa mapato ambayo yanaingia kwa *royalty* kwa nchi zingine mbalimbali tunakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi juzi nimejifunza kitu kimoja kwa kweli Serikali saa nyingine ina utata yenyewe kwa yenyewe na ndiyo maana nimetangulia kusema mzigo mzito mpe Mnyamwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wenye chokaa na nini walikuwa wamepata bahati ya kupata mrahaba, tumefurahia sana, lakini walipogundua katika mrahaba huo imo na Dhahabu na Almasi ambayo inatoka kwa Wanyamwezi wakasema hapana iondolewe. Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, alisema hapa hapa tena alisimama kwa urefu wake wote akasema Serikali imekosea, tangu lini Serikali inakosea? Mimi sijawahi kuona Serikali inakosea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichokifanya ni kutukumbusha sisi tunaotoka kwenye madini ya kwamba na mimi naomba ndugu zangu mnaotoka kwenye madini, Serikali imetukumbusha sisi tusiombe mrahaba ambacho Serikali imetukumbusha tuombe *minerals cess* na hiyo ndiyo tunaiomba tupeni *mineral cess,* toeni *mineral cess* kama ambavyo tunavyotoa *cess* kwenye mazao ya kilimo, tunatoa *cess* ya tumbaku,

pamba, pareto na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, watoe *cess* kwenye madini ndiyo ilichotukumbusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukumbuka hivyo nikakumbuka hadithi ya Bwana Yesu alivyokuwa duniani na wanafunzi wake aliwakuta wengine walikuwa wavuvi, wakulima na aliwakuta wengine walikuwa wafanyabiashara, walifanya naye kazi kwa muda wa miaka miwili au miaka mitatu, wanafunzi wake siku moja wakashtuka maana yake siku moja alikuwa anawambia kwamba bwana nyie tafuteni Ufalme wa Mungu kwanza mengine mtapata mara mia.

Lakini siku moja wanafunzi wake wakashtuka wakamuuliza sasa bwana mkubwa sisi vyote hivi tumeviacha, tumeacha nyumba zetu, tumeacha wake zetu, tumeacha nini, tutapata nini? Wananchi wetu kwenye maeneo ambayo tunatoka sisi yenye migodi wanatuuliza baada ya migodi hii yote ya Nzega, Kahama, Shinyanga, Tarime, Geita na kadhalika watapata nini au waambulie kupata mashimo? Hilo ni suala la msingi sana la Serikali kulijua na lazima ilijibu kwa kadri ambavyo kwa kweli inaingia katika mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara kwa mara inatwambia sisi tunaotoka kwenye maeneo yale kwamba nendeni mkazungumze nao, tuzungumze nao sisi wala hatuwajui, nyie mlioingia mkataba kwa nini hamkuzungumza nao katika mkataba moja kwa moja kufanya vitu ambavyo viko kisheria badala yake mnatusukumia sisi tuzungumze nao, tuzungumze nao nini? Wanatusaidia vitu ambavyo kwa kweli wala hatuvihitaji, unajua tu ukiwa maskini kwamba huna nguo, huna kandambili lakini siyo hitaji lako. Mheshimiwa Waziri hili limeturudisha nyuma na yeye akubali kwamba limeturudisha nyuma kwa sababu mikataba yetu haiko wazi, mikataba yetu siyo mizuri hasa kwa nchi, siyo mizuri hata kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata wachimbaji wadogo wadogo walikuwa na faida zaidi kuliko hata wachimbaji wakubwa. Ukiangalia miji ambayo ni ya wachimbaji. Kwa sababu mchimbaji mdogo akipata mazao yake aliyokwenda kuvuna kwenye uchimbaji utaona hata mji unachangamka, utaona hata mji unakimbia. Lakini wachimbaji wakubwa wapo wengine wanakaa Dar es Salaam wakati wanafanya kazi Kahama. Halafu gharama ile yote inakuja kwa wananchi kwamba uendeshaji ni mkubwa maana yake sisi hatukuzingatia kabisa maslahi ya nchi na hatukuzingatia kabisa maslahi ya wananchi wetu ambao tunawaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wakubwa mmewawekea na *centre* inaitwa *Tanzania Investment Centre(TIC)* ipo pale, lakini wachimbaji wadogo wako wapi, zamani kulikuwa na Kampuni ile ya *MEREMETA,* sasa hivi *MEREMETA* nayo haipo. Wachimbaji wadogo wanaenda wapi, hawapati mikopo, hawana mtu wa kuwasaidia, hawana mtu wa kuwashauri, hawana soko, hakuna soko la dhahabu, hakuna soko la almasi, hakuna soko la wachimba *Tanzanite.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunatengeneza *Tanzanite* lakini Kenya ndiyo wanaouza *Tanzanite* kuliko Tanzania. Sasa Mheshimiwa Waziri hili nalo linahitaji

ungoje sera hii inayosema inabadilisha hata hili la soko, hata hili la wachimbaji wadogo wadogo! Huoni huruma hata kwa wachimbaji wadogo wadogo, tumekaa tunawafukuza tu wakishavumbua machimbo hapo anakuja mchimbaji mkubwa anaangalia hivi na hivi, mnasema sijui sera yetu iko hivi, mchimbaji mdogo naye tunaihitaji tumwinue ili baadaye sisi Watanzania tuwe na wachimbaji wakubwa ambao zamani walikuwa wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi naomba sana, tafadhali Serikali basi iwe na masikio. Kama Bwana Yesu aliwaambia wale wanafunzi wake mtapata mara mia, basi waambieni na wananchi wanaokaa katika maeneo yenye madini ni asilimia ngapi watapata kwenye *cess,* waambieni kabisa waelewe kwa sababu hilo swali wanaliuliza na ni matarajio yao kwamba, Serikali inasikia na kama kusema tumeishasema. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kutwambia tusidai mrabaha tudai *cess* kama *mineral cess.* Hilo lilikuwa langu la kwanza la kuomba juu ya malipo kwa ajili ya maeneo ambayo yana migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuangalia wachimbaji wadogo wadogo kwani ndiyo wanaoinua miji hii na ndiyo raia ambao tunao. Wachimbaji wakubwa wakipata pesa hata siku moja hawawezi kujenga Nzega, hawawezi kujenga Singida, hawawezi kujenga Igunga lazima watahamisha vile walivyovipata wakajenga katika maeneo mengine. Lakini tukimwezesha mchimbaji mdogo mdogo ni mwananchi ataenda kwenye baa atakunywa pombe, atanunua nyama, nguo ndiyo uchumi wenyewe. Sasa nyie kila kitu kizuri wachimbaji wakubwa raha zote, *tax holiday* zote ni wachimbaji wakubwa, hawa wachimbaji wadogo wadogo ambao ndiyo raia wetu na ambao ndiyo wananchi wetu wameachwa bila chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia kwenye fidia, mwaka jana tumepiga kelele juu ya fidia, fedha zimeliwa pale Geita, tena zimeliwa na watu ambao wanajulikana kabisa, tumepiga kelele hapa hakuna mpaka tumehangaika sasa hivi ndiyo wamelipwa, lakini hakuna hata hatua yoyote iliyochukuliwa kwa wale waliokula hizo fedha. Hivi jamani sisi tutakuwa wageni wa nani kama hatuwapendi watu wetu wenyewe! Mheshimiwa Waziri, naomba hili aone aibu na kwa kweli ajitahidi kukimbia kama watu wengine wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, utakumbuka wewe ni Mbunge wa siku nyingi, kuna Wizara moja wakati fulani hapa ilikuwa inaongozwa ya Maji, alikuwepo Naibu Waziri wa Maji, alikunywa maji mpaka akazimia kwa sababu ya kelele za namna hii hii kama ambavyo zinapigwa kelele za namna hii hii kwenye umeme. Wale Waheshimiwa Wabunge wa zamani wanakumbuka ilitokea kelele zilikuwa namna hii hii. Wakati ule zilikuwa kelele za maji namna hii hii, lakini mimi namwomba Mheshimiwa Waziri yeye ameingia tangu mwaka 2000 kwa nini asichangamke? Kila siku tunakuona unaenda Ulaya, unafanya nini, changamka kama wanavyochangamka wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaki kumsifia bahati mbaya sijui kwa nini amekuja Mheshimiwa Edward Lowassa, humu nataka niseme wazi tulipiga kelele wakati ule kuhusu maji, lakini leo watu wa Kanda ya Ziwa tunafaidika na maji ya Ziwa ya

Victoria kwa sababu ya mtu mmoja amethubutu, Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Edward Lowassa, amethubutu maji ya Ziwa Victoria yameshuka. Sasa hivi Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo anatuambia Wilaya 50 mpaka mwaka 2005 zitakuwa hazina matatizo ya maji, amethubutu. Sasa Waziri wa Nishati na Madini hizi kelele zimekutosha, thubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yanahitaji tu uwe jeuri jeuri. Mheshimiwa Rais mwenyewe kawambia Mawaziri wote wa miavuli hakutaja kwamba baadhi ya Mawaziri ndiyo wa miavuli, kasema wote ni wa miavuli. Sasa Waziri wa Nishati na Madini kwa nini na yeye asiwe wa miavuli athubutu, atafute fedha kama wanavyotafuta wenzake wanapata. Kwanza, mimi namfurahia sana katika Mawaziri wote wanaovaa suti nzuri yeye ni wa kwanza, atafute fedha atapata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yetu ahadi ya Mheshimiwa Waziri ameshatuelekeza mahali ambapo ametuwekea mabaya. Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekuja kwangu kule Ndala na Naibu Waziri amekuja mpaka Ndala na wananchi wa Nzega walimpa koroboi. Nzega ilipata umeme miaka ya 1980 kweli! Lakini leo Nzega ina vijiji 150 ni vijiji sita tu vyenye umeme katika vijiji 150 miaka 20 iliyopita. Nzega imepitiwa na gridi ya umeme inayokwenda Tabora imepita juu, gridi ile imepita katika vijiji 15 au 20 hivi waangalia umeme miaka 20 iliyopita. Sasa Mheshimiwa Waziri amekwenda Ndala, ameahidi atawapatia umeme na umeona jinsi ambavyo unasukwa sukwa hapa juu ya suala la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Waheshimiwa Wabunge wanahitaji umeme. Je, umejiandaa vipi? Mimi katika hotuba yake sikuona hata sehemu ambayo ameeleza amefanya *feasibility study* ya kuweka umeme katika nchi nzima inahitaji shilingi ngapi hajasema? Angesema angalau tungeweza kusema kwamba huyu bwana kweli atakuja kuweka umeme baada ya miaka kadhaa. Angalia watu wengi ambao wamefanya haraka haraka ya kuhakikisha kwamba wanaleta huduma, watu kama wa *Celtel* na *Vodacom* wanaenda mpaka vijijini. Gharama ya kuweka nguzo ya *Vodacom* au ya *Celtel* kama hesabu zangu haziko sahihi basi mtanisahihisha ni karibu shilingi milioni 300 lakini wanaenda mpaka vijijini.

Sasa kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini umemem hauendi vijijini kwani wananchi wa vijijini wana tofauti gani na wananchi wengine kama *Vodacom* na *Celtel* wanawekeza mpaka vijijini, kwa nini Serikali haiwekezi umeme katika vijiji? Umefika wakati Serikali iamue kwa makusudi kabisa kuwekeza umeme katika vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu ni machache mno na nataka tu niongee haraka haraka. Lakini kikubwa ambacho naomba niwaeleze ndugu zangu wa Wizara hii hasa upande wa ugavi wa umeme *TANESCO*. Jamani inaelekea siwezi kuungana na mwenzangu alivyosema kwamba labda kuna baadhi ya viongozi wanakuwa hawaelewi matatizo ya vijijini hasa, lakini vijijini jamani ndiyo kwenye matatizo kuliko Mijini na hivyo vijiji huwa vinakuwa na mazingira yake.

Leo ninawajibika kuhakikisha kwamba ninamshukuru na kumsifia sana au kuisifia sana Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa yale yote ambayo imeweza kuyafanya kwa nia na madhumuni ambayo imeweka kwa ajili ya Kisiwa cha Mafia jinsi hali tuliyonayo, leo Mafia tunaona tumekombolewa, *Vodacom* tunaongea na Mheshimiwa Waziri akathibitisha na sasa tunasubiri uwanja wa ndege pamoja na gati na ninaamini kwa jitihada za Wizara wakati wowote sasa hivi shughuli zitaendelea. Kuna watu wanashughulikia huko, lakini Mheshimiwa Waziri mwenyewe atasema mbele ya safari huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Kisiwa cha Mafia jamani inatisha na pale panapokuwa giza basi huwa inazidi. Leo mashine inayofanya kazi ni moja tu kati ya mbili, hii mashine leo ina takriban mwezi moja toka imewashwa haijazimwa mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, wakati wowote ule kama itatokea *breakdown,* ina maana Mafia tutakuwa gizani sijui kwa kipindi cha miaka mingapi.

Kwa hiyo, mimi sina zaidi isipokuwa naomba sana Wizara ya Nishati na Madini mtuangalie hali ilivyo Mafia. Mkurugenzi wa *Net Group Solution* pale wanakusanya mapato mengi sana, hebu watoe kidogo hizo fedha ambazo wanazikusanya kuhakikisha kwamba mashine ya pili ile ambayo iko pale haraka iwezekanavyo wahakikishe kwamba inatengenezwa ili iweze kusaidiana na hii nyingine kabla halijatokea tatizo lingine kubwa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kwamba kuna mpango wa kutuletea mashine nyingine ambayo inahamishwa kutoka Mtwara ni mashine ambayo haifanyi kazi. Lakini sisi tunasema tunaitaka hiyo mashine na itakapofika ili ziweze kuwa tatu zitengenezwe na pale ziweze kusaidiana. Wazee wangu, hali ya Kisiwa cha Mafia jamani inatisha.

Kwa hiyo, kutakapokuwa giza hata huo mtandao tunaoringia ukija kuzimika kwa maana yake ndiyo tutazidi kuwa katika hali mbaya, tuoneni huruma jamani tuko Kisiwani kule. Jinsi mnavyotoa kipaumbele kwenye umeme na sisi Mafia tunashukuru *Alhamdulillah* umeme tunao, lakini hiyo mashine moja leo kama itaharibika patakuwaje pale Kisiwani? Hali ya hospitali itakuwaje, ikitokea dharura tutafanya nini kwa wale wananchi wa pale, tutawajibu nini na tutasema nini mbele ya Mungu hapo mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Wizara ikiangalie sana Kisiwa cha Mafia kwa jicho la huruma kabisa. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri tunawaombeni sana, chonde chonde jamani, mkiangalie Kisiwa cha Mafia tuko wapweke, tumetengeka, hatukutaka wenyewe, lakini ndiyo umbile la Mwenyezi Mungu alivyoumba dunia yake na sisi ndiyo ikabidi tuishi pale Mafia na sidhani kama watu watatoka. Tunakuombeni sana mtuonee huruma watu wa Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu bei ya mafuta. Bei ya mafuta jamani Tanzania inapanda sana, naomba Wizara hii iweke mikakati mizuri tu isijaribu kukaa na kusema kwamba biashara ni huria basi watu watakaa na kupanga na kufanya hivi. Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza mengi tu kwamba wanafuatilia wanafuatilia, lakini watafuatilia mpaka lini wakati kila siku zinavyokwenda bei ya mafuta inapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie nchi za wenzetu jirani Rwanda na Burundi, mafuta yanatoka nje kama yanapotoka kwetu sisi, yanafika Dar es Salaam wanaweka pale kuna *storage* tunapata sisi, yanapita kuna ushuru japo chembe ya fedha tutapata, kuna usafirishaji mpaka Kigali au Bujumbura au Gitega. Lakini ukiangalia bei ya mafuta ya Rwanda na Burundi haiwezi kulinganishwa na bei ya mafuta ya Tanzania ilivyo tunamkomoa nani na nani ambaye anaubeba mzigo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunasema kwamba watu walime, hata wakilima hayo mazao yatafika vipi sokoni? Leo gunia moja la nazi kulitoa Kisiju kuja Dar es Salaam wanalipia shilingi 5,000/= kwa sababu ya upandishaji wa bei ya mafuta. Kitu kilichokuwa juzi juzi tu hata mwaka mmoja na nusu bado ilikuwa shilingi 2,500/= asilimia 100 inapanda ya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuwaonee huruma kwa sababu mzigo wote yanapopanda mafuta anayobeba mzigo huo ni mwananchi hasa wa kijijini ndiyo yanayompata, mazao yake yanakuwa tabu kufika Mjini, hapati soko zuri, lakini pia yeye ndiye anayepandishiwa pia hata chakula kile cha kununua ama iwe sukari au kitu kingine au mchele basi atavinunua kwa bei ya juu, hayo yote ni shauri ya upandishaji wa bei ya mafuta.

Kwa hiyo, tunaiomba Wizara japokuwa biashara huria, lakini Serikali nayo ifikirie na iwe imara siyo iachie holela tu maadam biashara huria wanavyotaka wafanyabiashara ndiyo tuwafuatishe, lakini lazima tuwe stable na sisi, tusema hapa jamani mnazidi mno wacha tufanye hivyo. Pale ndipo tunapokwenda na ninaamini hata wananchi na wenyewe watakubali kwa yale maelezo mtakayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, narudi kwenye umeme, yale yale ya mafuta. Umeme Tanzania jamani ni ghali sana halafu pia huo huo umeme anayebeba tena mzigo ni nani, ni yule mwananchi wa kawaida. Matokeo yake wananchi wanashindwa kutumia vifaa vya umeme hali inazidi kuwa mbaya katika misitu yetu. Mazingira ya nchi yanaharibika panda ndege kutoka Dar es Salaam ukielekea Mafia, ukanda mzima wa Wilaya ya Mkuranga sasa unaelekea kuwa jangwa kwa sababu ya uchomaji mkaa. Sasa

tunatengeneza nini? Tunatengeneza nini au tunabomoa nini? Tunachokilinda ni nini au tunafanya kitu gani?

Kwa hiyo, hili jamani mlifikirie, wachomaji mkaa wanaisababishia nchi yetu hii kuwa jangwa na hii ni kwa sababu ya wananchi wengi kushindwa kutumia umeme kwa sababu ya kuwa ni ghali mno. Kwa hiyo, tunaomba hali hii muiangalie na huyu mwananchi atakapoweza kupunguziwa huu mzigo, basi mimi naamini hata hawa wachomaji mkaa watapungua. Kwa sababu watu wengi watakuwa wanafaidika kutokana na matumizi ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba gesi ya Songosongo imefika, naamini hali itakuwa nzuri, lakini hata hivyo isije ikawa chanzo cha gharama kubwa kwa usafirishaji wa gesi hii, isije kuwa badala ya kupungua ikawa tena tunaangalia gharama za mradi huu ni fedha nyingi sasa tutafute kiwango cha kuweza kupandisha na hizi asilimia tano tano walizopewa uwezo wa Bodi ya *TANESCO* kuweza kupandisha. Bahati mbaya hatukuambiwa, wanapandisha asilimia tano hizi kwa kiwango cha miezi gani? Kwa sababu wanaweza wakakaa leo wakasema tunapandisha asilimia nne, baada ya mwezi mmoja asilimia tatu. Baada ya miezi miwili asilimia moja. Ukitahamaki kwa kigezo gani mpaka inafikia wao wanakuwa na nafasi ya kuweza kupewa kuchangia yaani kuongeza bei kwa asilimia tano? Hili naomba tu mtufafanulie ili tuweze kuelewa. Lakini jamani umeme ni ghali mno na matokeo ya umeme kuwa ghali, hali ya mazingira ya nchi yetu inaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nililokuwa nataka kuchangia, linahusu Idara ya Madini. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mzingira na tumetembelea maeneo mengi sana kabisa kama vile maeneo ya Amani, Milima ya Usambara, Mererani na sehemu nyingi. Hebu nendeni mkaangalie kwa hao mnaowapa vibali, wachimbaji wadogo wadogo jinsi wanavyoharibu mazingira. Jamani ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Mazingira, nasema katika Idara au Wizara ambayo ni adui mkubwa wa mazingira ya nchi yetu basi ni Wizara hii ya Nishati na Madini hasa Idara ya Madini ni mbaya sana. Siwezi kusema ni mbaya, tunapata mirabaha hiyo ya asilimia tatu. Lakini hebu angalieni hao watoa vibali jinsi wanavyotoa. Kwa mfano, tumekwenda Amani, jinsi walivyokwenda kuharibu vyanzo vya maji, sijui vitarekebishika vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokiomba Wizara inapotaka kutoa vibali kwa na ni kweli wananchi wanahitaji wapate pesa. Lakini kabla hawajatoa vibali lazima washirikiane na Idara husika za Mazingira hasa *NEMC.* Nendeni mkapate ushauri kwao ili waweze kukupeni yale ambayo wao wanayo na hata kama patachimbwa haya madini, patachimbwa kwa uangalifu na kwa nia njema, wananchi watapata na nchi itakuwa haiathiriki.

Kwa hiyo, naomba sana huu utoaji ovyo wa vibali hasa kwa wachimbaji wadogo wadogo muuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia mema hao wachimbaji wasifikirie labda tunataka tuzuie. Lakini pale walipovamia Milima ya Usambara kwa siku tatu tu, hasara yake sijui hata kama mngeambiwa ninyi Idara mlipe fidia jinsi uharibifu ulivyotokea nadhani marupurupu yote mliyoyakusanya Geita pamoja Bulyanhulu, isingeweza kufidia pale, jinsi walivyoharibu wale na sijui nyie kama Wizara au Serikali ilipata nini?

Kwa hiyo, hili nilikuwa tu nitoe mawazo yangu kwa upande wa mafuta, umeme na utoaji wa vibali. Lakini chonde chonde jamani Kisiwa cha Mafia na giza, tunaomba pesa hizi zipatikane, tutengenezewe mashine zetu ziweze kusaidiana katika kuzalisha umeme pale kisiwani kwa sababu tukikosa maendeleo yatakuwa duni na kwa sasa Hoteli nyingi za Watalii zinajengwa. Mtalii hawezi kuja pale akalala kwa kutumia kibatari. Kwa hiyo, tunaomba sana mliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima zote naunga mkono hoja ya Wizara hii, lakini naomba sana tufikiriwe suala hili la umeme Kisiwani Mafia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hauwezi kutosha kwa mtu mwingine kuchangia. Sasa hapo ndiyo tumefika mwisho wa shughuli za leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 15 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*